**OORDHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

| | |
|---|---|
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |

| | |
|---|---|
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh’d Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Ishirini na Saba - Tarehe 22 Juni, 2015**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa heshima kubwa naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Thalathini Mia Tatu na Sitini Milioni na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti):** Mhe. Spika, kwa idhini yako na idhini ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, naomba kuweka mezani Maoni ya Kamati ya Wenyeviti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Thalathini Mia Tatu na Sitini Milioni na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2015/2016**
**Wizara ya Fedha**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali:** Mhe. Spika, awali ya yote naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo na sote hatuna budi kumshukuru Mola wetu aliyeweza kutupa pumzi hizi ambao tumeweza kuwepo hapa pamoja na wenzangu.

Nichukue nafasi hii kukushkuru Mhe. Spika, kwa heshima zote na taadhima kupata nafasi hii katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ambapo ulianza Alhamisi; Mwenyezi Mungu atujaalie atupe pumzi na nguvu ya kuweza kukamilisha hali hii.

Mhe. Spika, mimi nichukuwe nafasi hii leo adhimu mbele yako kwa kuweza kupata nafasi hii kwani imani yetu au imani yangu kwamba bajeti hii tunafikia ukiongoni, kwamba tunakwenda kwenye lala salama. Kwa hivyo nishukuru wenzangu wote, lakini nikushukuru wewe na Naibu Spika, pamoja na wenyeviti Mhe. Mahmoud na Mhe. Mgeni pamoja na wasaidizi kwa kuweza kutuwezesha sisi Wajumbe kwenda katika njia ya busara na hekima. Vile vile Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu akujaalie akupe afya, akupe nguvu kwa hekima zako na usikivu wako kwa kutuendesha sisi wawakilishi katika kuisaidia nchi hii. Kwani sote tumekuja humu ndani kuwatumikia wananchi bila kujali rangi, kabila au dini. Nachukua nafasi hii kushukuru sana.

Mhe. Spika, nianze kwa kuchangia hii bajeti ya Wizara ya Fedha ambayo imesomwa na kaka yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee; Waziri wa Fedha pamoja na wasaidizi wake aliokuwa nao. Nishukuru kamati iliyosoma na Mhe. Hija kwa utulivu pamoja na wizara yenyewe.

Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze Wizara ya Fedha na watendaji wake wote; kwa kweli ninaweza kuthubutu kusema hekima ya Wizara ya Fedha na watendaji wake wote imeweza kufikia malengo mazuri sana katika ukusanyaji wa mapato.

Nikianza na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wahasibu wa Wizara ya Fedha, *ZRB*, *TRA, Income Tax*, *ZIPA* na Taasisi zote zilizokuwepo, mimi ninaamini wenzetu hawa wana uwezo wa kufanya mapato yaweze kuendelea.

Mhe. Spika, watendaji hawa wote niliowataja katika Taasisi zote katika ukusanyaji wa fedha wana hekima, wana busara; changamoto iliyokuwepo ni *communication.* Mimi naamini kila wakijikusanya kwa pamoja basi neema itakuja. Lakini kwa kweli wamevuka malengo. Tumeona na ni wazalendo katika ukusanyaji wa mapato. Mimi nataka kutoa wito kwa wafanyabiashara nikiwemo na mimi Raza mwenyewe kwamba kubwa zaidi ni kulipa kodi zilizokuwa zinastahili ili zisaidie jamii.

Mimi ninafikiri Mhe. Spika, bado wafanyabiashara wana kazi kubwa ya kupewa elimu kwa sababu kodi tunazozitoa au zinazotolewa na wananchi mbali mbali ndizo zinazokuwa zinasaidia jamii katika mambo ya maji, barabara, umeme, uvuvi, kilimo, nk. Kwa hivyo haya yote yanatokana na ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, sina zaidi ya kusema kwamba hizi taasisi zinafanya kazi kwa bidii sana na mimi ningeliomba bado elimu inahitajika katika taasisi hizi. Nataka nimwambie Mhe. Waziri wa Fedha; nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa usikivu na kuwapanga vyema hawa watendaji kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha katika kusaidia tatizo hili.

Mhe. Spika, hakuna mkamilifu, sote tuna mapungufu hiyo ni kazi ya Mwenyezi Mungu lakini imani yangu hawa wenzetu kila wakipewa nguvu na nyenzo za kufanyia kazi basi mimi ninaamini watavuka malengo yanayotakiwa.

Mhe. Spika, nije sasa katika kusaidia katika ukusanyaji wa mapato. Kama tunavyoelewa bajeti yetu imesomwa, kwa masikitiko makubwa bajeti hii ilipokuwa ikisomwa imepata athari kidogo na athari yenyewe kama mimi mchumi ninayefahamu kidogo uchumi tumeathirika kutokana na kushuka kwa bei ya dola. Inabidi sasa Serikali kupitia taasisi hizi itizame nafasi gani zile ambazo zinaweza kusaidia katika ukusanyaji wa mapato ya ziada.

Mhe. Spika, ninashukuru Serikali imepandisha kima cha chini cha wazee kuwapa fedha hizi shilingi 60,000 kama sikosei, lakini bajeti hii tayari ishaathirika kwa sababu bajeti ilipotangazwa Mei, tuko Juni, asilimia kama sikosei zaidi ya 20 kutokana na kushuka kwa dola basi imekuwa tumeathirika. Sasa mapungufu hayo tumo ndani tayari Serikali ishaathirika, sasa hata kuwapandishia wazee hawa pamoja na mishahara ambayo tunategemea bado hali hii haijatupa muangaza Zanzibar na bajeti yetu kusema kwamba imekidhi mahitaji. Kwa hivyo bajeti imefanya, mishahara imepanda, *devaluation* ya dola.

Sasa Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kutoa mawazo ili tuweze kutafuta mapato mengine isaidie kuziba hili pengo ambalo tulilokuwa nalo. Bado tunakwenda lakini hali tete kushuka kwa thamani ya dola. Kwa hivyo lazima tutafute vyanzo vyengine *extra* vya kuweza kusaidia mapato haya angalau yaongezeke. Hawa wenzetu *TRA*, *ZRB* wote watavuka malengo, lakini malengo watayovuka wote hawa *ZIPA* bado kunakuwa na upungufu.

Mhe. Spika, nianze na kutoa ushauri ili Serikali itupe mapato. Fungu Mbaraka pale kuna vivutio vya uchumi na kisiwa cha Fungu Mbaraka kimekuwa ndani ya Zanzibar tokea Oktoba, 1890; kumbukumbu ambazo tunazozisoma na bahati nzuri katika 1958 mimi nilikuwa sijazaliwa, kisiwa kile kilipewa uchumi maalum kwa sababu ni kisiwa cha ndege, kuna ndege maalum pale.

Sasa Mhe. Spika, kwa kuwa pale kuna biashara, kuna mambo ya uvuvi, *of course* mimi ningelifikiri Wizara ya Fedha ingelikaa ikatizama jinsi gani ya kuweza kuongeza mapato. Tukianza kutoa leseni kwa sababu Fungu Mbaraka kama nilivyosema liko katika kisiwa cha Zanzibar na lipo katika ardhi ya Zanzibar, tukajaribu kutizama namna gani ya kuwahimiza watalii kwenda kutembelea pale, ili tukawa tunapata mapato ya kuweza kujiendesha. Kwa hivyo pale kuna mambo ya *fishing*, kuna ndege maalum ambao kwa eneo letu la Afrika mashariki nzima na nje hawapatikani.

Mhe. Spika, kwa hivyo mimi nilitaka niiombe Wizara ya Fedha ione jinsi gani ya kuweza ku-*express* pale ili watalii waende, wananchi wakenda, ikawa mapato yameongezeka. Kwa sababu tukitoa leseni sisi tutakuwa tumejikusanyia zaidi, hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili katika kusaidia mapato haya tukija katika suala la kumbukumbu Zanzibar tuna hazina kubwa sana ya kumbukumbu zetu na kumbukumbu hizi zinaweza zikatusaidia katika kukusanya mapato yetu kwa watalii na wazanzibari na watanzania. Hapa kulikuwa na changamoto mimi ninashukuru Serikali ya Oman ambayo inaongozwa na Mfalme Qaboos kwa misaada mingi kwa upande wa Zanzibar na kwa kweli wameonesha nia nzuri sana katika kipindi kifupi.

Sasa Mhe. Spika, pale Makumbusho Kilimani tulikuwa tunaambiwa kuna *documents* zinafungiwa ndani ya sanduku, sasa katika kusaidia ili kupata mapato zile *documents* zikajengewa sehemu maalum badala ya kufungiwa ndani ya sanduku ili wazanzibari, watanzania na watalii wakaisoma historia ya Zanzibar na ukusanyaji wa mapato.

Tuwaombe ndugu zetu wa Oman, Sharjah, Ras al-Khaimah; tuna mashirikiano. Leo historia Zanzibar unakwenda kuikuta Uingereza, Ujerumani, Ufaransa ambayo sisi ndio wenye hazina, ndio wenye asili. Kwa hivyo ingetafutwa maalum sehemu zikajengewa *archives* tukawaomba ndugu zetu wakajenga *archives* ikawekwa wazi historia ya Zanzibar.

Kuwekwa historia wazi itaondosha vile vile udokozi wa nyaraka. Kwa sababu wananchi wapo na ile ni historia, ni vizuri ikasaidia mapato ya nchi pale pale na tukawaomba ndugu zetu wa Oman tukakusanya kwa pamoja historia.

Mhe. Spika, Zanzibar ina historia kubwa sana katika Afrika nzima na Bara la Afrika. Kwa hivyo hiyo ni nyenzo ambayo inaweza kutusaidia mapato katika kuleta faida na kuziba mapengo haya yaliyojitokeza katika bajeti hii kuliko kwenda kufungiwa ndani ya sanduku ambapo inakuwa haina tija. Wazanzibari tunashindwa kuijua historia. Mhe. Spika, mimi ningelimuomba Mhe. Waziri kaa na taasisi zako ili kuzidisha mapato.

Mhe. Spika, jengine vile vile suala la fedha, hizi taasisi nyingi za *Tigo, Vodacom, Zantel* ni taasisi ambazo zinasaidia sana kwa upande wa Zanzibar. Mimi ningelimuomba Mhe. Waziri kupitia Wizara ya Fedha, *ZRB* ili kuona jinsi gani mapato haya yasivuje. Tumeshuhudia taasisi mbali mbali zinachapisha kadi za simu mfano zikishakuchapisha matokeo yake kunakuwa na *another printer* kwa kadi ile ile kuongezewa nambari na matokeo yake wananchi wanapokwenda kufuta ile wanakuta kadi ile ishatumika.

Sasa mimi ningelitoa rai kwa wananchi wenyewe wakikuta tatizo kama hili ni kulitolea taarifa kupitia Serikalini, kuona kwamba hizi fedha ambazo zinapotea na wachache ambazo wanatumia kwa faida yao, tuone jinsi gani tunaweza kukabiliana nayo katika mazingira haya ya uchumi wetu.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa ninaulizia tu hili suala la Tume ya Pamoja. Mimi ninaamini Waziri wa Fedha na watendaji wake ni watu wenye hekima, wafuatiliaji. Ili Tume ya Pamoja ya Fedha, kunaandaliwa mjadala wa sheria ya *gas* na mambo mengine wenzetu huko Bara. Sasa ningeliomba Mhe.Waziri wa Fedha akatwambia hii Tume ya Pamoja ya Fedha iliyokuwepo na imo ndani ya Katiba tuliyokuwa nayo hivi sasa, imefikia hatua gani na vikao vingapi vimeweza kusaidia kutatua changamoto na mambo mengine. Kwa hivyo mimi ningelimuomba Waziri wa Fedha atakapokuja kutusaidia vitu hivi vyote kwa pamoja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kuna vitu vyengine havihitaji na Katiba iliyokua imependekezwa, kuna vitu ambavyo tunaweza kuvifanya kutokana na historia.

Mhe. Spika, nasema hata hili suala la Fungumbaraka halihitaji Katiba Pendekezwa, hiki ni kisiwa ambacho kipo tunaweza... na nilisahau kuongezea kwamba hivi sasa wenzetu Bara wanatoa leseni ya *sports fishing*. Sasa kitabu hiki tunakwenda nacho lakini hakihitaji kwamba mpaka ile Katiba iliyopendekezwa kwa sababu ni nchi yetu sisi Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kwa kumalizia niombe Wizara hii ya Fedha kwa kweli imefanya kazi lakini mashirikiano, na vile vile niiombe wizara hii wenyewe ikaona kwamba hii miradi iliyokuwa tayari ikashirikiana na taasisi zinazohusika kuona changamoto gani zilikuwepo ili kusaidia sehemu yetu nzima hii ya ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, mimi nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa msamaha waliotoa kwa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani katika chakula. Lakini nimuombe tu Mhe. Waziri aendelee na hali hii ili kuwapunguzia makali ya maisha wananchi.

Mhe. Spika, kwa kweli hali ya wananchi wa Zanzibar maisha yamekuwa magumu sana, ni jambo ambalo linasikitisha, linatusikitisha sisi sote. Kwa hiyo nimuombe Waziri wa Fedha hili suala la kuendelea hali hii ya dola tunayokwenda nayo, ni kwamba hapa tunayo Benki Kuu, msaidizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Kwa hiyo, mimi nimuombe Waziri wa Fedha angalau kuwepo na utamaduni hizi benki zilizokuwa hapa kama Benki Kuu ya Tanzania ni benki ya Muungano…

**Mhe. Spika:** Unazo dakika tano.

**Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: ...**huyu Gavana Mkuu awe anateuliwa na Marais wawili lakini kipindi chote hiki hatujamuona Gavana Mkuu wala hii benki kutwambia au kutukusanya kuona changamoto gani wafanyabiashara wa Zanzibar wanakabiliana nazo.

Mhe. Spika, ile benki pale imekaa kama *white elephant* haina msaada wowote. Kwa upande wetu sisi kama uchumi, tunayakuta tu magari yanaingia ma-VX pale lakini sijaona tija ya benki ile tawi la Zanzibar kuona imenufaisha vipi Zanzibar na hakuna mpaka leo aliyekuja Gavana au Naibu Gavana akakutana na wafanyabiashara, wenye viwanda, wakulima; kuona jinsi gani waweza kuuliza masuala yao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha mimi ningelikuomba ni mtu msikivu sana pamoja na watendaji wako tuone jambo gani tunaweza kusaidiana.

Mhe. Spika, nakushukuru sana, nawashukuru wenzangu wote, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Uzini kwa kuweza kunipa nafasi hii katika kipindi cha miaka mitatu, labda nimwambie tu Mhe. Waziri wa Fedha nitamke rasmi. Ni kwamba katika kipindi changu cha miaka mitatu nimepokea pesa za jimbo milioni 10, ambazo nimezitumia kwa wananchi kwa kununulia vifaa, nikapata milioni 15, nimenulia madawa kuwakabidhi wananchi kama Mwakilishi wa Jimbo; pesa za wananchi nilizokuwa nimezipokea na nimezikabidhi mbele ya wananchi kupitia Rais Mstaafu kwa kuwasaidia vitu vyote vya afya.

Mhe. Spika, juzi nimepewa milioni 15, za wananchi, si zangu, nimezitumia katika kuwasaidia watoto wetu waliokuwa na hali ngumu ya maisha katika kujiendeleza kielimu, na afya.

Mhe. Spika, pesa hizo ndio nilizopata maana yake fimbo ya Mungu haina sauti, nimekaa hapa pesa ambazo nilizopewa ni za wananchi ndio nilizozitumia na Mhe. Waziri wa Fedha naomba uniongezee kama kuna pesa za jimbo nikakabidhi.

Wadi tatu zikiwemo ya Bambi, Uzini pamoja na Kiboje zilipata fedha hizi. Kwa hivyo, nataka nimwambie tu Mhe. Waziri wa Fedha pesa za wananchi nimezitumia katika njia ya *siratulmustakeem* pamoja na sehemu mbali mbali nilizokuwa napata mashirikiano.

Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru sana, nawashukuru wenzangu wote wawakilishi kwa mashirikiano mazuri tunaomba Mungu kila aliyejaaliwa basi arudi kuendeleza yale malalamiko na kuwatumikia wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Mjumbe mwengine kuchangia na leo tunao wageni ambao ni vijana wetu wapo pale juu

wamekuja kwa ajili kujifunza mambo yanavyoendelea katika chombo chetu hiki. Wageni hao, nikimtaka Mhe. Gavu atulie.

Wageni hao ni wanafunzi jumla yao ni 46 ikiwa ni pamoja na wanafunzi 40 na walimu wao ni 6. Kwa hiyo wageni nilionao ni jumla ya wageni 46 na wanaongozwa na walimu wao Bi. Khadija Abdalla Juma na Mwanajuma Amour, niwaombe wageni wetu hao wote; wanafunzi na walimu wasimame ili wasalimiane na Waheshimiwa Wajumbe. Ahsanteni na karibuni sana. (*Makofi*)

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, na mimi kwanza nakushukuru sana asubuhi ya leo kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha ndugu yetu, mwenzetu, mheshimiwa mahiri sana kuziba miaya ya kodi na kuweza kuwasaidia wananchi wavuja jasho wa nchi hii. Hilo nampongeza sana tena sana, sana, sana.

Mhe. Spika, lakini nimpongeze sana Mhe. Raza kwa kuwapelekea dawa wananchi wa Uzini. Hilo nampongeza sana kutokana na hali halisi ilivyo, lazima mheshimiwa awapelekee dawa wananchi na hasa kwa kuwa wananchi wetu huwa wanaumwa mara kwa mara, amefanya jambo la msingi sana.

Mhe. Spika, mimi niingie katika mchango kwanza kabla sijachangia nina mambo mawili makubwa, na haya nimeona niyaseme. Jambo la kwanza mheshimiwa nakubaliana na Mhe. Waziri katika harakati za kuinua uchumi, hilo mimi sina mjadala nalo tena nakubaliana kabisa. Lakini hali ya uchumi uendane na watu ambao waliokuwa na uchumi duni sana, watu duni ni wa aina gani ambao wanashindwa kupata maendeleo?

Niseme ni mara nyingi sana nilikuwa nalisema Mhe. Waziri kwamba tujaribu kutafuta mbinu za kuwawezesha kina mama, kuwafungulia benki. Hili suala nilisema sana kwa wewe naamini unaweza sasa hivi, tunakwenda ukingoni na unataka kuacha jina la kuonesha jinsi gani kina mama unavyowapenda kwa kuweza kuwawekea kitega uchumi ambacho kitaweza kuwasaidia katika maisha ya baadae.

Mhe. Spika, ulimwenguni sasa hivi kina mama na wao wanapewa kipaumbele na hasa katika kuwainua maisha yao *for example,* hapa hapa Bara wenzetu tayari benki hiyo ipo. Lakini kutokana na hali halisi naamini utanambia uhalisia kwamba hali halisi sasa hivi ni ngumu, sina tatizo nalo. Lakini *at least* naomba sana basi tuwafungulie dirisha dogo la kuweza kupata mikopo iliyokuwa ina unafuu ya masharti. Naomba hilo, laa kama haiwezekani basi ningewaomba benki yako ya *PBZ* iweze kuwasaidia hawa akina mama kwa kuwapunguzia masharti, ili na wao wawe na harakati za kufanya biashara.

Naomba sana mheshimiwa, hilo suala nimeona nilianze kwa kulifungulia dimba kwani ni suala ambalo kila siku nalisema sana.

Mhe. Spika, hili utaliona hapa lakini hata kwa Mungu utalikuta kwa sababu tumeambiwa katika hao ambao utakaowasaidia wamo wajane na wao watanufaika kwa fungu hilo ambalo utakaloweza kusema; wakati wa kuja kufanya majumuisho ikiwa leo au kesho utapotoa *plan* jinsi gani umejipanga na jinsi gani utaweza kuwasaidia. Na hiyo ni njia peke yake ya kukupeleka peponi. Hiyo wala usiwe na wasi wasi, tuwasaidie wajane. Hilo nimeona mimi niliseme ili tuweze kufika pahala pazuri sana.

Mhe. Spika, la pili, huko mitaani sasa hivi watu hawaelewi ongezeko la mambo ya dola, kwa sababu wanapiga kelele, mimi naomba hebu njoo uwape ufafanuzi kwani leo mihogo imepanda bei na kisingizio dola imepanda bei, ndizi imepanda bei kisingizio dola, majimbi yamepanda bei kisingizio dola. Hebu Mhe. Waziri nikuombe sana wewe ni mtaalamu njoo uwachanganulie jinsi gani je, hiyo dola inahusiana na muhogo, viazi vikuu, kwa sababu sasa hivi vitu hivyo vimepanda kweli kweli kupindukia, mpaka wanyonge wanashindwa kula futari. Hili nasema serikali namwambia kaka yangu hapo Mhe. Mohammed Aboud lisimamie, toa watu waende sokoni. Kwa kweli watu wanasikitika sana.

Mimi nakuamini Mhe. Waziri Mohammed Aboud ni mahiri usaidie hili kwa kupitia wizara yako kwa mujibu wa sheria, kwa sababu sasa hivi imekuwa kila anaekwenda sokoni analia machozi na huu ni mwezi mtukufu, ni mwezi wa kuchuma ya kheri, mwezi wa kuchuma thawabu, mwezi huu wa kujiandaa mtu kwenda Makkah. Naomba sana mimi na wewe tuko tayari kwenda Makkah, kwa hili naomba sana tulitafutie ufumbuzi ili tujitayarishe.

Mhe. Spika, mutajiandaa watu watatu; Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Makamu wa Pili hata na mimi ndugu yao tutakwenda Makkah hasa mwezi huu mtukufu. Kwa hiyo, mimi naomba sana hilo tuweze kuwasaidia wananchi kutokana na hali halisi.

Mhe. Spika, niingie ukurasa wa 14, hapa mimi nimefurahi sana kumbe yale tuliyokuwa tukiyasema na nyinyi kumbe mnayafanyia kazi. Nilisema sana hiki Kiwanda cha *ZAPOCO* nilikwambieni sana katika bajeti zilizopita, leo nimeona hapa *Alhamdulillah* wahakiki mali wamefanya kazi nzuri sana wamelirudisha hili suala kulileta serikalini.

Mheshimiwa mimi nimefurahi sana na niko pamoja na wewe kutokana na suala hili. Nimeridhika mpaka nafsi imefurahi kabisa kumbe zile kauli zetu zinafanyiwa kazi leo umetudhihirishia hapa umeshakichukua mwenyewe kiwanda hiki.

Mwenyezi Mungu akujalieni kila la kheri kwa suala kama hilo la kurudisha mali kwa wananchi, ili waweze kufanya masuala mengine.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alisifu sana masuala ya Kiwanda cha Sukari, mimi sina tatizo nacho, lakini uhalisia ndio mgumu; uhalisia wenyewe wananchi wale ambao tunaotegemea kufanya kazi katika kiwanda kile na ndio tuliotegemea watakaozalisha pato ili serikali iweze kupata. Mheshimiwa bado hawa wananchi hatujawatendea haki. Naamini sio Idara yako lakini kuna mambo ambayo yanahusiana na mambo ya *ZIPA*.

Kwa hiyo, naomba sana uweze kusaidia suala hili ili tuweze kufikia pahali pazuri ili mapato yale uliyosema, kwa sababu nilifanya majario lakini sasa hivi hakijazalisha tena kimo katika ukarabati wa hali ya juu. Nakubaliana nalo, lakini katika ukarabati pamoja na wafanyakazi wafanyiwe ukarabati wa mikataba.

Naomba sana hilo ikiwa kuna sehemu ambayo unahusika kuweza kuingia naomba uliingilie ili kulipatia ufumbuzi; wananchi wetu wanapata tabu sana, wanadhalilishwa sana. Inasikitisha mno kutokana na hali hii na hasa wenyewe ni wazalendo wa nchi hii na wavuja jasho, wakwezi na wakulima. Mimi ninaomba sana hilo, uweze kutusaidia.

Mhe. Spika, kuna moja humu sijaliona nataka niingie hapa hapa kuhusu habari ya kile Kiwanda cha Mpira. Mheshimiwa kiwanda hiki wamepewa watu wakiendeshe akiwemo na mwenyewe *investor* wa Kizungu; hili suala linasikitisha sana sijui sheria za *ZIPA* niseme zikoje na sasa hivi ni mwezi mtukufu wa Ramadhani wale watu tunawaweka wapi, wale watu fedha zao watapata wapi?

Mhe. Makamu wa Pili alikwenda lakini mpaka leo hatujapata *result* yoyote sijui kwa mujibu wa sheria ya *ZIPA* hapa anaweza kuhusika juu ya sheria gani yakuweza kuwasaidia wale watu kwa kuwatetea. Naomba sana mheshimiwa, wananchi wale wanaofanya kazi kule ni watu wanyonge, ni watu wadhalili, wanapata tabu. Sasa hivi watu wengine wana madeni chungu nzima, inasikitisha sana. Hili nakuomba sana kwa unyenyekevu wangu, naomba sana utusaidie kwa misingi ambayo unayoiona wewe tutaweza kupata ufumbuzi kwa sababu Ramadhani inaisha, sikukuu watu hawana.

Futari wameshaikosa, lakini sikukuu hiyo hapo mbele watashindwa kuweza kukamilisha. Inakuwa si vizuri kwa sababu mja yeyote ambaye anatakiwa afunge, basi na lazima siku hiyo avae vizuri, ale kizuri. Sasa kwa kweli hatutokuwa tunatenda haki, mimi naomba sana kwa misingi ambayo utakayoona wewe na jitihada zako na ukusanyaji wako wa kodi, basi naomba sana hili tujaribu kuwasadia hawa watu ili waondokane na hali hii.

Sasa hivi kiwanda kimefungwa lakini katika kufungwa kiwanda kile sijui nani kakabidhiwa; kama serikali ndio ishachukua wenyewe au bado kipo katika mikono yao.

Mhe. Spika, vile vile jambo ambalo la kusikitisha zaidi kwa hawa wenzetu tumesikia tatizo kodi serikalini nao hawajalipa. Je, mheshimiwa sheria yako inasemaje kwa kuwa hawa watu hawajalipa kodi ufumbuzi utakuja kuniambia wewe umefikia wapi na kuweza kuwazuia.

Mhe. Spika, sasa niingie ukurasa wa 22 Benki ya Watu wa Zanzibar. Mimi nawapa *hundred percent,* nimewafyagilia sana. Benki hii imeinuka kwa kiwango kikubwa sana tena kweli kweli, kumbe inaweza ushindani wakiwezeshwa. Benki inatambaa sasa na ninaamini yote hii ni kutokana na umahiri wako wewe amiri jeshi. Ingekuwa si wewe basi tungekuwa bado benki yetu inasua sua na ikiongozwa na Meneja mwenyewe pamoja na watendaji wake.

Mhe. Spika, umahiri mzuri na ninafurahi sana, *Alhamdulillah* huko Bara sasa hivi benki yetu ni *number one* watu wanaiamini. Watu wanakwenda kuweka mapesa chungu mzima. Mimi naomba watu waendelee kuwaamini hivyo hivyo na tuwape tena fursa waingie mpaka Mikoani huko. Tumesikia sasa hivi wanapenya penya Mikoani.

Kwa hiyo, naomba sana hapa na wao wabuni, na niwashukuru sana sasa hivi wamefanya *research* na nimewakubali. Nasema nimewakubali nilitoa wazo mimi la kusema sasa waingie katika vikundi vya *SACOS*, waingie kwenye vikundi hivi vidogo vidogo. Nawashukuru sana, sera imekamilika na sasa hivi tayari wamo katika *process* ya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa hili nalo ni moja katika kuwasaidia. Walikuja Jimbo la Kitope, wameangalia vikundi vya visanduku, wameshaongea nao. Kwa hiyo, naomba mheshimiwa ili na sisi tusaidie, mimi ni mmoja katika mfyagiliaji waje kabla ya kura. Waje kule, waendelee, wawape zile fedha jinsi ambavyo walivyoona, kwa sababu visanduku ni moja katika *training* nzuri ya kukopeshana, ni kama *small bank village.*

Kwa hiyo, mimi nimefurahi sana ni watu ambao wako vizuri wanakopesha vizuri. Wanarudisha vizuri. Hilo ni zoezi kubwa na waliliona hilo. Nimshukuru mama muhisika Meneja, ameli-*handle* vizuri sana. Kweli wanawake wanaweza wakipewa msukumo, nakubaliana nao. Namkubali mama yule ni mjasiri, ameandaa mpango mzuri na madhubuti na hasa nimpongeze kanisikia sauti yangu kwa sababu aliona jinsi gani benki itaingiliana na wananchi wadogo wadogo. Nalo hilo kwa kweli

limenipa faraja kubwa sana, *Alhamdulillah*. Ndio maana *PBZ* ikitusikiliza masharifu kama sisi ndio inainuka. Si mchezo mheshimiwa sasa hivi ina-*improve* kila siku kukicha. *Wallahi* tofauti na zamani. Zamani tukubaliane hilo lakini leo tuna Benki ya Kiislamu na wakati zamani kulikuwa hakuna. Imetokana hapa hapa na suala hili wanakwenda vizuri sana.

Mhe. Spika, nizungumze moja hapa katika Benki ya Kiislamu; watu wanasema wanachelewa kupewa fedha walizoomba. Naomba sana meneja muhusika awe *faster* kwa wateja wake wanalalamika na haki yao kulalamika.

Mhe. Spika, niingie katika ukurasa wa 25 *ZSSF*; hapa naomba nitoe ushauri kwa kuwa hizi fedha zinazokusanywa wenyewe ni wale ambao kwa mujibu wa sheria wamekubalika wazipeleke pale. Hebu tuwafanyie na wao kama mfumo wa benki. Tuwakopeshe wenyewe wajikwamue kimaisha, iwe inazunguka pale pale. Iwanufaishe, tusingojee miaka 60. Miaka 60 sio ya leo na hii sheria tumeshachelewa, lakini nilisema miaka ya nyuma kwamba tuilete tuwasaidie watu kwa sababu watu wanafanya kazi mahotelini wanafukuzwa ovyo ovyo, hata watu wa Kiwanda cha Sukari na wao sijui kama wamepeleka fedha kule, isitoshe na watu wa Kiwanda cha Mpira pia.

Mhe. Spika, kama hao watu wa mpira hawajawapelekea wananchi pesa zao za *ZSSF* watiwe pingu, nilisema nije na pingu yangu lakini nimeisahau, tusichezewe katika masuala haya. Huu Mfuko sio mchezo. Ni Mfuko ambao unakuja kuwasaidia wanyonge baada ya kustaafu. Leo kwa nini mtu anayachezea chezea mafao kama hayo.

Mhe. Waziri naomba sana leo tutoke mimi na wewe tukawatie watu pingu, hapa nakusubiri nje kwa sababu imekuwa wanachezea watu kipuuzi. Mhe. Waziri nataka aje anambie ni kesi ngapi kafanikiwa na kesi ngapi kawatia watu ndani. Kwa kweli inasikitisha sana kwa sababu watu wanafanya kazi kwa kutegemea kuwa ana Mfuko wake utamuhifadhi huko mbele ya safari, japo miaka mingi kwa sababu hiyo ni miaka mingi.

Kwa hiyo naomba sana na ninamuomba mkurugenzi muhusika asiikubali hii sheria ikachezewa, awe mkali kabisa. Vijana wanajitahidi siwatoi shukurani, mimi huwa nakwenda pale nakutana nao lakini sio niondoke tena na wao wakalala usingizi. Kwa hivyo, wananchi wanaofanya kazi kiwanda cha mpira wanadai haki zao hawajui kama zinakwenda *ZSSF*.

Namuomba Mhe. Waziri aje anambie kama zinakwenda na kama haziendi sababu gani zinazosababisha kuwa zisiende, wakati wao wanakatwa kwa mujibu wa sheria.

Vile vile, hivi sasa maisha yanapanda na katika kupanda kwake ningeomba tuwe *faster* katika kutafuta. Mhe. Hamza Hassan Juma ana kampuni ambayo inajenga nyumba nafuu sana, hebu tumuite tukae naye tumsaidie. Mimi siku moja nilimwambia mkurugenzi kwamba hebu tusikilizeni na sisi tukusaidieni maarifa. Sisi wengine tuna akili ya kuzaliwa. Tuna akili ya kuweza kuendesha jambo likaleta manufaa kwa umma.

Sasa mimi ningeomba mtusikilize tukitoa ushauri jamani, kwa sababu hili suala la mfumo wa kibenki nimesema zamani sana na mwenyewe mkurugenzi kama yupo juu hapo ni shahidi; nilizungumzia suala hili kwamba tuwe na mfumo ambao tunawakopesha watu kwa kuendelea kuzalisha.

Nakubaliana na miradi iliyokwishaanzwa midogo midogo; mradi wa mnara, mradi wa pembea zile lakini hii *income* yake ni ndogo. Hebu tutafute *big project* ambayo itaweza kuingiza *income* kubwa ikawanufaisha wananchi.

Mhe. Waziri namuomba sana watuite na sisi wapate hazina za kichwa, waje tuwasaidie. Tuna mambo mengi sana ya kuweza kuinua hii *ZSSF* ikawa nzuri sana. Tunatembea tunaangalia, tunapishana na mkurugenzi wangu, mimi ninatua Marekani yeye anaingia hao tunaondoka. Ndio tunatafuta maisha namna hiyo. Kwa hivyo, mimi nimefurahi na Mfuko huu aendelee kujitahidi sana.

Mhe. Spika, niingine katika *ZRB*. Nashukuru sana kwa mapato waliyokusanya vizuri sana, kama uwezekano upo basi hawa wangetunzwa na hasa kwa vile huu ni mwezi wa Ramadhani. Kwa sababu wametuonesha jinsi gani ya ukusanyaji wa mapato wamebadilika. Tulikuwa tunakusanya shilingi 13 bilioni, sasa hivi tunakwenda 14. Kwa nini tusiwatunze? Mimi naomba tuwatunze ili na wao roho zao zikonge, zijisikie raha na kuwatunza watu kama hawa wapewe mikopo ya magari makubwa wajisikie, si vibaya haki yao.

Mhe. Spika, nije kwenye Mfuko wa Barabara ambao watu wengi hawajui jinsi gani vya kuweza kuupata. Ningeomba wananchi wa majimbo wataweza kujua wafanye njia gani ili waweze kuutumia Mfuko wao huu kwa kuweza kupata zile *feeder roads* na kuweza kusaidia vifusi kwenye madaraja. Hili ningeomba nisaidie sana kwa kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, nimalizie vitega uchumi. Hapa kidogo kazi ipo, uchumi wote uko hapa. Lakini hapa kwanza nataka nishukuru sana; unajua miaka ya nyuma wakati ule kuna kaka yangu mmoja anaitwa Azizi tulikuja tukawaambia pale kulikuwa na tatizo la wananchi. Mtu alijenga ukuta, kwa kutumia sheria mara moja watu walikwenda kuvunja, lakini naomba kwa mujibu wa sheria zetu za nchi nije kuelezwa hapa, yanapotokea matatizo kwa watu wanaofanya kazi mahotelini

wanapaswa wakae upande gani na wasaidiwe nini katika kutoa ushauri ili kuweza kusuluhisha tatizo. Kuna matatizo mengi yanatokea ya wawekezaji; mwekezaji mwanzo anakuwa ni rahimu anafunga mikataba na wananchi vizuri, lakini baadae anakuwa anawageukia. Sasa je, mkataba unaofungwa ndugu zangu wa *ZIPA* hawahusishwi? Kama ni hivyo basi naomba sana wawe wanatoa elimu kuwaelimisha wananchi wasifunge mikataba na wawekezaji kabla *ZIPA* hajaingilia kati na yeye akawemo katika suala hili.

Mhe. Spika, suala hili linaendelea kuongeza matatizo. Nimshukuru mkurugenzi anafanya kazi vizuri sana, lakini kama hakupelekewa ripoti maana yake inakuwa hajui nini kinachotokezea. Nataka nimuombe sana mkurugenzi wangu aendelee kuwaelimisha, wananchi wetu wanadhalilishwa kabisa kwenye mahoteli humo. Hawa wananchi ni masikini kwa sababu wanategemea kikiweko kile kitega uchumi kiwasaidie kukuza uchumi, lakini kinageuka kinakuwa kitu cha kudhalilisha, sasa sio vizuri.

Ninaomba sana tuwe karibu sana na wananchi hasa kupitia *ZIPA*, wanakuwa karibu nao, wanakuwa na *team work* nao, lakini naomba sana kuhusu suala hili.

Mwisho kuhusu habari ya biashara. Biashara tulisema sana kuhusu *TRA*, hebu Mhe. Waziri ajaribu tena kuzungumza na wenzetu kodi ipungue, basi hata mafriji wanayopelekwa wananchi inakuwa bei kubwa, honda ile pia inakuwa kodi kubwa. Hii *TRA* ni moja lakini kutokana na hali yetu sisi, uchumi wetu ni mdogo hawa ndugu zetu wanaobahatika kwenda kupeleka kule wanakwenda kutafuta maisha, ili kuondokana na umasikini na kujiokoa na kufanya yale yasiostahiki.

Mhe. Spika, nakubaliana na muda wako, naomba kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Pia nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake, niwapongeze sana kwa mfumo wa mara hii wa bajeti wa *PBB*. Kwa hayo machache nawagaiya asilimia mia moja, ahsante sana.

**Mhe. Farida Amour Mohammed:** Mhe. Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kufika hapa nikiwa na afya njema.

Pia naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake jinsi walivyoiandaa hotuba yao hii na pongezi zaidi zije kwa Mhe. Waziri jinsi alivyoiwasilisha kwa umakini sana na kila mmoja wetu kaifahamu.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa mdogo mno. Nitaanza katika ukurasa wa 18; Ofisi Kuu Pemba. Pamoja na majukumu mengi ya Ofisi Kuu Pemba, lakini

pia imo katika kuratibu na kusimamia malipo ya kiinua mgongo na pencheni kwa wastaafu.

Mhe. Spika, kiukweli katika uchukuaji wa kiinua mgongo wenzetu wastaafu hawa wanacheleweshwa sana kupata kiinua mgongo chao. Mtu anastaafu inachukua karibu mwaka hajapata kiinua mgongo chake. Nasema hivi kwa sababu wafanyakazi wetu wote tunawajua. Kwa mujibu wa mishahara yao wanayopokea hawana uwezo wa kuweka akiba ya mishahara yao wakasema mtu nikistaafu nipate kitu cha kuanzia. Sasa naiomba sana wizara iliangalie kwa umakini sana hili kwa sababu mtu yeyote anapomaliza kufanya kazi anatakiwa apate malipo yake mapema, ili mwenyewe ajiandae na chochote anachotarajia kukifanya.

Mhe. Spika, nije katika suala langu jengine kwenye Mamlaka ya Vitega Uchumi. Katika mamlaka hii nataka nije kwenye ujenzi wa mahoteli. Ninakumbuka katika kikao kimoja hapa nilichangia suala hili la ujenzi wa mahoteli katika kisiwa cha Pemba kwenye visiwa viwili vya Fundo na Uvinje.

Mhe. Spika, bado nina malalamiko au nina kilio katika ujenzi wa mahoteli haya bado mpaka leo hii wale wananchi wanaoishi katika maeneo yale wanapotoka kwenda kufanya harakati zao za kimaisha, mfano kwenda shamba kulima, kutafuta kuni, bado wale askari wa vikosi waliowekwa pale kwa ajili ya ulinzi wa kujenga hoteli ile wanawaendesha kichura, wanawahangaisha, wanawadhalilisha. Hili jambo linatushitua sana kwa sababu uwekezaji tunategemea mwekezaji apate, lakini pia na wale wananchi waliopo katika maeneo yale nao wafaidike. Lakini sasa katika hatua ya awali ya ujenzi wa mahoteli haya tunatumia mtutu wa bunduki, sasa sijui kulikoni au kumezidi nini mpaka likaja hili.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha ni msikivu sana labda kama binadamu alisahau, lakini nafikiri katika kikao cha hapa ndani ya ukumbi huu lilizungumzwa suala hili na yeye akaniahidi mbele ya ukumbi huu wa Baraza kwamba tutakwenda mimi pamoja na yeye na watu wengine wanaohusika, ili tukazungumze na wale watu wa eneo la Uvinje na Fundo kuwapa elimu. Kwa sababu mtu yeyote akielimishwa anaelewa, wale watu kitu kikubwa kwao ni elimu.

Mhe. Spika, sasa katika hatua ya awali watu wanajenga hoteli ile kwa mtutu wa bunduki. Je, watu hawa nini hatma yao ya baadae baada ya kumalizika ujenzi ule?

Kwa sababu ninavyofahamu watu wa maeneo yale ni watu wa visiwa; ni wavuvi, wengine wakulima, sasa watahitaji kupeleka bidhaa zao pale. Lakini katika hali kama hii watakuwa hawana imani ya kupeleka bidhaa zao katika hoteli zile wakati kwa hatua ya mwanzo tu wanaanza kudhalilika. Ninamuomba sana Mhe. Waziri katika hili aliangalie kwa umakini mkubwa. Mahoteli yanapojengwa panahitajika

mashirikiano na wale watu waliopo. Kwa sababu watu wale wanapokuwa na mashirikiano ya dhati na wawekezaji ndio neema itakapoingia, serikali ikapata mapato yake na wale wananchi wakafaidika kwa kupata ajira.

Pia namuomba Mhe. Waziri vikosi hivi vilivyowekwa pale kwa ajili ya kuwadhalilisha watu haitokuwa suluhisho la kupata maendeleo. Namuomba sana Mhe. Waziri, vile vikosi pale havina haja; cha msingi ni kwenda mamlaka husika wakenda kuzungumza na watu ili kupata mashirikiano mazuri, sio kwa sababu ya vikosi.

Mhe. Spika, naomba niendelee kidogo katika misaada ya kibajeti. Misaada hii mwaka huu hatukupata msaada wa kibajeti, lakini miongoni mwa sababu tulizopewa kwa mimi binafsi naziona sio za msingi sana. Sababu tulizopewa ni kwamba tumeingizwa katika sakata la *Escrow*, jambo ambalo sisi Wazanzibari halituhusu, sakata la *Escrow* ni la watu wa Tanzania Bara.

Sasa kinachonishangaza kwa nini serikali yetu inashindwa kujenga hoja nzuri kwa wafadhili na kuonekana kwamba sisi sakata lile halituhusu ili tukaweza kupata misaada ile kwa ajili ya kusaidia nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Spika, miaka ya 1990 nakumbuka tulinyimwa misaada hapa kuhusiana na Haki za Binadamu Zanzibar, lakini wenzetu Tanzania Bara walijenga hoja nzuri tu wao wakapewa, sisi tukanyimwa. Sasa na sisi naomba sana Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla wajenge hoja nzuri ya kuonesha kwamba sisi sakata lile la wizi wa *Escrow* halituhusu ili tuendelee kupata misaada katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kidogo naomba niendelee katika *PBZ. PBZ* Pemba mwaka jana kama sikosei lilizungumzwa na Mhe. Salma Mohammed Ali kuhusu *ATM* inayotumia *Visa Card*. Watalii wanaingia katika maeneo tofauti na Pemba sasa hivi watalii wanakwenda kwa wingi, lakini kwa bahati mbaya wanashindwa kutumia mpaka waje Unguja, Pemba hakuna *ATM* inayotumia *Visa Card*.

Kwa hiyo, naiomba wizara iliangalie hili kwa umakini sana ili wale watalii wetu wasihangaike na pia hili linazorotesha mapato katika Sekta ya Utalii. Kwa sababu watalii wakipata kutumia kule na sekta yetu ya utalii nayo pia itapata kuingiza na ikiingiza serikali nayo inapata mafanikio.

Mhe. Spika, pia nasema nizungumze suala ambalo ni muhimu kuhusu *ATM* hapa kwenye Baraza la Wawakilishi. Mheshimiwa mfano mzuri huigwa, tulipokwenda Bungeni pale kwenye Bunge la Katiba tuliona pale palikuwa na *ATM*. Sasa naiomba wizara hii ifanye utaratibu na hapa kwenye Baraza la Wawakilishi waweke *ATM* kwa sababu sio lazima sana kuwa mtu atoke hapa aende nje

akapange foleni kwa kutoa pesa. Naomba sana liangaliwe hili na ikiwezekana lifanyiwe utaratibu huo ili watu watoe pesa katika maeneo haya bila ya kwenda kwenye maeneo mengine.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mchango wangu hautokuwa mkubwa lakini naomba nimalizie kwa suala moja la kupanda bei kwa bidhaa. Suala hili wengine linatuhuzunisha sana, kwa sababu kweli dola imepanda lakini kuna baadhi ya wafanyabiashara wale wakubwa wakubwa bidhaa wanazo ndani ya *store* zao, lakini baada ya kupanda dola tu zile zile walizokuwa wakiuza kwa shilingi mia nne sasa wanauza shilingi 1,400.

Mhe. Spika, huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani; naiomba serikali kwa nguvu kubwa ifanye utafiti na italiona hilo. Wafanyabiashara wale wakubwa wanawaumiza hawa wadogo wadogo wanaokwenda wakichukua biashara kwao. Kwa sababu wao biashara na bidhaa wanazo ndani mwao *store* kwa miaka mingi tu, lakini sasa wale wadogo wanaokwenda kuchukua kwao wanawauzia kwa bei kubwa na mwananchi anakufa kabisa. Kwa hiyo, ninaiomba wizara na serikali kwa jumla iliangalie hili.

Mhe. Spika, nitaunga mkono hoja hii pindi Mhe. Waziri wa Fedha atakaponijibu hasa suala la ujenzi wa mahoteli Pemba na jinsi ya kudhalilishwa wale watu wetu wanapokwenda kwenye harakati zao za kimaisha na kuondoshewa kwa kikosi kile. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Bismilahi Rahmani Rahiim. Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura na mimi nikaweza kutoa mchango wangu wa mawazo katika Wizara hii ya Fedha.

Mhe. Spika, kama walivyotangulia wenzangu na mimi nampongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wake anaotupa sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Waziri wa Fedha yuko muwazi sana na sisi mara nyingi hapa kwa muda wa miaka mitano tulikuwa tukimshauri sana katika kuhakikisha kwamba mianya au uvujaji wa mapato ya serikali anaiimarisha kwa kuiziba.

Kwa kweli tunamshukuru sana kilio chetu kile amekisikia na sasa hivi *Alhamdulillah* kama alivyosema mwanasheria wangu pale Mhe. Makame Mshimba kwamba sasa hivi angalau mapato ya serikali yanaingia vizuri sana. Tulikuwa tukikusanya shilingi 13 bilioni sasa hivi tuko karibu shilingi 35 bilioni. Kwa kweli ni hatua kubwa sana ambayo tumepiga. Kwa hiyo, nampongeza sana Mhe. Waziri kwa usikivu wake lakini kwa ushirikiano wake, lakini vile vile kwa utendaji kwa usikivu wa watendaji wake kwa vile vilio ambavyo tulivyokuwa tunaviwasilisha hapa Barazani.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa ninataka niende moja kwa moja katika michango. Zanzibar bado tunayo nafasi ya kutangaza visiwa vyetu au maeneo yetu kiutalii ili kuongeza mapato ya Serikali. Naungana mkono na rafiki yangu pale ingawa ameondoka kwamba Kisiwa cha Funga Mbaraka, kweli kisiwa kile kuna ndege wengi sana adimu na ndege wale wanakuwa wanahamahama halafu wanarudi na ndege wale huwakuti katika maeneo mengine. Kwa hivyo ina maana Kisiwa kile cha Fungu Mbaraka kina harufu na mvuto fulani ambao unaowafanya ndege adimu, wanakwenda katika kisiwa kile.

Mhe. Spika, kama utateremka katika kisiwa kile basi sijui nikitumia lugha hii, ile samadi ya ndege basi unaweza ukatia mguu wako ukafika kwenye goti. Kwa sababu ni ndege wengi wanaokwenda pale, wanakwenda haja sana na kwa kweli kile kisiwa ndiyo maana kikawa kina hiyo raslimali ya mafuta na gesi.

Kwa hivyo bado Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Mhe.Waziri wake hapa simuoni, bado anayo nafasi ya kukitangaza kile, kwa sababu kisiwa kile ni mali ya Zanzibar, kama tunavyosema na kama taarifa mbali mbali na *documents* zinavyoonesha. Isipokuwa tu lile suala moja ambalo juzi nilitofuatiana kidogo na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali kuhusu suala la uchimbaji wa raslimali ya mafuta na gesi. Lile kama tulivyosema lazima kwanza tufanye marekebisho ya Katiba ili sasa tuweze kutumia kikamilifu kwa ile samadi ya wale ndege, lakini vile vile na ile raslimali ambayo iko chini ya ardhi.(*Makofi*)

Mhe. Spika, nikiendelea katika suala zima la mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Naomba sana wafanyabiashara watuhurumie, wawaonee huruma wananchi wetu wanyonge. Enzi za Manabii kuna hadithi moja inasema, "Ubora wa tajiri kuingia peponi, basi bora ngamia inakuwa ni wepesi kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia peponi", kwa sababu gani, mifano ndiyo kama hii.

Mhe. Spika, tunaishukuru sana Serikali kuwa imetoa msamaha kwa bidhaa mbali mbali za vyakula. Leo bidhaa zile Serikali ilipotoa msamaha tayari zimo madukani zilikuwa zimeshaingizwa nchini, zimeshanunuliwa na kuingizwa nchini. Tulitegemea bidhaa zile zingelishuka bei au zingeliendelea kuwa na bei yake ile ile lakini leo sukari tayari imepanda bei. Sasa je, halafu wafanyabiashara hawa ndiyo wanaotoa zakka. Sasa inakuwa zakka au nini.

Mhe. Spika, kwa kweli ni kitu ambacho hakipendezi. Zakka si lazima utoe umpe mtu, ile kuwa muaminifu katika ile kodi inayosimamiwa na Serikali kumuuzia mwananchi kwa bei halali, ile ilikuwa inatosha kuwa ni zakka. Leo ninawaomba sana na Serikali hili munapotoa misamaha muangalie, muwape *conditions* bidhaa ambazo zipo ndani ya soko lakini na bidhaa ambazo zinazoingia ndani ya soko.

Leo kila mtu anasingizia *dollar*, kweli *dollar* imepanda lakini hiyo *dollar* ilipopanda wewe bidhaa tayari ilikuwepo ghalani, tena hiyo bei imeongeza wakati gani. Lazima wafanyabiashara wetu wawe na huruma na wananchi wetu.

Mhe. Spika, ninakuja maeneo ya uwekezaji. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha akija kutoa ufafanuzi umpe muda wa kutosha atufafanulie mipango na mikakati ya Serikali katika kuyaendeleza maeneo huru ya kiuchumi.

Mhe. Spika, maeneo haya tumeyazungumza sana. Maeneo huru yamekaa kwa muda mrefu na kwanza kabla anapokuja kutoa ufafanuzi atueleze je, tulitoa agizo hapa kwa Serikali, maeneo kwanza yapatiwe hati miliki, yawekewe utaratibu wa matumizi.

Je, hili suala kwanza limeshafanyika na kama limeshafanyika au kama halijafanyika kuna sababu gani. Lakini je, atupe mipango ya Serikali na tena mipango madhubuti ya Serikali ya kuendeleza haya maeneo ya vitega uchumi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tuna eneo la Fumba na Micheweni. Mhe. Subeit Khamis Faki siku zote hapa anapiga kelele, hali ya wananchi wa Micheweni na sisi tunapokwenda tunaona hali kidogo siyo nzuri. Maeneo yale yakishughulikiwa, yakianzishwa viwanda vidogo vidogo na viwanda vya kati, watu watapata ajira. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri akija hapa aje atueleze uendelezaji wa maeneo huru ya kiuchumi. Vile vile Mhe. Spika, nilikuwa ninataka Mhe. Waziri aje anisaidie ufafanuzi mwengine. Ufafanuzi ninaotaka eneo la Maruhubi. Sasa hivi Serikali imeshatangaza kwa muda mrefu na sasa hivi kuna mipango imo mbioni na mbio zenyewe zinakaribia kufikia, kuhusu suala la ujenzi wa bandari ya Mpigaduri.

Mhe. Spika, Serikali ilipokuwa inafanya mpango huu bado tulikuwa hatujaweka ndani ya akili zetu suala la uzalishaji wa mafuta na gesi. Leo bandari ya Mpigaduri tunategemea ndiyo itakuwa ni *hub* kwa Zanzibar na tunaweza ikawa pengine kwa Afrika Mashariki, hasa kutokana na kina cha maji kilichokuwepo katika eneo la Mpigaduri. (*Makofi*)

Bila matarajio eneo lile tumesikia tayari linaanza kuwekezwa na baadhi ya wawekezaji wengine. Sasa je, leo eneo lile, mimi nilitegemea na ndiyo maana juzi nilisema tuna *master plan* ya bandari zetu. Kwa sababu kama hatuna *master plan* tunaweza tukaja tukala hasara kubwa kununua eneo ambalo lilikuwa la Serikali ili sasa kuweza kuweka *investements*.

Mhe. Spika, tukiwa na uchumi wa gesi na mafuta, bandari zetu zitakuwa hazitutoshi, kwa sababu meli zitakuja kwa wingi na viwanda vitakuwepo vingi, maeneo ya bandari yatakuwa hayatoshi. Sasa hili nilikuwa naomba aje atusaidie. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Spika, eneo ambalo ninahisi Serikali bado hatujalifanyia kazi ipasavyo na hili naomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na *ZIPA*. Je, hivi visiwa vyetu uwekezaji wake kweli unaendana na hadhi ya Zanzibar na hadhi ya visiwa vya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi sikubaliani na huu uwekezaji katika visiwa. Mimi ninaomba Serikali i-*review* ile mikataba, iifute halafu tutafute wawekezaji au hata kama hao wapo wanaweza tupate uwekezaji ambao wenye thamani kubwa.

Mhe. Spika, visiwa duniani vina thamani kubwa ukiacha kisiwa cha Zanzibar kinajiuza lakini hivi visiwa vidogo vidogo ni visiwa ambavyo vinatakiwa viongeze mapato makubwa. Leo katika bajeti yetu hii Mheshimiwa umetuomba bilioni 30 tukuruhusu ukope, visiwa vile kama kungekuwa kuna *investment* nzuri tusingemkopa mtu wala usingehangaika kwenda *BOT*.

Mhe. Spika, naomba uje unipe ufafanuzi wa kutosha. Je, *investment* ya visiwa ina tija kwa Zanzibar. Mimi ninavyohisi haina tija na mikataba hii ifutwe, aidha kama iitishwe *tender* kwa utaratibu ambao tutaweka, tunataka uwekezaji wa aina fulani, *capital* ya aina fulani iwekezwe katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu Kiwanda cha Maziwa. Tunashukuru sana ndugu yetu mwekezaji Said Salim Bakheressa kwa kuanzisha Kiwanda cha Maziwa na tunashukuru kwamba vijana wetu wengi pale sasa hivi wameweza kupata ajira. Lakini kuna jambo ambalo kiwanda kabla ya kuwepo, tulipewa maneno mazuri tu na Serikali kwamba angeweza kununua maziwa kutoka kwa wananchi, wafugaji walipata moyo mkubwa sana kwa kutegemea wangelifuga ng'ombe na soko tayari lipo la maziwa. Sina uhakika lakini kwa taarifa niliyoipata maziwa ya kuendesha kiwanda kile yanaagizwa kutoka nje ya nchi ni maziwa ya unga. Sasa je, hawa wafugaji wetu, hawa wakulima wanaofuga ng'ombe wanafaidika vipi.

Vile vile tunaambiwa hata hayo maziwa yanayoingizwa *exemption*. Sasa kama maziwa yale yanapatiwa *exemption*. Je, kuna tija gani ambayo inayopatikana kupitia ile *exemption* ya hayo maziwa. Kwa sababu sisi tulitegemea wananchi wangelifuga ng'ombe kwa wingi wakazalisha maziwa kwa wingi ili kuweza kusaidia kuwapunguzia umaskini wa kipato katika maeneo yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninakuja eneo jengine na hili naomba sana *ZIPA* mutusaidie. Kuna mwekezaji anataka kuweka Kiwanda cha Maji pamoja na Kiwanda cha Vibiriti. Kuna viwanda kama vitatu kwenye eneo baina ya Kiboje na Dunga, pale kati kati. Lile eneo ambalo ilipokuwa ikijengwa barabara ile palichimbwa kifusi likatoboka shimo na shimo lile, limetumbuka maji. Eneo lile tokea kutumbuka maji limeachwa lipo *idle*, lakini leo ametokea mwekezaji anataka ku-*invest* katika eneo lile, ametokezea mtu eti anasema lile shimo lake.

Mhe. Spika, yaani sisi tumekaa kama......, sijui akili zetu zina wadudu. Wewe shimo limekaa halimsaidii mtu yeyote, leo katokezea mwekezaji anataka kuwekeza, unasema shimo lako. Wewe una shimo umelipa wapi. Mhe. Spika, mimi naomba sana *ZIPA* watusaidie ajira. Mimi nimefanya mazungumzo na huyo mwekezaji anasema pale Kiwanda cha Vibiriti anategemea kuwaajiri vijana mia sita na katika mia sita hao, mia moja ataajiri watu wenye virusi vya Ukimwi ambapo tayari anacho kiwanda kama hicho. Tumeshakitembelea Dar es Salaam, tumewakuta vijana pale wengi sana na miongoni mwao wamo vijana wenye virusi vya Ukimwi. Lakini kiwanda hicho anakusudia atachukua vijana kwenye *sober houses* vijana wengine mia moja. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, leo mwekezaji kama huyu mtu anatokea anasema shimo langu, tena hilo shimo hata hati miliki ya eneo hana. Mimi naomba Mhe. Waziri tuwasaidie sana *ZIPA* wasimame ili hiki kiwanda kiweze kuwekezwa pale. Pale zitatoka ajira karibu elfu moja na mia mbili, hizo mia sita za Kiwanda cha Kibiriti tu.

Mhe. Spika, hili nilikuwa naomba Mhe. Waziri alifanyie kazi. Ndiyo tunaongeza mapato, tunaongeza na ajira na kupunguza umaskini. Leo mtu anasema shimo lake halimpatii shilingi, yeye amekaa kutia hasara tu na mbu pale. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Kiwanda cha Sukari. Ninamshukuru alau leo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (*professor*) Kiwanda cha Sukari amekisifu, siku zote alikuwa analalamika yeye na wananchi wake na Kiwanda cha Sukari, leo alau amekisifu. Inaonesha kuna hatua Serikali imezishughulikia. Sasa lakini naomba ufafanuzi.

Kuna taarifa kwamba kuna ukarabati mkubwa wa kile kiwanda. Je, Serikali haya yanayofanyika; kuna mashine zinang'olewa, kuna miundombinu baadhi yao inang'olewa. Hili Mhe. Waziri analijua kwa sababu isijekuwa kama Hoteli ya Bwawani; tumempa mwekezaji, matokezeo yake akang'oa ng'oa ile mitambo mizuri akaweka yake, matokeo yake ametuachia sasa hivi zimekuwa ofisi. Kwa hivyo na kule Mahonda nilikuwa naomba Mhe. Waziri hebu hili alifanyie kazi atakapokuja kutujibu atupe taarifa za kutosha.

Jengine Mhe. Spika, bado kuna malalamiko ya wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; bado wanadai haki zao. Sasa hili hebu Mhe. Waziri naomba alifanyie kazi akija kutoa ufafanuzi atusaidie maelezo.

Mhe. Spika, nakuja *ZSSF*; mimi ninashukuru sana Serikali tulimleta hapa mwekezaji kutoka Marekani tukampeleka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tukazungumza naye, na kwa bahati akatualika Marekani na mimi ninashukuru katika ziara ile nilishirikishwa. Mwekezaji yule alikuwa yupo tayari kushirikiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii katika kufanya *joint venture*, katika kujengwa nyumba za bei nafuu. Sasa hili suala mpaka leo lipo kimya. Hebu naomba akija hapa Mhe. Waziri aje atueleze ile mipango imeishia wapi, Mr. Shumaker.

Mhe. Spika, yule ni Balozi wa Heshima wa Tanzania kule nchini Marekani. Kijana yule ni investor mkubwa na tayari ameshafunga mkataba Dar es Salaama kwa kujenga *train* za mjini; zile *train* za kasi. Wenzetu wamekwenda mwisho wamesaini mkataba mwanzo, sisi tumekwenda mwanzo mpaka leo sijui mkataba umeishia wapi. Nilikuwa naomba sana kama alivyosema mwenzangu hapa Mhe. Makame Mshimba wafanyakazi wetu hawa wakijengewa nyumba nafuu itapunguza hata udokozi dokozi.

Mhe. Spika, watu wengi wanaodokoa dokoa wanakwenda kujenga nyumba, kwa sababu hawana pa kukaa. Sasa mtu akishapata pa kukaa *Alhamdulillahi* na mshahara anapata udokozi utapungua na nidhamu ndani ya Serikali itakuwepo vile vile.

Kwa hivyo naomba sana ndugu zetu wa *ZSSF* hebu mutwambie ile hatua mumefikia vipi. Lakini vile vile ninawapongeza kwa kufanya kazi nzuri pale Uwanja wa Kariakoo. Unajua kila na mtu uwono wake, wengine wanalaumu wanasema pesa zimepotea. Kariakoo pesa hazijapotea. Kariakoo panatakiwa usimamizi mzuri wa yale mapato ama wasimamie wao wenyewe au watafute kampuni pale wafunge nao mikataba uweze kuendelea. (*Makofi*)

Mhe. Spika, maeneo kama yale huwezi ukawa na nchi watoto hawana pa kucheza. Leo kila pahala watoto vumbi, leo alau nchi yetu inaanza kung'ara. Mhe. Spika, wewe ni shahidi. Tumeshakwenda China mara nyingi. Kwa kweli China kila eneo unalokwenda unakuta sehemu watoto wanacheza na kuburudika na watoto wakipata pahala pazuri pa kucheza, ndiyo wanakuwa kiakili, isiwe kila wakati wanakaa tu wanapishana na wala unga, mara sijui wanapishana na nani wauza mihogo, wauza nini, hawana maeneo watoto pa kucheza. Kwa hivyo eneo lile Mhe. Spika, ninawashukuru sana lakini ninaomba unajua sisi tatizo letu katika kuendesha, katika ku-*invest* tunaweza tuka-*invest* lakini katika uendeshaji naomba

wafanye mahesabu yao, kama wanaweza wao, kama hawawezi basi watafute mwekezaji. (*Makofi*)

Mhe. Spika, huna haja ya kuniambia dakika tano nimeshajua zimebakia dakika tano, ninajitahidi *points* zangu nizimalize.

Jengine ni kuhusu *PBZ*. Ninawapongeza sana kwa kazi nzuri...

**Mhe. Spika:** Unazo dakika tano.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Ahsante sana. Mhe. Spika, mimi nimeshakujua kuna style ukikaa tu ninajua unataka kuniambia dakika tano. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe.Spika, kuhusu Benki ya Watu wa Zanzibar. Sasa hivi munafanya vizuri lakini bado munakaa katika nyumba za kupanga, kwa nini? Mhe. Spika, tunataka Benki ya Watu wa Zanzibar, kwanza sisi ndiyo tuliokuokoweni hapa, tayari ilikuwa inakwenda kubinafsishwa. Sasa hebu tafuteni jengo lenu. Mimi ninaona haya sana Mameneja wanapendeza, makoti mazuri, suti nzuri, lakini munakaa nyumba za kukodi. Hatutaki tena mukae katika majengo ya watu, tunataka mujenge *headquater* yenu ili Benki ya Watu wa Zanzibar tuone ile hadhi yenu na jengo lenu vile vile. Hayo maeneo muliokodi wapate kupangishwa watu wengine, lakini kwa kweli kazi munafanya vizuri.

Tunashukuru sana *Islamic Bank* sasa hivi inafanya kazi vizuri na basi isiwe kama mgema, tunakusifuni muendelee kufanya kazi vizuri vile vile.

Mhe. Spika, vile vile Shirika la Bima; tunaomba sana Shirika la Bima kwa nini hawawekezi katika *Health Insurance*. Sasa hivi maradhi mengi, tunaumwa sana, mara sukari, mara *pressure*, yaani maradhi tele mpaka Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali yeye pesa zake za jimbo kaamua kuzipeleka Uzini kwenda kununulia madawa. Kwa hivyo inaonesha sasa hivi Uzini madawa itakuwa siyo *issue*. Lakini naomba kama yatabakia yaletwe Hospitali ya Kwamtipura.

Mhe. Spika, naomba sana sisi tupo tayari kuanza kushirikiana nao Shirika la Bima la Zanzibar katika kuanzisha Bima ya afya. Hivi sasa tayari tuna hospitali nzuri; tuna hospitali za kisasa. Tuna hospitali ambazo zinaweza zikamtibu mgeni yeyote; mtalii wa aina yeyote kutoka nje. Hata viongozi wa nchi wanaweza wakatibiwa katika baadhi ya hospitali ambazo sasa hivi wameshakuwa wame-*invest* Zanzibar.

Sasa hospitali zile zina gharama, yaani unaweza ukasema sasa hivi India tunayo hapa. Mimi naomba basi hebu uanzishe ile *health insurance* ili watu-*insurance* kuweza kupata tiba ambazo tayari zinapatikana Zanzibar na itapunguzia hata

Serikali watu kwenda India kwa maradhi ambayo sasa hivi Zanzibar yanaweza yakatibika. Basi tunaomba sana  hebu ajaribu kuangalia katika mipango yao, ili tuweze kupata hii huduma ambayo inayo tija.

Mhe.Spika, Mfuko wa Barabara; ninawashukuruni sana lakini mimi naomba katika Mfuko wa Barabara tayari barabara yetu ya Kwa-Abass Hussein/Shaurimoyo/Mboririni mpaka Darajabovu mumeshaanza kuijenga lakini mumeijenga robo, watu wangu wanapata vumbi. Kipindi kama hiki kila siku pumu, kikohozi, mafua basi ninaomba Mfuko wa Barabara sisi fungu tutalipitisha, lakini ile sehemu iliyobakia basi mushirikiane na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ili mutumalizie.

Mhe. Spika, ZRB kwa kweli tunawapongeza sana pamoja na *TRA* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ninampongeza Mhe. Waziri na bajeti yake ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja, lakini zaidi ule ufafanuzi hasa katika maeneo huru, naomba, uje mpe nafasi ya kutosha atusaidie ipi mipango ya Serikali.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*).

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said akifuatiwa na Mhe. Marina Joel Thomas wakati Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi anajitayarisha. (*Makofi*)

**Mhe. Fatma Mbarouk Said:** Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa fursa hii asubuhi ya leo kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Kwanza nimshukuru yeye pia pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao mpaka kufikia kuisoma bajeti hii mbele ya Baraza lako Tukufu.

Pia nichukue fursa hii kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu wao na hasa hasa mume wangu kwa kunivumilia kwa muda mrefu pale ninapokuwa kwenye majukumu ndani ya nchi na hata nje ya nchi na kumuacha kumweke nyumbani akiwa peke yake pamoja na watoto wetu.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kitabu hiki, kwa kweli kwanza kitabu hiki nimpongeze sana Mhe. Waziri ambae kwa njia ya peke yake, au kwa mfumo wa peke yake ambapo mpaka majina hakutaka kupandika ile karatasi hapa juu, lakini

moja kwa moja imechapishwa. Kwa hivyo, nimshukuru sana. Naomba na wizara nyengine hiyo miaka itakayokuja waandae vitabu kama hivi vya kileo.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki niende katika ukurasa wa 7 ambapo kuna utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka 2014/2015 ambayo ni kuandaa kutoa miongozo na kusimamia bajeti ya serikali. Niipongeze sana wizara kwa kufanyakazi kwa uwajibikaji mkubwa, hata kufikia hapa leo.

Mhe. Spika, nikienda kwenye Idara ya Bajeti, kwa kweli idara hii ni kama nilivyosema, kwamba ina majukumu makubwa na uwajibikaji uliofanyika kwa mwaka huu umekwenda kwa mfaumo mpya wa PBB, kuandaa vitabu vya bajeti kwa mwaka 2015/2016. Yote haya ni majukumu ambayo wameyatekeleza kwa kiasi kikubwa na kugharimika sana kwa mujibu wa matumizi haya waliyotumia hapa.

Mhe. Spika, katika ukurasa namba 9 Idara ya Mhasibu Mkuu. Kwanza niishukuru idara hii na nimpongeze kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato ambayo wamejionesha ndani ya kitabu hiki. Usimamizi mzuri pamoja na kuimarika kwa misingi bora ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwa kweli hili ni jambo la kupongeza na ambalo linaonekana kwamba kuna ukuaji wa mapato unaokwenda sambamba na ukuaji wa uchumi.

Kwa hivyo, niishukuru sana na niseme hii ni Idara yangu mama, kabla ya hapo nilikuwa ni Mhasibu wa Idara ya Nyaraka na nimepata mafanikio makubwa kwa kunifunza na kuwa ni mtu ambaye niliwajibika vizuri mpaka kufikia hapa, sikupata kashfa hata moja ya kusema kwamba nilitumia vibaya fedha hizo. Nilikuwa nasimamia vizuri na kufuata zile sheria pia za manunuzi. Kwa hivyo, nizidi kuwaambia Wahasibu wenzangu hili jambo ni la msingi kabisa.

Mhe. Spika, kwa upande wa matumizi ya serikali ambayo yamefanyika, haya yaliyojionesha katika ukurasa wa 10. Inasema kwamba kuna fedha ambazo mara nyingi tunakuwa tunawategemea wahisani. Hivyo, niiombe wizara sasa tuondokane na huko kutegemea fedha kutoka nje, kwa sababu tunaona ni namna gani taasisi hizi zinasuasua.

Mhe. Spika, mambo yanayohitajika zaidi ni kutekeleza kuimarisha uwazi na ufanisi katika kufanya manunuzi ya umma, ni muhimu kuandaa mipango kazi kabla ya kufanya manunuzi. Vile vile *Public Procurement System* ni muhimu zaidi, hii ni lazima iwepo, bila ya hivi basi matumizi yetu yatakwenda ovyo. Tuhakikishe manunuzi pia yawe ya kiuchumi, yasiwe ya fedha nyingi ambazo zinatumika.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 13 tumeona kwamba kuna changamoto kubwa inayoikabili serikali, ni kutokuwa na uhakika wa upatikanaji wa miswada, ambayo nimeshaizungumza huku. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, hilo ni jambo la lazima. Vile vile kuna hii Idara ya kusimamia mali na mitaji ya serikali inayowekezwa katika Kampuni mbali mbali, pamoja na Mashirika ya Umma.

Mhe. Spika, kwa kuwa mali hizi zinatakiwa zitathminiwe, kwa hivyo naomba tu Mhe. Waziri na nimuulize, kwa sababu mali hizi baada ya kuwa zinatathminiwa na vile vile kutiwa kwenye *register* na pia ni lazima ziwe na thamani. Sijui kama wanao huu utaratibu wa kutathamini hizi mali wameshakuwa, kwa sababu nyuma tulikuwa tunajua kulikuwa kuna mapungufu ya hawa watathmini.

Vile vile Mhe. Spika, nipongeze kwa Idara hii ya uhakiki mali kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imesimamia upatikanaji wa TSH. 3,920 milioni kama ni mapato yanayotokana na ukodishwaji wa uwekezaji wa mali za serikali. Mapato haya sawa na asilimia 23. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri nipongeze sana idara hii. Vile vile ukurasa wa 15 Idara hii imesimamia ufufuaji wa Kiwanda cha Sukari katika kipindi cha majaribio. Kiwanda kimeweza kuzalisha tani 200. Kwa hivyo, niombe na vile viwanda vyengine vyote tulivyokuwanavyo, kama tulikuwa na Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Siagi navyo basi vifufuliwe ili tupate mapato na kukuza pato letu la taifa na vile vile tutapata ajira kwa watoto. Kwa hivyo, viwanda vyote vile tulivyokuwanavyo viwe endelevu pia. Kwa hivyo, Mhe. Waziri niombe na vile viwanda vingine basi ili tupate ajira kwa watoto wetu.

Mhe. Spika, pia Idara ya Uendeshaji na Utumishi, hii nayo ni idara mama katika wizara na imetoa mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi, hilo ni moja ya majukumu yake. Naona humu kuna mambo mengine nayo ni muhimu vile vile kwa sababu inamfanya yule mfanyakazi kuwa na *moral* ya kila mwaka ambapo anatakiwa aende likizo na ile stahiki yake apewe.

Mhe. Spika, najua tuna matatizo mengi, lakini stahiki nayo iwepo, kwa sababu baada ya mwaka mzima, baada ya kwenda kupumzika yeye na watoto wake huko nyuma tulikuwa tunajua, kwamba mtu akienda likizo anapewa yeye na familia yake stahiki, mkewe pamoja na watoto wake wanne. Lakini sasa kutokana na hali ya fedha labda hakuna, lakini angalau basi ile pesa ndogo basi mfanyakazi apewe ili aweze kupumzika vizuri. Haiwezekani kuwa anakwenda likizo bila ya fedha yoyote, ingawa ilikuwa sio sheria, lakini ilikuwa ni kama utaratibu ulikuwepo kwamba unapokwenda likizo unapewa Afrika ya Mashariki hii nzima; unapewa ule uwezo au unawezeshwa kutembea hii Afrika ya Mashariki. Lakini sasa hivi kwa kweli tunapata fedha ndogo kwa likizo.

Mhe. Spika, hapa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, inaonesha ni namna gani madeni yanavyokua. Kwa hivyo, ningemuomba waziri haya madeni basi tupunguze kidogo kidogo, yasiwe yanakutana, mwisho tutakuja kuuzwa pamoja na sisi ikiwa hatutolipa madeni haya. Mhe. Waziri hili ni jambo nalo la kuliona kwamba madeni tusikae tu malimbikizo ya madeni. Unakopa basi unalipa, na humu muna madeni ya ndani na madeni ya nje. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ni lazima haya madeni tuyalipe kwa wakati.

Mhe. Spika, taasisi nyengine ambayo naona niipe pongezi ni hii ya Benki ya Watu wa Zanzibar, kwa kweli tulikuwa na wasi wasi wa kwamba labda haitojiendesha kutokana na yale madeni, au kutokana na amana na halafu zile pesa labda zinatoka kwa mambo mbali mbali ili tuweze kuona kwamba benki yetu haitoanguka tena, iendelee kufanya kazi zake kwa vizuri kwa mitaji yake ambayo itakuwa ni lazima kuwe na faida na hasara. Lakini ikiwa kuna faida kubwa basi inatuonesha kwamba ni namna gani kama inapata faida na kuendelea kwa benki hii. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na uwajibikaji mzuri na fedha ile inayokopeshwa, basi irudishwe vizuri ili benki yetu iweze kuwa na *standard* ile ile ya kuweza kuendelea.

Mhe. Spika, na Shirika la Bima pia nilipongeze ingawaje wenzangu wamesema ianzishwe Bima ya Afya; ni kweli, ni lazima ione mwahali kama humu mwa kuwekeza. Kwa sababu hivi sasa kuna hizi bila ambazo mara nyingi zinakuwa ni za ajali na inatokezea kama ajali imetokezea basi lazima ilipe, kwa hivyo ni lazima itafute na mbinu mbadala nyengine. Vile vile nilishukuru sana Shirika la Bima kwa kuanzisha ofisi zake mbali mbali na kuwa na wakala wa kanda, kwa ufanisi mkubwa tumeona ni namna gani Shirika la Bima liko maeneo mbali mbali. Tulipokuwa tukipita na kamati yangu ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali, tulikwenda tukaona maeneo mbali mbali kwamba wanaendelea vizuri na waendelee hivyo hivyo, ili shirika letu liende vizuri na lisije likafilisika.

Mhe. Spika, kitabu hiki cha bajeti kimeeleza mengi na kwa kweli sina ambapo nimeona kuna tatizo lolote isipokuwa nichukuwe fursa hii na mimi nimpongeze waziri pamoja na watendaji wake. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani, naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Marina Joel Thomas:** Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha, kwa mwaka fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, kwanza napenda kuwatakia Ramadhani njema Waislamu wote, Mwenyezi Mungu akujalieni mufunge kwa salama hadi hapo mtakapomaliza.

Akuepusheni na shari, kwa hivyo nawatakia kila la heri kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuipongeza serikali kwa utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, ambapo imetimiza karibu asilimia 90 ya utekelezaji wake. Nasema hii ni hatua kubwa na asilimia 10 iliyobaki tutaimalizia hapo baadae, lakini asilimia 90 ya ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezaka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia napenda kutoa pongezi kwa serikali kwa suala zima la uwekaji wa taa za *CCTV* camera katika maeneo ya Mji Mkongwe, hii ni hatua nzuri na ni hatua ambayo itasaidia kupunguza mambo mengi ya uhalifu au mambo mbali mbali yanayotokea ya kuhatarisha nchi yetu. Nasema naipongeza sana serikali kwa hili.

Pia Mhe. Spika, nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wake wote wa wizara hii kwa kazi kubwa na kazi nzuri ambayo wanaifanya. Vile vile nazipongeza taasisi ambazo zinasimamiwa na Wizara ya Fedha, zikiwemo *PBZ, ZRB,TRA,ZSSF,* Mfuko wa barabara na kadhalika. Nazipongeza taasisi hizi kwa kazi nzuri za nakusanyo ya fedha na huduma mbali mbali ambazo wanatoa katika nchi hii.

Mhe. Spika, nitakwenda katika maeneo kama manne hivi. Eneo la kwanza ni Bodi ya Mapato, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Ufuatiliaji na Uratibu wa Mikopo kutoka Washirika wa Maendeleo na Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi.

Mhe. Spika, maendeleo ya nchi yoyote duniani yanachangiwa na kodi, tunapozungumzia madawa hospitalini maana yake ni kodi, tunapozungumzia elimu bora maana yake ni kodi, tunapozungumzia maji safi na salama maana yake ni kodi. Huduma zote hizi zinahitaji kodi na kodi ndio inayoendesha maendeleo mbali mbali ya nchi yetu.

Pia Mhe. Spika, napenda niipongeze Wizara ya Fedha kwa kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato na hasa ukiangalia katika suala zima la mapato ya Visa kwa njia ya mashine ya Uwanja wa Ndege, imeonesha mafanikio makubwa. Nilisikiliza ripoti ya kamati walisema pesa za Kimarekani karibu milioni tatu, zimekusanywa kwa kipindi cha miezi 9, ukilinganisha na dola laki 400,000 kipindi cha nyuma ambapo kabla mfumo huu haujawekwa. Hii ni hatua nzuri na inastahiki pongezi serikali yetu.

Mhe. Spika, hapa naomba nitowe ushauri, licha ya wizara kuboresha mfumo huu wa ukusanyaji mapato, lakini pia na sehemu nyengine wangejaribu kuboresha mfumo huu, ili tuondokane na mfumo ule wa zamani wa kukusanya pesa kwa mkono. Hii naweza kuchangia upotevu wa mapato katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nakwenda katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii; mfuko huu katika kitabu hiki uko katika ukurasa wa 25, ambapo wamesema katika kipindi cha miaka 5 iliyopita, idadi ya wanacha ajira imeongezeka na kufikia 1,272 ikilinganishwa na idadi ya wanachama 926 waliokuwepo mwaka 2010. Idadi ya wanachama waajiriwa nayo imeongezeka hadi kufikia 74,890 kwa mwaka 2015 ukilinganisha na idadi ya wanachama waajiriwa 61,396, mimi nitazungumzia wanachama wale ambao wanachangia mfuko huu.

Mhe. Spika, kila taasisi ya serikali na mashirika wanachangia mfuko huu, wanachangia kutokana na baadae kupata mafao wakati wanapostaafu. Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri, kuna wengine hawafikii kustaafu, kuna wanachama wengine wanapata maradhi mbali mbali na pengine mtu anaweza kupata maradhi hata kazini asiende tena.

Kwa hivyo, nilikuwa naiomba wizara hapa ipange utaratibu basi, angalau huyu mtu ambaye yupo kitandani pengine ana hali ngumu na hana watu wa kumuhudumia, hiki chake ambacho amechangia wakati alipokuwa mzima na afya yake anafanyia kazi, basi apatiwe katika kipindi kile ambacho yupo katika hali ile tusimngoje astaafu, kwa sababu kustaafu kunategemea. Wengine wanaweza wakafariki kabla ya kustaafu, lakini kwa hawa wengine ambao wanapata maradhi ambapo pengine hawezi tena kuendelea kazini na amechangia katika mfuko huu. Kwa hivyo, ufanywe utaratibu ili wale watu waliokuwa katika hali hii watengewe zile fedha angalau zikaweza kuwasaidia katika huduma ambazo yupo kitandani. Kwa sababu alipokuwa na nguvu zake aliitumikia nchi hii na anahitaji kupata fedha zile kwa ajili ya matibabu.

Mhe. Spika, nakwenda katika Mamlaka ya Vitega Uchumi; pia naipongeza serikali kwa miradi mbali mbali ambayo imeisaidia nchi yetu kuingiza mapato na maendeleo. Lakini siku za nyuma kulikuwa na utaratibu, miradi kama hii ya vitega uchumi zinaletwa taarifa katika ngazi ya wilaya, mikoa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, wanaleta ili kama kuna mradi fulani ambao utafanyika katika labda shehia fulani au mkoa fulani. Kwa hivyo tunakuomba Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa utowe maoni yako kuhusu mradi huu. Basi wilaya au mkoa unakwenda katika sehemu husika inaangalia na kuuliza baadhi ya watu katika eneo lile, halafu inatoa maoni yake.

Halikadhalika na ngazi ya mkoa na pia ngazi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Lakini nahisi utaratibu huo siku hizi haupo, kwa sababu nimeulizia mimi utaratibu huo haupo na utaratibu huu ulikuwa ukisaidia sana hata kupunguza hii migogoro mbali mbali inayosababishwa na wenyewe wategauchumi au wale wananchi wa pale, lakini wakipewa taarifa hii mapema kwa sababu mimi nakumbuka nilikuwa nishashiriki na nishakwenda kwenye sehemu kama Afisa

Mipango nimekwenda zangu nikakaa na watu, nimechukua timu yangu ya uchumi katika ngazi ya Wilaya ya wataalam tunakaa tunakwenda katika eneo husika, tunauliza watu wanatupa maoni yao, tukifika ofisini tunatoa taarifa Wizara ya Fedha kuhusu mradi ule, mradi huu labda mzuri na una faida hii na hii, lakini unachangamoto hizi na hizi.

Kwa hivyo, Mkuu wa Mkoa na pia Mkuu wa Wilaya wanatoa taarifa zao, Wizara ya Ardhi nayo inatoa taarifa yake, baadae tena Wizara ya Fedha nayo inachukua hatua ambayo inaweza kufanya, lakini sasa hivi utaratibu huo haupo na utaratibu huu unasaidia Mhe. Waziri, ulikuwa ukisaidia sana na ndio maana sasa hivi kuna migogoro mbali mbali inajitokeza kwa wananchi hata kwa wawekezaji. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nahisi ule utaratibu Mhe. Naibu Waziri, urudie unasaidia kiasi fulani na si kama mtu amekaa juu ya meza anatoa maoni yake tu lakini anakwenda katika sehemu husika anangalia anatoa maoni yake, Mkuu wa Mkoa anatuma wataalam wake, Mkuu wa Wilaya anatuma wataalam wake na wanatoa maoni kuhusu mradi ule.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri, nilikuwa nashauri utaratibu ule urudishwe kwa sababu hata Wizara ya Ardhi nao pia hawapati hiyo, ingawa nimefuatilia na nimeuliza pia nao walikuwa wanakwenda wanatoa maoni yao kuhusu utaalamu wao kuhusu ardhi ya eneo lile, kwa hivyo, wewe Wizara ya Fedha unakuwa usharahisisha ile kazi unakwenda kwa kuthibitisha tu, lakini nahisi utaratibu huu ni mzuri unaweza kusaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nakwenda katika suala la Uratibu wa Misaada na Mikopo ya Maendeleo. Mhe. Spika, misaada ni mizuri na mikopo ni mizuri, mikopo inasaidia nchi yetu kufanya miradi mbali mbali ambayo inaweza kuinua pato letu la Taifa, lakini mikopo ina masharti yake na mtu akipewa mkopo atakwambia nitakupa mkopo huu lakini kuna masharti, hakuna mkopo unaopewa usiwe na masharti huo ni ukweli.

Kwa hivyo, inategemea na masharti yenyewe pengine yanaweza kuwa magumu, masharti mengine yakawa mepesi, kwa hivyo, nilikuwa nahisi hapa Mhe. Spika, ishafika wakati nasi tujipange tusikae tukaitegemea sana mikopo tukajisahau, maana yake kwa sababu mikopo baadae itakuja kutuathiri pakubwa tu, kwa sababu unaweza kuanzisha miradi baadae hafla mfadhili akakatisha pengine katika masharti yake aliyokupa hujatekeleza, kwa hivyo, inaathiri kiasi fulani katika shughuli za maendeleo.

Mimi namshauri Mhe. Waziri, azidi kubuni vyanzo vyengine vya mapato ambavyo vinaweza kusaidia kuliko kuwa tegemezi sana karibu ya asilimia sabini sitini inategemea wafadhili, tunakwenda siko huko Mhe. Spika, lazima na sisi tubadilike

tuzidi kuanzisha vyanzo vyetu vya ndani mbali mbali ili tuondokane na huu utegemezi, utegemezi ambao unaweza kutuletea matatizo hapo baadae Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kumalizia huo ndio mchango wangu, kwa hivyo, baada ya kuchangia mchango huo Mhe. Spika, naomba niunge mkono hotuba hii ya bajeti asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Spika.*(Makofi)*

**Mhe. Mwajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo kuchangia kidogo tu hotuba hii ya Mhe. Waziri, lakini vile vile kwanza niseme sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha leo nikiwa salama pamoja na wenzangu hapa, lakini vile vile niwatakie Wajumbe Ramadhani njema na tukufu kwa mwezi huu wa funga.

Mhe. Spika, mimi nitaanza kidogo tu na Shirika la Bima, nikija katika Shirika la Bina ukurasa wa 26 hapa unaosema kwamba;

> "Shirika la Bima la Zanzibar lilijipangia kutekeleza malengo yake mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yake."

Mhe. Spika, lakini niseme pamoja na ukusanyaji wake wa mapato na kuvuka lengo zaidi lakini bado Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, shirika bado linahitaji kuwahudumia wateja wao hasa pale wanapotokezewa na matatizo ya ajali. Lakini vile vile Mhe. Spika, shirika linapaswa kuzidisha mashirikiano kwa mawakala ikiwa ni pamoja na viongozi wa shirika katika mashirika mbali mbali yaliyoko nje ya Mji wetu wa Zanzibar kama vile Shirika la Bima Arusha kwa kuwatembelea na kuwasikiliza maoni yao ili waweze kutoa matatizo yao.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nikija katika Bodi ya Mapato *ZRB*, kwanza naipongeza bodi hii kwa kuvuka lengo la makusanyo yao, lakini vile vile niseme katika kodi ilikadiriwa kukusanya jumla Shs. 181,000,300.0 ya utekelezaji halisi katika kipindi cha Julay/Mei 2015. Lakini vile vile niseme Mhe. Spika, makusanyo haya waliokuanya walikusanya Shs. 160,000,829.92 milioni sawa na asilimia 89 nawapongeza Mhe. Spika, lakini je, niseme kwamba mwaka 2013/2014 ambapo mapato yao jumla ni Shs. 146,597.71 milioni. Lakini niseme hivyo hivyo katika makusanyo ambayo hasa aliyokusudia Shs. 181,000,300, kwa nini hayakufikia lengo na wakapata Shs. 160.829.92. Naomba Mhe. Waziri, atakapokuja aje anifahamishe vizuri.

Mhe. Spika, nikija katika mfuko wa barabara ukurasa wa 29, mfuko wa barabara kazi yake ni kukamilisha maendeleo ya barabara, lakini nataka nimuulize Mhe. Waziri, pamoja na mifuko hii ambapo inatolewa mifuko kwa ajili ya kujengea barabara, kwa nini barabara ambazo zinatolewa ule mfuko na tayari fedha

zimeshatolewa, kwa nini barabara zile inakuwa hazitengenezwi na mfuko tayari umetolewa. Je, Mhe. Waziri, huoni hii inakutia kasoro Wizara yako wakati wewe mfuko umeshatoa lakini barabara zile zinakuwa hazitengenezwi.

Mhe. Spika, nije katika Chuo cha Uongozi cha Chwaka, Chuo hiki kinahitaji kuendelezwa Mhe. Spika, kwani Chuo hichi ndio kinachotoa wataalam wetu zaidi na chuo hichi ndio chenye fani zaidi hapa, kwa hivyo, Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri, Chuo hichi afanye jitihada za makusudi ili kuzitilia fedha na kuweza kuendelezwa chuo hichi ili kiweze kutoa wataalam ambao ni wa fani hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, nikija katika *ZSSF*, ukurasa wa (25). Niseme kwamba Mhe. Spika, mfuko huu wa hifadhi unahitaji kuongezewa taaluma juu ya huduma mbali mbali zinazotolewa na mfuko huu Mhe. Spika, ili wananchi wawe na mwamko zikiwemo huduma za uchangiaji mpya wa mfuko wa hiyari. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, hapa atoe taaluma zaidi kwa sababu kuna watu wengine bado hawajaelewa nini mfuko wa *ZSSF*, sasa watakapopata  taaluma zaidi naamini wateja watakuwa wengi.

Mhe. Spika, nikija katika Idara ya Uhakiki Mali, Idara hii kuna haja ya kupatiwa nyenzo na nyenzo zaidi za kitaalam kwa sababu Mhe. Spika, kazi yoyote ile ikiwa haina nyenzo inakuwa ni matatizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, Idara hii aipatie nyenzo za kufanyia kazi zinazolingana na uzito wa kazi zao, Mhe. Spika, hususan kisiwani Pemba, namuomba Mhe. Waziri, hili aliangalie sana kwa kina.

Mhe. Spika, mwisho nije katika *ZRB* na *TRA* Mhe. Spika, huoni kuwa kuna haja kubwa ya kuimarisha ulinzi wa doria katika Wizara hii ya *ZRB*, kwa sababu mambo mengi ambayo wanayafanya katika bahari ni kuchukua mambo mengi, kwa mfano kama mafuta, meli za mafuta zinapoingia pale huwa watu wanaiba mafuta yale na kuyasafirisha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, azidishe ulinzi wa doria wa baharini ili kuepukana na matatizo mengi yanayotokea katika kazi hii.

Mhe. Spika, baada ya hapo nilisema leo sina mchago mkubwa na sijisikii vizuri, naomba uniruhusu nikae. Ahsante nashkuru. (*Makofi*)

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na hatimae kutupa uwezo na nguvu za kutosha hadi hapa katika Baraza hili tukufu. Aidha, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nadhani Mhe. Spika, sitakutendea haki kama na mimi sikukupa shukurani za dhati kwa kuweza kutia angalau nyalio kidogo kwa sababu mimi si msemaji mzuri katika mambo ya fedha, angalau nitie tie nyalio tu kidogo, si haba nashukuru sana kupata nafasi hii.

Mhe. Spika, Nimalizie kwa kumpongeza Mhe. Waziri, kwa kweli pamoja na benchi lake la ufundi wametoa darasa kwa Serikali mara hii, mara nyingi unajua Mhe. Spika, hivi vitabu huwa vinababaisha unaona vikaratasi hivi hubanduka, ikabidi mtu hajapata na nini kwa sababu vikaratasi vinabanduka banduka, lakini Mhe. Waziri, kaipa Serikali nzima darasa kwamba sasa majina ya vitabu yakija yanakuja moja kwa moja kitabu na jina. Kwa hivyo, nampongeza Mhe. Waziri, pale mtoto wangu Omar Yussuf na Katibu Mkuu wake kwa kuweza kufaya hii kazi nzuri.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja katika hoja zilizopo mbele yetu, mimi naona kwanza nianze na huu mfuko ambao Mhe. Waziri, ameueleza kwa kina sana katika ukurasa wa 28. Mhe. Spika, Zanzibar ni visiwa viwili vidogo hivi, kwa hivyo, Zanzibar si rahisi kusema wewe unatoka Mkoani unakwenda Konde kwa ndege, si rahisi kutoka Tumbatu ukasema unakwenda zako Mkaunduchi kwa ndege aaa, hapa aidha unaweza kutumia mashua au barabara hizi. Kama kuna mfuko muhimu sana ambao unahitaji kutunzwa pamoja na kujazwa basi ni huu mfuko wa barabara, kwa sababu ni mfuko pekee ambao unazitunza, unazilinda na unazihifadhi hizo barabara zetu. Sasa kama kuna jambo la kutunzwa kwa hapa Zanzibar basi ni huu Mfuko.

Mhe. Spika, kazi za mfuko huu ni kufanyia matengenezo barabara zetu ili barabara ziweze kupitika pamoja na kusafirishika mazao barabara nyingi hasa za vijijini huwa zinasinyaa sana kutokana matumizi pengine mazito yanayofanywa na baadhi ya Wizara ikiwemo hii Wizara ya Miundombinu hii, Miundombinu inajenga barabara lakini halafu Miundombinu hiyo hiyo barabara hizi inazichafua kwa kiasi kikubwa sana.

Mhe. Spika, kwa mfano sisi watu wa pale Vitongoji pale tulikuwa na shida sana kutoka barabara ya Machomane/Vitongoji mpaka kufikia Makaani pale, nafurahi Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamo wa Pili mdogo wangu pale Mohammad kafurahi sana kwa sababu ni barabara anayoipita mara kwa mara, barabara hii ilijengwa katika kiwango kizuri na kipindi kile cha Mhe. Amani na tuliipa jina mgongo wa ngisi, ulikuwa unateleza kabisa, yaani unapita na gari yako unatelea kabisa, na kama hukuangalia ukiwa kama unatoka Machomane kuja Wawi hapa basi unajikuta umefika Vitongoji bila ya kujijua kwa barabara ilivyokuwa inateleza.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwaba barabara ile ile tuliyokuwa tunaiita mgongo wa ngisi sasa imekuwa mgongo wa taa kwa sababu imechanika chanika sana, ni tatizo, hii ni kutokana na kwamba hawa wawekezaji hawa, haya mapampuni yanayokuja tukayapa kazi za kutujengea barabara nyengine wanakuja wakichukua kifusi kule kwetu Vitongoji, wakichukua mawe, wakichukua na *hard core*

nyengine kule katika magari yao ya tani kumi kumi na sisi tulijenga barabara hii ya mgongo wa ngisi kwa kupitia gari angalau tani tano hivi, lakini wanabeba mpaka tani kumi, kumi na tano katika magari hatimae barabara ile imesinyaa sana.

Mhe. Spika, sasa nasema mfuko huu ni muhimu kwa sababu ndio unatakiwa ufanye zile *minor renovation* ya ile barabara, sasa inasikitisha sana kwamba mimi naona huu mfuko vyanzo vyake havitoshi vya kujazwa huu mfuko ili ukafanya *major innovation* za barabara ikiwemo barabara ya kwangu Machomane/Vitongoji. Mheshimiwa, inasikitisha sana haya makampuni yanakuja tunayapa kazi yanatuharibia barabara yakishatuharibia barabara yanaondoka hivi hivi, inasikitisha, sasa mimi leo nadhani katika chanzo kimoja cha mfuko huu Mhe. Waziri, hapa mwanangu pale Omar Yussuf naomba sana katika vyanzo vya mfuko huu iwe ni pamoja na *ten percent* ya makisio ya ujenzi wa mradi unaopewa kampuni basi *ten percent* iingizwe katika mfuko huu ili upate nguvu ya kupata *minor or major renovation* iweze kupata nguvu. Leo haya makampuni yanatufanyia ujeuri.

Mhe. Spika, vile vile, wakiweza kutoa huko kwao haya makampuni kwa mfano *H. Yang* pale wanapitisha madude yao wanatuharibia mpaka lile daraja, sasa nilikuwa naomba niulize tu hapa Mhe. Waziri, kwamba mfuko huu unafanya matengenezo ya barabara je, vipi madaraja inafanya matengenezo ya madaraja madogo madogo, daraja la Vitongoji lile linalounganisha Vitongoji na Chake Chake ambalo lipo pale karibu na Umangani pale nyumbani kwangu limekuwa bovu sana. Mhe. Mohammed Aboud, anapenda sana kutembelea tembelea pande za kule, daraja ninavyokwambia Mhe. Waziri, ni bovu lile wakati wowote linaweza kusababisha hatari, sasa ikiwa huu mfuko wa barabara una nguvu kidogo, maana nilimwambia Waziri hapa wa Mawasiliano, naona sikuona hata kujibiwa suala langu.

Sasa naomba ikiwa huu mfuko wenu una uwezo wa kutengeneza mpaka madaraja basi itupie jicho lile daraja la Vitongoji lile, limekuwa bovu ukienda vyuma vimechanika ile *concrete slab* imeshaanza kumeguka kwa chumvi na wakati wote magari makubwa yanapita pale pale, basi naomba tuzibe ufe kabla hatujajenga ukuta na watu wakubwa wakubwa wanaopita katika daraja lile akiwemo Waziri wa Nchi, (OR), Makamu wa Pili wa Rais, ambaye anapita mara kwa mara kwenda kuwaangalia jamaa zake Changuo na sehemu ya Umangani pale. Sasa mimi ninadhani tuijenge hii daraja ili mambo yawe mazuri pale.

Mhe. Spika, niende katika Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi. Hii Mamlaka kazi yake kubwa ni kuwashajihisha wawekezaji wa nje na ndani pamoja na kurahisisha mchakato wa uwekezaji. Hii ni taasisi muhimu sana, lakini naona kama taasisi haipo makini kwenye kufanya shughuli zake ya uhamasishaji.

Mhe. Spika, hii naona haiangalii mazingira ya nchi. Taasisi ilikuwa inataka iwahamasishe wawekezaji kwa mujibu wa mazingira ya nchi. Kwa mfano, sisi katika utajirisho ni kumfanya mtu aweze kupata maisha kutokana na mazingira yaliyomzunguka. Ikiwa kazungukwa na bahari aweze kuishi kwa mujibu wa maji ya bahari, kazungukwa na ardhi yenye *fertile* tumuwezeshe, hiyo ndiyo *Enrichment policy*, yaani huo ndiyo utajirisho.

Mhe. Spika, hawa ndugu zetu wa Mamlaka hii ya *ZIPA* inaonekana hawafanyi *thorough feasibility study* katika kuwasaidia Wazanzibari na katika kuisaidia nchi. Nchi yetu imezungukwa na bahari, nchi yetu inapata mvua mara tatu kwa mwaka. Sasa mimi ninashangaa wao wanaelekeza kazi kwenye utalii tu, katika mambo haya ya ardhi na mbolea hii iliomo katika kuendeleza kwenye kilimo na kuwekeza kwenye bahari hatuoni kama wanajihisha kwa kiasi gani. Hili ni tatizo, wameganda kwenye utalii tu.

Kwanza katika hili ninapenda nimpongeze sana mwekezaji Said Salim Bakheressa, ninampongeza sana yule jamaa, ana imani na sisi sana Wazanzibari na huu ndiyo uzalendo. Yeye hivi sasa kaona kwamba Wazanzibari wamejikita katika mambo ya mifugo nikiwemo mimi hapa, kaweka Kiwanda cha Maziwa pale. Ninadhani niweke sawa tu *Hansard* kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma, kasema wanaagiza maziwa kutoka nje ya nchi, kwa nini asifanye hapa, aah! Mhe. Spika, yule ananunua maziwa ya hapa Zanzibar, lakini hayatoshi na yeye kenda mbali zaidi Bakheressa kwamba anatoa ng'ombe sasa, ng'ombe anakupa mmoja ufuge baadae mutakuja kuelewana. Sasa kwa hili Bakheressa mimi ninamsifu, kaenda angalau kwa wafugaji. Nyinyi *ZIPA* hamujamuhamasisha, huo ni moyo wake tu, ila nyinyi munahamasisha kwenye utalii tu. (*Makofi*)

Sasa mimi ninadhani katika hili, hapa hatuna vile viwanda vya kuzindika kwa sababu bahari tunayo. Mimi ninamshauri ndugu Bakheressa akishajikita katika mambo ya maziwa basi aje kwenye bahari nako, samaki wanapatikana sana na wakubwa tu hivi hivi. Maana yake sisi tunavua samaki hatuna pa kuwauza, dagaa lile tunavua linaozeana wenzetu wanatupa hatunonoki. Kwa hivyo, vile vile, tunamsifu kwa hili na namuomba Bakheressa awekeze sasa katika mambo ya *chemical industry specially* katika *marine chemical industry* kwenye mambo ya kusindika sindika hawa samaki na hali ya uokoaji vile vile.

Mhe. Spika, nyinyi *ZIPA* muwahamasisheni hawa, inasikitisha kwamba bahari tuliyonayo hatuna hata kiwanda kimoja sisi hapa cha kusindika samaki. Kazi yenu nyinyi ni kuwekeza kwenye utalii na mambo mengine, fukwe zote hazipatikani tena, hata pahala pa kwenda dago sasa hivi ni shida, mule mwahala mwa kwenda dago sisi wavuvi hatupati kwa sababu ya nyinyi, munaweka Wazungu, Wataliana

sisi hatupati kupiga kambi tukavua. Hili ni tatizo. Tujengeeni kiwanda cha kusindika samaki muone hapa. (*Makofi*)

Halafu kuna hizi *Agro-processing industries*, kwa mfano pale shambani kwa Mhe. Mohammed Aboud, kuna embe mviringo na boribo kubwa nyingi zinaoza pale, yaani shambani kwao huwa mimi ninapita pita haya maembe hayana mlaji. Kwa nini sisi tununue *Azam juice* na tusitengeneze pale na kuyaachia maembe haya. Lakini ninamsifu vile vile ndugu Bakheresa magari yake siku nyengine huja yakanunua maembe kwenye mashamba ya Mhe. Mohammed Aboud na shambani kwangu kule. Kwa hili ninamsifu sana na tunamuomba na sisi hapa atuwekee *Agro-processing industries* ili tuweze kusindika maembe na nyanya hapa, zile *tomato paste* zinazotoka Maweni tunanunua sisi, ni aibu, mimi ninaona aibu kununua *tomato paste* kutoka Mascat. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nadhani katika hili watu wa *ZIPA* muwe makini sana. Tushafika ile *point of elastic limit* katika mambo ya *tourism*, imeshakuwa *exceeded*. Kwa mfano hivi sasa fukwe zote zimejaa. Kasa wale wanakuja siku nyengine mimi ninatembelea kufanya mazoezi, kasa wanakuja juu kuna Wazungu, baadae kasa wanakimbia wanarudi baharini, wapeni nafasi hawa kasa katika baadhi ya sehemu, waondoshwe watalii wale ili hawa kasa waweze kupata sehemu ya kutaga. Mhe. Spika, inasikitisha sana kasa hatagi baharini, anataga juu. Yule ana *double life*, ana-*spends* maisha yake wakati mwengine katika *marine habitat* na wakati mwengine anakuja huku kupumzika katika *torrential habitation* pamoja na kufanya tendo la kuzaa na kuzaa kabisa huku. Sasa ufukweni hakuna nafasi tena kwa sababu watalii wako wengi huku. Hii ni *point of elastic limit* ya mambo ya *tourism* imeshakuwa *exceeded*, anajua Katibu Mkuu Khamis Mussa hapa, kwa sababu mimi sikusoma *physics* ila yeye mwenzangu kasoma *physics*, atatufahamisha zaidi katika mambo haya, kwamba tumeshafika *point of elastic limit* kwenye masuala haya. Sasa tupelekeni kwengine. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kuna miradi hii iliyokuwa hata haifanyiwi upembuzi na uchunguzi yakinifu. *ZIPA* tunawaomba muwe makini sana, hivi sasa kule Uvinje alikozungumzia Mhe. Farida Amour Mohammed, pale, kunataka kujengwa tena chumba cha chini, kama hichi chumba cha chini ya bahari kilichopo huku Makangale. Je, mushafanya *Environmental Impact Assessment*, kwa sababu ninasikia kile chumba hakikufanyiwa ile *Environmental Impact Assessment*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa je, kama hakikufanyiwa na munataka kuongeza vyumba vya chini kama Uvinje huku, kila mmoja sasa anataka kutengeneza vyumba vya chini ya bahari. Sasa ikiwa ni hivyo, hichi cha hapa mushakifanyia *Environmental auditing*, ili kama kuna athari tuzuie na kule. Musikimbilie mapesa tu Zanzibar, mukimbilie

na mambo ya *Environmental degradation within the marine*, muangalie hilo, musiangalie kupata pesa tu baadae mukaangamiza viumbe vyengine.

Mhe. Spika, mimi ni mtu wa *ecology*, muna-*disturb* mazingira ya bahari kule kuhusu yale ma-*glasses possibly* yana-*cause fabric material,* munaweza mukaondosha *spices* nyengine za samaki kule ikiwa hamukufanya utafiti wa kina. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naomba kwa Mhe. Waziri, akija hapa anieleze, je, katika kuwekeza hivi vyumba kwa wawekezaji hichi chumba cha baharini kilichopo kule Makangale kilifanyiwa *Environmental Impact Assessment* (*EIA)* na kama hakikufanyiwa na huku kunataka kuongezwa vyengine kama Uvinje na Vitongoji, sijui vyengine vinataka kuongezwa wapi huko. Jamani hamutakuja kutuathiri samaki wetu baharini? (*Makofi*)

Mhe. Spika, ninadhani kwa upande wa Mamlaka ya Uwekezaji nimalizie hapo. Sasa niende katika masuala ya Benki ya *PBZ.* Kama kuna watu wa kusifiwa na kupongezwa basi ni watu wa *PBZ.*

**Mhe. Spika:** Bado dakika tano.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ninatumia fursa hii kuwapongeza sana *PBZ,* kwa sababu *PBZ* ilikuwa *ICU*, yaani mahututi. Lakini kabla sijawapongeza *PBZ,* niwapongeze na nyinyi Wawakilishi kwa kuweza kuizuia hii benki isibinafsishwe.

**Mhe. Spika:** Unazo dakika tano.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Maana yake ingebinafsishwa ni kama mtu angekuwa anauza roho yake.

**Mhe. Spika:** Unazo dakika tano.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, ninadhani zitanitosha hizo usiwe na wasi wasi wewe, unaona.

Mhe. Spika, mimi nadhani kuibinafsisha *PBZ* ni sawa sawa na mtu ambaye angebinafsisha roho yake kwa vile kusimama imara kwa Wawakilishi isibinafsishwe munastahiki pongezi sana na *keep it up*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hii *PBZ* ni mtoto wetu ambaye kwa kweli sasa hivi anatupati maslahi, lakini maslahi yanataka yapanuliwe. Kwa maslahi katika mambo ya uwekezaji kwa *PBZ* lazima mtaji uongezwe. Mimi ninadhani sasa kwanza tuwaongeze mtaji hawa

ili *PBZ* iendelee kutuhudumia kabisa kabisa. Mimi ninawapongeza hawa vijana wanatuhudumia vizuri tukenda pale wanatusaidia sana Mameneja wale wa Malindi na Forodhani na Mwanakwerekwe pale, tukenda kila upande tunawashukuru wanatusaidia. Kwa hivyo, hawa wanataka waongezwe mtaji. (*Makofi*)

Mhe. Spika, halafu mimi nina *point* moja kwamba *PBZ* wameshaanzisha *mobile service* kupitia simu za mikononi. Lakini nina kitu kimoja ninataka niwashauri hawa kwamba Wazanzibari, kama huu uchumi wa nchi unataka uwe *supported* vizuri lazima upanue sana *Rural economy* (uchumi huo wa vijijini). Sasa uchumi wa vijijini ni pamoja na wakulima wa karafuu na wavuvi waliopo Tumbatu. Hawa ndiyo wanaofanya uchumi wa nchi kupanuka. Hivyo, tu-*support* sana *Rural economy*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa inasikitisha sana kwamba mama aliyekodi karafuu, pengine mama wa miaka 50, 60 kakodi karafuu sehemu za Bogoa, Nanguji na Kiwani, anataka kulipa vibarua wake huyo kiguu na njia mpaka Chake Chake. Hili ni tatizo, akishatoka Chake Chake ana mapesa sasa kapu zima anakuja kulipa vibarua sehemu za Bogoa huku na yeye hana askari wa kumlinda na vibaka wamekuwa wengi na watu wanaokula unga. Mama wa miaka 60 akitokezewa na walaunga watatu tu wanaweza wakamnyang'anya mzigo wake ule wa pesa.

Mhe. Spika, sasa ninashauri, nadhani Mhe. Waziri, hanisikilizi tu sasa hivi, lakini ni *point* nzuri. Hii ni hoja nzuri ninayoijenga kwamba Mhe. Waziri, naomba unisikilize kidogo ninajenga hoja, kuwa kuna mchumaji karafuu Bogoa mwanamke ana miaka 60, anataka kulipa vibarua wake inabidi kule hakuna huduma za *PBZ*, anakuja Chake Chake kuchukua milioni 20, milioni 25 anakwenda kuwalipa vibarua wake sehemu za Bogoa, Nanguji, Kiwani, Gando huko, tena mtoto mwanamke na sasa walajiunga siku hizi ni wengi, akifika kwenye chochoro pale mara anabakwa na wanazichukua milioni 20. Sasa katika kunusuru hili, *PBZ* lazima watusaidie. Mimi katika kutembea nchi mbali mbali nimefika kule na nikaona kuna *Bank mobile ATM* na hizi zinakuwepo nchi mbali mbali kama Sharjah, Dubai na Oman. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa na hapa kwetu si geni hili, hata pale Dodoma Bungeni katika Bunge la Katiba kama mutakumbuka yalikuja magari ili kutupatia *mobile ATM*. Kwa nini isiwe *PBZ* sasa? *PBZ* anzisheni *mobile ATM* muende Tumbatu kwa wauza samaki kule, mwende Bogoa kwa watu wa karafuu kule, muje Vitongoji kwa sisi wachimba mawe na wakulima wa tungule kule, ili tusipate shida hizi za pesa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nimalizie tu kwa Benki Kuu ya Tanzania (*BOT)* kwa sababu umeniambia nina dakika tano na zitabakia dakika mbili tangu uliponiambia.

Urasimu katika *BOT* umekuwa mkubwa sana. Wizara ya Fedha sijui inaleta nini kwa *BOT*, kuna wale watu watatu wa Wizara ya Fedha sijui wanasaini, *BOT* wanamchakato wao, halafu kuna masaa sita ndiyo pesa uipate, huku watu wanasubiri mishahara. Wahasibu wa Mawizara wanapata shida, hata huu urasimu uliopo ni tatizo. Hizi pesa ni za walipa kodi lazima mupunguze urasimu ili Mhasibu wa Wizara akenda pale au Wizara ya Fedha ikileta *cheque* yake *BOT* haraka haraka ifanywe *process*, ili fedha zifike Wizara ufanisi upatikane. Leo anakuja pale anaambiwa baada ya masaa ya sita muda umeshapita wa kazi, huku mfanyakazi anadaiwa hajapata mshahara, ufanisi utapatikana hapo?

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, katika hili naomba kwamba hebu watu wa *BOT* mukazungumze nao watupunguzie urasimu ili Wahasibu wakenda pale kutaka mambo ya madughuli wapate haraka haraka ili wawape wafanyakazi wao na hatimaye ufanisi wa kazi upatikane.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mimi naunga mkono hoja hii kwa kiasi kikubwa sana. Ahsante. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Saleh Nassor Juma. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Bikame Yussuf Hamad, afuate baadae Mhe. Hassan Hamad Omar na baada ya hapo Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, atajitayarisha.

**Mhe. Bikame Yussuf Hamad:** Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara ya Fedha.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mapenzi yake kuweza kunijaalia kutoka nilikotoka mpaka nikafika hapa nikiwa nimo ndani ya hali ya uzima na afya, lakini pia kunipa uwezo wa kuweza kusimama kwenye chombo hichi. Kwa hivyo, sina budi niseme *Alhamdulillahi Rabil-Alamina.*

Mhe. Spika, lakini kwa sababu tumo ndani ya kipindi cha mwisho tena, ni vyema basi kuombana samahani kwa wale wote pengine tuliokosana. Nikianza na wewe na Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini kuanzia wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wote, Mawaziri wote wa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar na mpaka Mhe. Rais na Makamu wake wote wawili, basi kama kuna mambo tuliyafanya pengine kupitia chombo hichi hayaridhisha basi tuombane samahani na mimi kama kuna watu walionikosea basi mimi ninawasamehe na naomba na wao pia waweze kunisamehe. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia, ninataka nichukue fursa hii kuishukuru sana familia yangu kwa kuweza kuniruhusu kuvuka Kisiwa cha pili kuja hapa, kukaa siku kadhaa hasa hasa

mume wangu. Kwa sababu bila ya yeye nisingeliweza kufika hapa, kama Dini inavyoturuhusu. Kwa hivyo, nichukue fursa kumpongeza sana kwa ustahamilivu wake aliouchukua hasa katika kipindi hichi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kuweza kustahamili na kuniruhusu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri na kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma, kuwa kitabu chake mara hii inaoneshea kuwa watendaji wake wa Wizara wanatutambua sote katika Baraza hili, kwani vitabu vyote vinavyoletwa vya bajeti vinaletwa Barazani halafu vinawekwa vikaratasi, lakini kitabu cha Mhe. Waziri, moja kwa moja *originally* kabisa kimeweza kutambua majina yetu na kuweza kutuweka katika kitabu hiki.

Kwa hivyo, niwapongeze kwa hili, lakini pia kwa utendaji wao mzuri ambao umemuwezesha waziri wao kupitia kitabu hiki na kuweza kukiwasilisha hapa. Mhe. Waziri, kwa sababu wizara hii na mimi ninakumbuka miaka miwili na nusu nilikuwa ni mjumbe wa kamati, ninawapongeza na ninawashukuru sana kwa mashirikiano yao ambayo walikuwa wakituonesha tulipofika katika wizara zao, ilikuwa ni mashirikiano mazuri sana.

Mhe. Spika, lakini pongezi za pekee nimpongeze Mhe. Waziri, pale alifika pahali katika Baraza hili kuweza kusimamia taasisi zake hasa yanapoguswa masuala ya fedha. Mhe. Spika, wewe ni shahidi kipindi kilichopita bajeti ya mwaka jana tuliweka ahadi na Mhe. Waziri, badala ya kuona kuwa kuna miradi ambayo haitendeki kwa haki, lakini Mhe. Waziri, aliweza kuitekeleza ahadi ile na tukaweza kufuatana tukenda mpaka katika maeneo husika na watendaji wake na kwa kweli tunashukuru sana kupitia wizara yake kuweza kushuhulikiwa katika Soko lile la Tumbe Mhe. Spika, kama utakumbuka.

Mhe. Spika, lakini baada ya hayo, nataka nitoe mchango wangu mdogo katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri katika Idara hii ya Fedha za Nje ambapo katueleza Mhe. Waziri, kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita, Idara imeweza kufanikisha uanzishaji wa Mfuko wa Afya ambao lengo ni kuendeleza huduma za afya Wilayani. Nichukuwe fursa hii kuipongeza Serikali na kuipongeza Wizara hii ya Fedha kwa kuweza kuendeleza huduma hizi za afya hasa katika mawilaya.

Mhe. Spika, tunajua kama Rais alipokuja kuzindua Baraza hili alisema miongoni mwa mambo atakayoyapa kipa umbele ni kuendeleza hospitali za Wilaya na kuziweka katika kiwango kizuri. Kwa tunashukuru na tunapongeza hili. Lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri, kwamba katika Wilaya yetu ya Micheweni waiangalie sana ile hospitali ya Wilaya ya Micheweni na juhudi zinazochukuliwa, lakini tunaomba pale Serikali itakapopata fursa ya kupata pesa hizi au penginepo

basi waweze kuiangalia lile lengo lililokusudiwa pale kuwekwa kile chumba cha upasuaji basi ifikie lengo.

Naomba sana kupitia Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ione Wilaya ya Micheweni na wananchi wake waliopo katika Wilaya ile ili waweze kuwapelekea huduma zilizokuwa ni nzuri na waepukane na kufatilia huduma zile maeneo mbali mbali ya hospitali nyengine, naomba hilo Mhe. Waziri.

Hapa ulieleza kuwa changamoto kubwa inayoikabili Serikali ni kutokana na uhakika wa upatikanaji wa misaada kama inavyokusudiwa. Tunajua hilo sasa Mhe. Waziri, kasema kuwa ili tukubaliane na changamoto Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato pamoja na kudhibiti mianya ya uvujaji wa upatikanaji wa kodi. Nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe.Waziri na mimi niwaombe wafanye hivyo kwa sababu kuna hata taasisi zetu za Serikali bado zina udanganyifu katika ukusanyaji wao wa mapato lakini pia kuna wafanyabiashara ambao mpaka leo hii wanauza biashara zao bila ya kutoa risiti. Kwa hivyo, ni jambo zuri na Mhe. Waziri, basi aendelee kufanya hivyo yeye na watendaji wake ili kuona kuwa mapato hayavuji ya Serikali kwa kuona kwa yale tuliyokusudia basi tumeyafikia.

Suala la pili katika hii Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma Mhe. Waziri, kaeleza hapa kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara imesimamia upatikanaji wa mapato haya aliyoyaandika hapa, lakini haya pia ni katika uekezaji wa mali za Serikali tu. Basi tuone kwamba kuna umuhimu wa kuzitambua mali za Serikali kwa sababu nazo zinaendelea kuongeza mapato ya Serikali. Kama mali za Serikali zitakuwa hazitambulikani basi pia itakuwa ni kukosa mapato kwa Serikali. Kwa hivyo, kama hili wameliona tuiombe Idara hii ya Uhakiki wa Mitaji ya Umma iendelee na uhakiki wake, lakini izitambue mali zake ili iweze kuongeza hayo mapato na tuondokane pia ile kutegemea wafadhili wa nje na mambo yetu ikabidi *time* nyengine yalale kutokana na kuwa hatujapata kuingiziwa fedha hizo za misaada. Kwa hivyo, niombe sana Mhe. Waziri, kupitia Idara yako hii basi wafanye juhudi zao za makusudi katika kuzitambua basi hizo mali za Serikali.

Suala jengine Mhe. Spika, katika Idara hii ya Uhakiki Mali, Mhe. Waziri, alisema kuwa Idara pia imesimamia ujenzi wa Ofisi nne za Serikali zikiwemo; Ofisi ya Makamu wa Pili, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Katiba na Sheria na kuendeleza usimamizi wa jengo la Chuo cha Uandishi wa Habari Kilimani.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Waziri, kwa usimamizi wao huu wa Ofisi hizi ambazo zimejengwa katika kiwango kizuri na ni Ofisi za kisasa, lakini nikumbushie tu kuwa kuna Wizara nyengine bado zina changamoto ya majengo. Lakini humu ndani ya kitabu sijaona yanavyoelezwa hasa katika Idara ile ya Uwezeshaji, Wanawake na Watoto nao wana changamoto sana ya kukosa Ofisi.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, haya mmeshasimamia yamefika hapa yanapofika lakini tuombe na wizara nyengine muzione katika majenzi ya Ofisi, japokuwa ni mwendo mdogo mdogo lakini nia ikiwa nzuri basi tunaweza kufikia huko tunakokusudia na wao hawa tuwaone na tuachane na mambo ya kukodi maofisi kupoteza fedha nyingi za Serikali. Hii inagharimu fedha za kukodi maofisi ya Serikali kwa muda mrefu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, ninakuomba hilo nalo ulione.

Nije katika Mfuko wa Barabara katueleza Mhe. Waziri, katika ukurasa wake wa 29;

> "...hadi 2015 mfuko wa barabara umefanikiwa kutoa fedha na kufuatilia matengenezo mbali mbali ya barabara kwa kuitumia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano yakiwemo matengenezo ya kawaida ya barabara zote za lami kwa kuzifanyia usafi na kuziziba mashimo."

Mhe. Spika, nauomba Mfuko wa Barabara kwanza juu ya juhudi zao hizo wanazozifanya na huku kaeleza mpaka kuzifanyia barabara ambazo zinazoingizwa kifusi, tuwapongeze kwa hili kwa sababu njia nyingi tunazishuhudia kwa sasa hivi kuingizwa vifusi, lakini bado wanaoingiza vifusi au hiyo taasisi yenyewe kwa sababu kuna huu mfuko wa barabara, lakini kuna Idara nyengine za Serikali pia nazo zinasimamia katika utengenezaji wa njia hizi ndogo ndogo, hawazingatii mambo yoyote wanapokwenda kupeleka kuingiza kifusi kile, hawazingatii hata kidogo. Kwa hivyo, watambue kwamba wanapokwenda kupeleka kifusi basi watambue hasa tatizo la maji yanakotoka na kwendea.

Kwa sababu nataka nitoe mfano mmoja pale petu Tumbe tuliingiziwa kifusi kipindi hiki cha miezi miwili mitatu nyuma lakini kifusi kile Mhe. Waziri, kilipoingizwa hawakuzingatia maji wala hawakuzingatia njia za maji, imefikia pahali wananchi mvua zinashanyesha za Masika njia zile wanazichakura kupitisha mitaro ya maji ili isije ikatokea athari. Sasa wanapoanza kwenda kujenga barabara zile wasizidharau wakasema ni barabara za kifusi tu waangalie maji yanatokea wapi na yanaendelea wapi ili kuepukana wananchi baadae kuharibu tena yale mazingira. Kwa hivyo, niombe mfuko huu wa barabara au taasisi nyengine zinazohusika na kujenga barabara kama hizi za ndani wazingatie mazingira ya upitikaji wa maji.

Mhe. Waziri, barabara hii Mhe. Rais katuahidi katika ufunguzi wake wa soko kuwa barabara hii itaingizwa lami, naomba hilo mulitambue na mulijuwe yeye ni banaadamu anaweza akasahau, kwa hivyo, tunaanza kusema kuwa hii ni ahadi ya Mhe. Rais alipokwenda kwenye ufunguzi wa soko hili la Tumbe. Kwa hivyo, muzingatie sana hilo suala Mwenyezi Mungu atakapojaalia uwezo basi ile barabara

iweze kutengezwa kwa uzuri wakati mmekusudia kuimarisha lile soko lilioko kule Tume basi na ile barabara iweze kuimarishwa na pale palipokuwa pana vikwazo ambapo kuwa vimefanya *cross* sana za kushindikana kuvunjwa nyumba, hakuna nyumba nyingi ambazo zitavunjwa. Basi Serikali angalau basi waweze kuwalipa fidia wale wenyewe waliokuwa hawakukubali kuvunjia baraza zao ziendelee kulipwa japo kwa thamani ambayo itapigwa tathmini waweze kulipa na barabara ile iwekwe katika kiwango kizuri.

Suala jengine Mhe. Waziri, niingie kwenye mamlaka ya uwekezaji wa vitega uchumi Zanzibar. Kwenye kitabu chako hiki umeeleza kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mamlaka imeweka mkazo kuendeleza maeneo huru ya uchumi Fumba kwa kutayarisha mpango wa matumizi ya ardhi na kuanza ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kulifanya hili lakini niombe kwa sababu maeneo huru bado wanalia kilio cha kuona bado Micheweni yapo maeneo huru na sisi tunahitaji angalau kuweko na miundombinu mizuri ili waekezaji basi na wao wavutiwe kuja kule katika kijiji kile cha Micheweni kuekeza biashara zao.

Mhe. Spika, kupitia eneo hilo humu kwenye kitabu sijaona kwa sababu Mhe. Waziri, mwaka jana katika kitabu chake cha bajeti alitueleza kuwa kuna muekezaji huyu wa kiwanda cha sukari, juzi nililiuliza kwa Mhe. Waziri wa Biashara, basi sijui alinijibu au sikusikia vizuri, lakini sasa ninaliingiza kwako. Ulitwambia hapa kuna huyu muekezaji wa Kiwanda cha Sukari alitegemea kwenda katika eneo lile kule la Micheweni ili kwenda kuanzisha basi huo mradi.

Hebu Mhe.Waziri, utakapokuja tuambie umefikia hatua gani, kwa sababu roho zilitia tamaa tukaona kuwa itakapofikia hivyo basi wananchi wetu kwa kiasi fulani watafaidika kwa sababu mashamba wapandaji wa mua wapo kule, yaani maeneo ya Kwale kuna wapandaji wa miwa wengi na wengine wangehamasika kutafuta maeneo kwa ajili ya kuja kuona na wao itakapokuja kufika pahali muekezaji huyu akaja pale basi wakaweza kupata chochote nao.

Mhe. Spika, suala la mwisho niingie katika vipaumbele vya wizara. Vipaumbele vya Wizara kwanza Mhe. Waziri hapa kipa umbele cha pili kasema ni kuanza ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Wizara ya Fedha Pemba. Nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuanzisha hili jengo la Ofisi ya Wizara ya Fedha Pemba, lakini Mhe. Waziri, mimi nataka nilizungumzie lile jengo lililojengwa ambalo halikufikia kiwango na likaweza kuwa halifai kuendelezwa tena kwa ujenzi. Lile jengo lipo pale na si jengo dogo, sasa Mhe. Waziri, lile jengo nakuomba kama mnaona kuwa halifai tena lile jengo bora mulivunje muliangushe chini kuliko kuliacha kuendelea kukaa vile.

Kwa sababu ile ni hasara, pale wanapita chungunzima kila siku, maeneo ya uwanjani, watu tunakwenda kwenye mikutano na nini, watu wanapanda juu kule, lisije likatokea la kutokea halafu tukaja tukasema kwa kuwa ni mambo ya kupeana fidia. Naomba Mhe. Waziri, lile jengo kama halina tena uwezo wa kuendelezwa kujengwa na halina, basi msiendelee kuliwacha pale mkaweza kuweka adui yule, yule ni sawa sawa na adui. Hasa ardhi ile iliyopo pale kwa sababu ni ardhi ya chumvi chumvi pengine linaweza kuja kuporomoka mara moja, kwa hivyo, ninawaombeni lile jengo muweze kulifanyia ufumbuzi wa kuweza kulivunja.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mchango wangu ulikuwa si mkubwa, niendelee tena kumshukuru Mhe. Waziri, lakini na mimi niseme kuwa naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kufuatana na mtiririko wa michango ilivyo tunategemea itapofika kiasi saa 6.30 tuweze kufanya majumuisho. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe walioko nje wanapumzika pumzika huko waanze kujitayarisha kurudi ndani. Tunao wachangiaji watatu ambao wamebaki.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Fedha. Kabla yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataalla* aliyonijaalia kuwa katika uhai, uzima na afya inaniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kwa neema hiyo sote tuseme *Alhamdulillah*.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Waziri wa Fedha pamoja na Katibu wake na watendaji wake wote kwa shughuli nzuri waliyoifanya kutuwasilishia hapa aliisoma kwa ufasaha kabisa na tumemfahamu.

Mhe. Spika, mimi kwanza mchango wangu nitaenda katika Shirika hili la Bima. Shirika la Bima kama walivyoeleza ukurasa wa 26 kuhusu makusanyo wame-*overlap*, kwa hiyo, maelezo yaliyoelezwa hapa yote ni mazuri na ninawapongezeni sana na waendelee na makusanyo kama ilivyokusudiwa kwa maslahi ya nchi yetu.

Lakini Mhe. Spika, hapa nikizungumzia hawa Shirika la Bima hawana jengo na waliomba jengo pale karibuni miaka 3 na mpaka leo hawajafanikiwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atufahamishe wamefikia wapi wanakodi jengo kule na wanatumia pesa za nyingi za Serikali ambapo watapokuwa na jengo lao watafanya kazi kwa ufanisi kabisa kuliko hivi sasa wanavyokodi.

Mhe. Spika, lakini pamoja na hilo maslahi nayo ni matatizo kwao, kwa hivyo, tuangalie hawa na maslahi yao ili waweze kufanya kazi ya makusanyo kwa uzuri

kabisa. Mimi ninawapongeza sana katika makusanyo yao lakini na maslahi tuangalie ili kufikia hayo malengo.

Mhe. Spika, nikienda katika sehemu ya pili, nizungumze katika sehemu waliyozungumza wenzangu sana ile Fungu Mbaraka au kisiwa cha ndege. Kisiwa hiki kama wenzetu wa Tanzania Bara wanavyokigombania kukifanya kama ni cha kwao, kisiwa hiki kina maslahi mengi sana kama tutakitunza au tutakishughulikia na kubakia kuwa chetu, sio anayekwenda pale ni ndege tu, kuna mambo mengi bahari yake ina mazingira mazuri kweli kweli.

Mhe. Spika, ninakuhakikishia pale mahali pana samaki wa aina nyingi sana, kuna samaki wa kolekole, kuna samaki wa mbono, kuna samaki wa kibua wale wanaoitwa hunsa, sijui wengine wanawafahamu hao, samaki wa gongola wako wingi sana na wavuvi wetu pale wanafika kwa matatizo makubwa sana, wanakodi ma-BOTi yale yanayokwenda Mafia yale, lakini Mwenyezi Mungu tujaalie katika msimu wa shwari wanapokwenda pale basi wanavua samaki wa shilingi milioni ishirini mpaka milioni 30 kwa siku zao tatu tu. Wanagonga barafu katika maboksi wanaohifadhia wanakwenda siku mbili au tatu ukifika huo msimu na wanapata kipato kizuri, lakini sasa mapato hayaingii huku Zanzibar, mapato yanaingia kwa upande wa pili na wavuvi wanaovua ni Wazanzibari, lakini huondokea kule Dar es Salaam na kwenda Fungu Mbaraka, hilo lipo mimi mwenyewe nimeshuhudia wakati nipo pale *ferry* wanakwenda kule samaki wengi wanawavua, aina ya samaki tena wale wazuri niliokutajia, lakini sisi tumekaa tu, sio ndege tu pale.

Mhe. Spika, pale bahari yake ina mazingira mazuri ikiwa zitatuzwa na kuzifuatilia basi tukawawezesha hawa wavuvi wetu wakatoka Zanzibar na kwenda kuvua sehemu ile pale ambalo ni eneo lao la bahari, basi tutapata maslahi makubwa kuliko kuvua haya maji ya ndani, lakini maskini ya Mungu hawafiki kutokana na vyombo vyao ni vidogo na uwezo wao ni mdogo, ni jambo la kulizingatia na kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, nikienda na sehemu yangu ya tatu katika mfuko wa barabara, mfuko huu umezungumzia hapa ukurasa wa 29, kama ulivyoelezewa naomba kwa ruhusa yako ninukuu;

> "Mhe. Spika, Mfuko wa Barabara umeendelea na jukumu lake la kuweka utaratibu madhubuti wa kutunza fedha za matengenezo ya barabara, kutoa fedha hizo kwa ajili ya matengenezo ya barabara pamoja na kufuatilia na kukagua matumizi ya fedha hizo kwa dhamira ya kuwa na miundombinu endelevu. Aidha, mfuko una majukumu ya kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika kwa ufanisi na kwa lengo lililokusudiwa."

Mhe. Spika, maneno haya ni mazuri sana ambapo tukiyafanyia kazi kama inakusidia kwa malengo yaliyokusudiwa. Lakini ukiangalia mfuko huu wa Barabara umejikita sana huku Unguja, tukiangalia barabara za Unguja mimi nimetembelea sana kama kamati yetu barabara nyingi za Unguja zina lami tofauti na Pemba, na barabara za Kati zimetengenezwa vizuri sana tumeshuhudia.

Lakini ukiangalia mfuko huu hawaoni kule Pemba ilivyo, tuangalieni barabara iliyotoka Wete kwenda Chake Chake tuiangalie jinsi ilivyo au hawapiti wakaona? Ni matatizo makubwa sana barabara ile hata yale mashimo mpaka leo hayazibiki, hebu Waheshimiwa watendaji mnapotoka hapa mukaiangalie ile barabara mfanye angalau fungu la huruma, wale wananchi wanaopita njiani nao ni walipa kodi kama watu wengine, lakini ukiangalia hatuoni mantiki ya barabara ile, maisha utasikia haijapatikana mkandarasi, hata yale mashimo kutengeneza katika mfuko huu mnashindwa.

Mhe. Spika, ni tatizo, hebu waangalieni kwa fungu la huruma kabisa muiangalie ile barabara ilivyo, pahali penye barabara nzuri ndio pahali pakufika maendeleo, lakini watu barabara wanaikwepa kutokana na hali ilivyo. Kwa hiyo, tunawaomba watendaji waifikirie ile barabara na *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu awape uwezo mutekeleze kwani ile barabara ni mbovu kabisa.

Mhe. Spika, vile vile, kuna barabara zetu za ndani, zile barabara tunashukuru kama barabara ya Mzambarauni, Takao kupitia Gasi, Kijikani, Vumba mpaka Mchangamdogo imetiwa fusi vizuri. Lakini barabara isiyofanyiwa matengenezo ya fusi, si vibaya kama itaweza kupigwa kioo angalau nayo ikatiwa kiwango cha lami japo hapo baadae, kwa sababu zisije zikaharibika tena zile barabara. Ni barabara ambayo ina watu masaa 24 wanakwenda na kurudi kwa shughuli za maendeleo hasa ukifika msimu wa karafuu.

Kwa hivyo, ni jambo la kuliangalia zile barabara tulizozitia kifusi tuziangalie kwa jicho la huruma baadae tuzitie lami na *Inshaallah* tutafikia maendeleo. Pemba hakuna kilomita nyingi katika barabara yenye kilomita ndogo tu, mimi nashangaa hasa Zanzibar hii barabara zikawa za kifusi, barabara zote zinatakiwa ziwe za lami, hatuna kilomita nyingi barabara zetu, eti lakini masikini ya Mungu mpaka leo hali ndio hii. Karibu tunavyojitahidi lakini bado hatujafikia malengo, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atuwezeshe tufikie malengo.

Mhe. Spika, nikienda katika ukurasa wa 55 katika kitabu hiki cha hotuba ya Waziri wetu wa Fedha na hapa naomba ninukuu kama ilivyo, kuanzia 105 mpaka kuendelea;

> "Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nichukue fursa hii adhimu kuzungumzia umuhimu wa amani katika yetu. Amani na utulivu ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo endelevu ya nchi hii; kama tunavyotambua kwamba ghasia na migogoro katika nchi ni kikwazo kikubwa cha maendeleo."

Mhe. Spika, unaiona sentensi ilivyopangika vizuri hiyo, hii sentensi nzuri kweli kweli Mhe.Waziri, pamoja na wajumbe wote tuiangalie sentensi hii inavyosomeka, kwamba kama mahali hakuna amani basi hakuna shughuli za maendeleo, ila ni kikwazo kikubwa sana bali panapotokea ghasia na ikawa hapana amani. Huwezi kukusanya mapato kama nchi haina amani, utakusanyia wapi wakati pahali pana vurugu unakusanya mapato kutoka wapi?

Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi niiambie serikali amani haiji tu kwa maneno, amani inakuja kwa vitendo na hili tulijue sana.

Mhe. Spika, amani inakuja kwa vitendo, sio kwa maandishi tu kama tulivyoandika, maandishi nimesoma ni mazuri, lakini ukiangalia vitendo vinaashiria ubaya kabisa, si jambo zuri sana. Mhe. Spika, hivi sasa maana yake tukisema ndani ya Baraza la Wawakilishi hili tunaonekana kama sijui nani. Mtu mwenye haki yake hapati na aliyekuwa hana haki ndiye anayepewa.

Tumesema hapa kuna watu kuna watu kila siku wanaandikishwa katika vituo, hapa Chukwani kipo kituo hapa, lakini tukisema hapa tunaonekana kama ni upande wa Upinzani. Hakuna, sote ni Wawakilishi wa wananchi, jambo jema likitokezea tutalisifu na baya likitokea tutalisema, ndio wajibu watu, nasema hapo nitoe angalizo bado utaratibu huu unaendelea na tukisema tutaonekana kama Wapinzania. Hakuna Mpinzani humu ndani ya Baraza la Wawakilishi, sote ni wamoja na tuko pamoja kwa kufanya kazi sasa hapo ndipo amani tunapoichezea.

Mhe. Spika, kuna watu ikifika kipindi hapa wanavaa ninja, yaani askari unavaa ninja unajificha nini, wewe askari unavaa ninja wewe si jambazi. Ni jambazi kabisa, unakwenda kwa wananchi kusimamia unavaa ninja, unakusudia nini na una vyombo vya moto wewe, hili si jambo zuri hata kidogo kama tunahubiri amani hapo ndio pakuzingatia kabisa, bihayri ya hivyo tutatwanga maji katika kinu.

Maji ukitwanga katika kinu hayakai yanaruka yote, kwa hivyo, hili jambo tusionekane kama tunasema tu kwa utashi, hatusemi kwa utashi, ni jambo la kulifanyia kazi na tukajenga mazingira mazuri kufikia hiyo amani tunayoitaka, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atuelekeze huko.

Mhe. Spika, kwa nini museme kwa maneno matupu isiwe kwa vitendo, hili jambo lifuatilieni, wajibu wake serikali inapozungumza kitu hapa ifuatilie na ione na kama lipo ikataze na kama halipo basi watwambie, lakini kama lipo lifanyiwe kazi, si vizuri.

Mhe. Spika, mimi sina mengi ya kuzungumza lakini ujumbe umefika na nalielezea na nalitoa mtakuja kunikumbuka kama nimo ndani ya Baraza au simo ndani ya Baraza, lakini hili jambo lipo.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa mchango wangu mdogo *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atufikishe salama, naunga mkono mia juu ya mia hotuba yako hii Mhe. Waziri na wewe usimamie vizuri maendeleo ya wananchi, wewe ndiye kigezo kikubwa. Ahsnteni sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Spika, ahsante sana kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha siku hii ya leo kuendelea kuwa pamoja hapa na kuendelea na mambo ambayo ilikuwa tumejipangia katika shughuli zetu. Lakini pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti ya Wizara hii yetu ya Fedha, wizara muhimu na wizara ambayo ina mikondo na mambo yote katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pia kwa aina ya kipekee niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kunichagua na kuniwezesha kuingia humu ndani na kuja kushirikiana nanyi kwa pamoja na wenzangu wote kufanya kazi ambayo tulikuwa tunaendelea kuifanya, lakini ikiwa pamoja na utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ndani ya jimbo na nchi yetu kwa ujumla. Vile vile, niwashukuru kwa namna ambavyo tulikuwa tunashirikiana kwa kipindi chote cha miaka mitano hadi leo tumefikia hapa ikiwa tunafikia bajeti hii ya mwisho katika Wizara yetu ya Fedha, na niwaombe basi wakubaliane na haya ambayo mimi nataka kuyazungumza na *Inshaallah* sote tuna nia njema ya kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, nikimaliza hapo sasa niseme tu *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia amani ya nchi yetu itaendelea kuwepo na kusimama na *Inshaallah* tutaishi katika misingi ya amani hadi kufa kwetu katika dunia hii ambayo Mwenyezi Mungu ametuleta ili kuja kupita njia. Baada ya hayo sasa Mhe. Spika, itakuwa mwizi wa fadhila kama sikuwashukuru watendaji katika wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya ndani ya wizara hii, wakiongozwa na kaka yangu ndugu Khamis Mussa Omar ambaye ni Katibu Mkuu katika wizara hii. Baada ya shukurani hizo sasa Mhe. Spika, niende katika kazi ambayo nimesimama hapa sasa kuifanya.

Jambo la kwanza ambalo Mhe. Spika, nitamuomba Mhe. Waziri anisaidie kama ambavyo nilikuja kuchangia juzi wakati tulipokuwa tunapitisha Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Pale niliomba kufahamu juu ya ile hoja ambayo msingi wake ilitolewa na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika suala zima la kutumia *database* moja baina ya mawaziri hawa wawili na nchi zetu kwa ujumla. Ningelimuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie, je, matumizi yale ya *database* hii yatakuwa yana faida gani kwa upande wa Zanzibar na hasara zake ni nini.

Mhe. Spika, kwa sababu suala hili linagusa moja kwa moja katika uchumi mzima wa nchi yetu hii ya Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, utakapokuja hapa nitaomba suala hili ulieleze kwa kina ili niridhike basi, kwa sababu sina kawaida ya kuzuia wizara hii na nisije nikafanya hivyo, naomba unijibu kwa ufasaha na kwa mantiki ambayo Wazanzibari wote na Watanzania watalielewa suala hili ili Zanzibar iendelee kuishi na amani yake.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakuja katika maeneo huru, wenzangu walikuwa wamelizungumzia sana suala hili, lakini ningelipenda tu Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atusaidie suala zima la wizara yake imejipange vipi katika kuhakikisha kwamba haya maeneo huru ambayo tunayo sasa katika kipindi chetu hiki cha miaka mitano. Sasa hivi tunazungumzia programu, utaratibu na mikakati yake, kwa sasa wizara imejipangaje maeneo haya kuyaboresha ili hawa wawekezaji ambao wanakuja nchini kwetu waweze kuyatumia maeneo haya na waweze kuwasaidia wao, lakini hasa yafikie malengo yakuwasaidia Wazanzibari ambao sote kwa umoja wetu tunajenga nchi yetu.

Mhe. Spika, pia katika hili ningelimuomba Mhe. Waziri, tuna matatizo katika suala zima la wawekezaji na vile vyombo vinavyoshughulikia wawekezaji katika nchi yetu. Hebu Mhe. Waziri, utakapokuja hapa tuelekeze hasa nini mpango wa serikali katika kuifanyia *reform* ile *One Stop Centre* ili wawekezaji wetu na wananchi wetu hawa waweze kuneemeka katika kutumia chombo hiki kwa manufaa ya kukuza uchumi wetu ndani ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo wenzangu walizungumzia sana suala la matumizi ya bahari katika kueneza uchumi na kuendeleza uchumi wa nchi yetu. Mhe. Waziri, utakapokuja hapa nitamuomba basi atusaidie kutuelekeza na kuifahamisha Zanzibar ni hatua gani serikali imefikia katika suala zima la ile taasisi ya uvuvi ambayo kuna mpango wa kujengwa hapa Zanzibar na hatimae watu wetu waweze kuneemeka na kuitumia vizuru bahari ambayo tunayo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa nakuja katika kifungu cha 12 cha hotuba ya Mhe. Waziri ambayo ameisoma hapa, naomba kunukuu;

> "Mhe. Spika, jukumu la kusimamia uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma (ikiwemo ufuatiliaji wa mapato ya ndani na nje, kusimamia matumizi pamoja na kutoa huduma za kiuhasibu serikalini) liko chini ya Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali pamoja na Idara ya Fedha za Nje".

Mhe. Spika, katika michango yangu niliyotoa katika miaka ya nyuma iliyopita nilitaka kuelewa ni utaratibu gani unaotumika wa kuweza kupata taarifa juu ya utafiti unaofanywa wa matumizi ya hesabu za ndani. Ningeliomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie basi kwa sababu tumezoea kupata taarifa ya hizi kazi ambazo zinafanywa na *Auditor General* peke yake, lakini ukaguzi wa hesabu za ndani hizi naomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atusaidie kutufahamisha vile vile utaratibu wake unakuwa vipi.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika eneo la upandishaji wa mapato katika kifungu cha 14. Hapa nimeona katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi na wizara hii mapato ya ndani ya serikali yameongezeka kwa shilingi 156,934,000 kutoka 171,690,000 zilizokusanywa kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Hapa ningeliomba kupata ufafanuzi zaidi kwa sababu haya mahesabu naona mimi yananizonga hapa, sasa sijui kama hivi ndivyo ilivyokusudiwa au mahesabu tu yamekosewa. Naomba Mhe. Waziri, utakapokuja unisaidie.

Mhe. Spika, tukiondoka hapo tunakwenda katika kifungu cha 24 cha kitabu chetu ambacho Mhe. Waziri, amekuja nacho hapa. Hapa kuna maelezo kwamba jukumu la kusimamia mali, mitaji ya serikali pamoja na kusimamia upatikanaji na uondoshwaji wa mali linasimamiwa na Idara ya Uhakiki Mali na Mitaji ya Umma.

Mhe. Spika, pamoja na maelekezo haya ningelimuomba sasa Mhe. Waziri, atakapokuja hapa naunganisha kifungu hiki cha usimamizi wa mali za umma pamoja na mapato yale ya serikali katika suala zima la mapato yetu yale yanayotokana na mashirika ya simu. Nilichangia katika Wizara ya Mawasiliano, na nikachangia vile vile katika bajeti kuu ya serikali, lakini hapa sasa ndio kwenye wizara ambayo ni *mas-uul* katika masuala ya fedha. Kwa hiyo, ningelimuomba Mhe. Waziri, anisaidie taarifa na msimamo wa serikali juu ya suala zima la haya mapato yetu yatokanayo na sekta za Muungano kama ambavyo niliweza kuanisha katika wizara zilizopita.

Mhe. Spika, vile vile, ningependa kufahamu pamoja na kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, lakini sina taarifa muhimu au taarifa za uhakika kuhusiana na suala zima la kuendeleaji wa Kampuni ya *ZANTEL* kufanya kazi Zanzibar. Kwa hiyo, ningeliomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa

anithibitishie hilo je, Kampuni ya *ZANTEL* kweli imeuzwa au inaendelea na shughuli zake Zanzibar. Na kama imeuzwa, zile haki ambazo zipo katika maeneo yetu kuna utaratibu gani ambao umepangwa na serikali juu ya kuendelea kuyasimamia maeneo hayo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika kifungu cha 36 kinazungumzia kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Ofisi Kuu Pemba iliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,146.12 milioni kwa kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Mei 2015 ofisi hii imetumia jumla ya shilingi 897.57 milioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya mwaka wa matumizi wa fedha ya kawaida.

Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa maelezo haya tunayoelezana katika kitabu hiki yanakwenda sambamba na uhalisia halisi wa thamani ya fedha ambayo imetumika katika eneo hili. Namuomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie kwa sababu zamani Mhe. Spika, miaka miwili na nusu iliyopita nyuma mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo katika Baraza lako hili tukufu. Yako mambo ambayo tulikuwa tumeyafatilia na hatimae wajumbe waliokuweko sasa wakiongozwa na Alhaj Hija Hassan Hija baada ya kifo cha swahibu wetu Mhe. Marehemu Salmin Awadh Salmin, bado kuna mambo ambayo tunaelezana tunakuta kuwa bado yana utata katika maeneo tofauti. Kwa hiyo, ningeliomba ile thamani ambayo ilikuwa imezungumzwa hapa, je, inalingana na uhalisia wa utekelezaji wake. Namuomba Mhe. Waziri, akija hapa anisaidie.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika ukurasa wa 45 wa kitabu hiki ambapo hapa kuna suala zima linalozungumzia Benki Kuu.

Mhe. Spika, namuomba pia Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie lile suala ambalo nimeliuliza miaka minne nyuma na leo narejea tena. Ni jinsi gani na namna gani *BOT* iwe Zanzibar au iwe Tanzania inasaidia katika kukuza kuendeleza na kusaidia uchumi wa Zanzibar. Namuomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie katika hilo.

Jengine nikiondoka hapa kuna sifa nyingi ambazo zimepewa Shirika la Bila la Zanzibar hususan kwa namna ambavyo limeweza kujitawaja na hatimaye kuweza kufanya mambo mazuri mazuri ambayo sote tunafurahika nayo. Naendelea kuwaomba kwamba wawe waangalifu kwa wale watu ambao wanakwenda kuzidai bima zao, wafatilie kwa kina na hatimaye wanapolipa yale malipo yanayohusiana na bima, yawe ni malipo ambayo hayawezi kuleta matatizo baadae. Kwa sababu zile bado ni fedha za wananchi wavuja jasho katika nchi yetu ya Zanzibar. Vile vile, nimeingia wivu kuona maendeleo ya bima yanakwenda vizuri, lakini pamoja na sifa nyingi ambazo zimetolewa kwa upande wa Benki ya *PBZ*. Ningeliomba

sasa na wao *PBZ* waige mfano wa bima na wahakikishe kwamba wanatawanya huduma zao na zinafika mikoa mingi zaidi, ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari ambao wako nje ya mikoa yetu ya karibu wanafaidika na kuona kwamba wanapata huduma hii muhimu katika mamlaka yetu ya Zanzibar.

Mwisho kabisa nikielekea katika kifungu cha 58, nigelipenda vile vile kuhakiki na kupata uthibitisho ule Mfuko wa Barabara ambao unakuwa unasimamiwa na Wizara ya Fedha lakini matumizi yake yanafanyika katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliao kupitia Idara ya Barabara, nani mhakiki wake kwa yale mambo ambayo yameasisiwa kutendeka na hatimaye ikawa hatuoni utekelezaji wake kwa ufanisi uliolengwa. Namuomba sana Mhe. Waziri, atakapokuja hapa atusaidie katika hilo ili tuweze kupata mustakabali mzuri wa haya mambo tunayoyazungumza.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa nawapongeza sana *TRA* kwa kazi nzuri pamoja na *ZRB* waliyoifanya katika kuhakikisha kwamba mapato yetu yanakua na yanakuwa endelevu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, Serikali ya Awamu ya Saba katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tulipoingia madarakani serikali hii ilikuwa inakusanya pato la shilingi bilioni zisizopungua 13, lakini sasa hivi tunaelekea shilingi bilioni zisizopungua zaidi ya 32 na kuendelea. Hii nipongeze sana kwa serikali na malengo yetu ilikuwa tukusanye shilingi 50 bilioni. Lakini bado Mhe. Waziri, ana kazi ya ziada tutakaporejea humu kwenye Baraza, kwa mwaka wa fedha mwengine unaofuata na *Inshaallah* sote tuliomo humu tutarejea tupige *target* yetu na tupindukie shilingi 50 bilioni ili tujitosheleze na mambo tuliyojipangia. Vile vile, mafuta yapatikane, yachimbwe na tuongeze mapato yetu na utalii ukue zaidi tufanikiwe na kiwango chetu tulichokiweka.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja, lakini hapo hapo namtaka Mhe. Waziri, anipe ufafanuzi unaokidhi ili tuepukane na masuala ya mabuti katika wizara hii. Ahsante sana.

**Mhe. Abdi Mosi Kombo:** *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutufikisha hapa leo na tukaweza kuchangia. Kabla ya kuchangia mchango wangu kwanza naipongeza serikali kwa kuishughulikia barabara kongwe kule Kijini, Matemwe; kwamba hivi sasa barabara ile inajengwa na kututia tamaa ili wananchi wa kule kuondokana na tatizo la barabara hiyo.

Mhe. Spika, katika mchango wangu wa leo nitaanzia katika Mfuko wa Barabara. Lakini kabla ya kuchangia naiomba serikali au napendekeza uweko Mfumo wa

Baharini, kwa sababu na baharini nako kunakuwa na matatizo makubwa kama barabarani.

Sasa nikienda katika ukurasa wa 29, kifungu 58, Mfuko wa Barabara ni Mfuko ambao unatengeneza barabara zetu aidha zilizoharibika au zinazoundwa undwa. Nikisema zinazoundwa nakusudia zile barabara za *Feeder Road* kama sehemu za vijijini.

Mhe. Spika, katika barabara ambayo hivi sasa ni mbovu na inataka ukarabati ni barabara yetu kutoka Mjini kwenda Kaskazini. Barabara hiyo hivi sasa ni mbovu na imechafuka vibaya na ina madaraja mabovu.

Juzi katika daraja moja la Kitope panaitwa Kazole limeingia gari moja la mchanga na limevuruga kila kitu. Kwa hivyo, kama Mfuko wa Barabara unahifadhi basi kwanza uhifadhi madaraja yaliyoko katika njia ya Kaskazini. Njia ile hivi sasa ina hatari kupita hata gari hivi sasa kwa ubovu uliokithiri wa madaraja.

Mhe. Spika, katika Mfuko wetu wa Barabara sisi Wawakilishi aghalabu huwa tunapewa Mfuko wa Jimbo na huwa tunajengea zile barabara ndogo. Mimi kwenye jimbo langu la Matemwe ninazo barabara ambazo tumezianzisha katika Mfuko wetu wa Jimbo lakini hazikuwahi kumalizika sawa sawa kwa kutia kifusi. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Fedha kwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano barabara zile ambazo tulizianzisha naomba msaada wa kwenda kuzisafisha ili zitengenezwe vizuri kwa kujazwa kifusi tena. Barabara zenyewe nilizitaja wakati nachangia katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambazo ni mbili; barabara ya Kachongwa na Mifuuni. Hizi ndizo barabara ambazo tuliziunda katika Mfuko wetu wa Jimbo, lakini *UUB* haikuwahi kumaliza barabara hizi. Kwa hivyo, Wizara ya Fedha iwahakikishie Wizara ya Miundombonu kupitia *UUB* waje wanimalizie barabara zile.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 47, kifungu cha 90, Mamlaka ya Uwezeshaji na Vitega Uchumi. Katika dunia mara nyingi vitega uchumi vinakuwa katika rasilimali iliyokuwa katika nchi yake. Nchi yetu ya Zanzibar ni nchi ambayo imezungukwa na bahari pande zote na tuna samaki wengi ambapo samaki hao kama tutakuwa na utaalamu wa kuweza kuwavua samaki hao basi nchi yetu inaweza ikajenga viwanda vya kusindikia samaki na wananchi wetu wakapata ajira.

Katika mwaka 1964 serikali ya mwanzo ya Marehemu Abeid Amani Karume ilijenga viwanda hapa Zanzibar; Kiwanda kimoja kikubwa ikawa ni Kiwanda cha Sukari. Kiwanda hiki kilikuwa kinachukua watu wengi sana, kiwanda chengine cha viatu, sigareti, viwanda vidogo vidogo vya mipira, viwanda vya masufuria

vilikuwepo, viwanda vya *sheet metal* vilikuwepo na viwanda vya nguo. Lakini viwanda vile vyote havipo na vimekufa na viwanda vile vilikuwa vinachukua wananchi wengi sana ili kuondoa tatizo la ajira katika nchi yetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, viwanda vile je, serikali itakuwa na mpango gani wa kuvileta viwanda kama vile ambavyo vililetwa katika serikali yetu ya Awamu ya Kwanza na vikafa ili wananchi wetu wapate kuondokana na tatizo la ajira?

Mhe. Spika, kuna wajumbe hapa walizungumzia habari ya Kiwanda cha Sukari. Kiwanda hiki wamekisifu sana, lakini mimi ningeliomba Mhe. Waziri, aje atuhakikishie kiwanda hiki cha sukari hivi sasa kina uwezo wa kutoa tani ngapi za sukari na vile vile sukari hii inauzwa katika nchi gani na gani, au tunauziwa sisi tu hapa wananchi? Kama tunauziwa sisi wananchi katika Serikali yetu ya Zanzibar tujue ili tuhakikishe kwamba kiwanda chetu cha sukari kinatoa sukari tunaipata.

Mhe. Spika, kwa vile wajumbe wengi wameshazungumzia katika hotuba hii na mimi nakushukuru naunga mkono hotuba hii, lakini naiomba tena serikali ituwekee viwanda ili wananchi wetu wapate ajira katika viwanda hivyo. Mhe. Spika, nakushukuru naunga mkono hoja.

**Mhe. Spika:** Nakushukuru Mhe. Abdi Mosi, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji tumemaliza, nichukue nafasi hii basi nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha. Wakati huo huo tunaanza majumuisho, kwa hiyo, wajumbe walioko nje warudi ndani ili tuweze kuimaliza kazi hii.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa heshima kubwa naomba kwanza kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao. Michango yao ilikuwa ina maswali, ilikuwa ina ushauri, nataka niwaambie tu kwamba nipo hapa pamoja na watendaji wangu tumeipokea na kwa yale ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi katika kipindi kifupi basi tutayafanyia kazi na kwa yale ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa kipindi kirefu kidogo basi tumepokea na tutaanza kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kuwatambua wale wote ambao wamechangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2015/2016, nikianza na Mhe. Hija Hassan Hija ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo; akifuatiwa na Mhe. Mohammed Raza Hassanali, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Farida Amour, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa na wa mwisho ni Mhe. Abdi Mosi Kombo.

Mhe. Spika, ninaamini wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia bajeti hii ni kwa sababu tu michango ya wezao imekidhi hoja zao. Sasa basi, naomba nianze kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo zimewasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Kwanza ni hoja ambayo imewasilishwa na Mhe. Hija Hassan Hija na hii nimetaka niiweke iwe ya kwanza kwa sababu ni hoja pekee. Nilikuwa nina hamu kubwa na shauku ya kutaka kusikia basi na Wawakilishi wengine wanaiibua hoja hii, lakini Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ameiibua ni imani yangu kwamba ni hoja ya kamati nzima.

Mhe. Spika, tumekuwa na desturi ya kuzungumzia mapato, mapato, lakini leo kupitia bajeti yangu hii Mhe. Hija Hassan, Mwenyekiti wa Kamati ameishauri basi wizara yangu kuwa makini katika matumizi kupitia utaratibu mpya wa programu, ametushauri tuwe makini katika matumizi. Na mimi nataka nilihakikishie Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba ushauri huo tumeupokea na kwa kupitia kwa mawaziri wenzangu wa wizara mbali mbali pamoja na Makatibu Wakuu tutasimamia umakini huo katika matumizi kupitia programu kama tulivyopitisha bajeti zetu.

Mhe. Spika, lakini la pili ambalo limezungumziwa pia na Mhe. Hija Hassan na likatiliwa mkazo na Mhe. Bikame Yussuf, ni suala zima la kuendeleza ujenzi wa majengo ya serikali. Hili tumelipokea, tutaendeleza ujenzi wa majengo ya serikali na hasa Mhe. Bikame Yussuf, pale alipotilia mkazo na kusema kwamba ujenzi wa majengo mengine ya serikali au taasisi nyengine za serikali kama vile Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto.

Nataka nimhakikishie tu Mhe. Bikame na Waheshimiwa wengine, kwamba Wizara ya Wanawake na Watoto jengo lao la Unguja katika bajeti hii tutaliongezea ghorofa moja na vile vile katika jengo tunalolijenga Wizara ya Fedha kule Pemba litakuwa lina *wing* tatu; *wing* moja itatumiwa na Wizara ya Fedha, *wing* moja itatumiwa na Wizara ya Uwezeshaji na *wing* ya tatu itatumiwa na Wizara ya Ajira. Kwa hivyo, hilo usiwe na wasiwasi tutalifanyia kazi na tutalisimamia.

Vile vile, Mhe. Hija Hassan, alitatutaka tusimamie ujenzi huu basi usije ukawa kama ule uliopita wa jengo lile la Wizara ya Fedha. Nataka nikuhakikishieni Waheshimiwa tutakuwa karibu zaidi na masuala hayo ili athari ile iliyotokea isije ikatokea tena.

Mhe. Spika, suala jengine limezungumzwa na Wahehsimiwe wengi kidogo Mhe. Hija Hassan, Mhe. Mohamed Raza, Mhe. Fatma Mbarouk, Mhe. Marina Joel, Mhe. Bikame Yussuf, suala la ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine na hasa

baada ya kuonekana kazi nzuri iliyojitokeza pale *airport* kwa upande wa *visa*. Nataka niwahakikishie kwamba suala hilo tutatilia maanani na tunaangalia. Hivi sasa kuna maeneo mengi tumeshayakusanya na yamo katika mchakato wa kuwekewa mashine, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakapotujaalia na maeneo hayo vile vile tutayawekea mashine ili tusiwe na ule utaratibu wa kutumia pesa moja kwa moja (*cash money*), hilo tutalifanyia kazi.

Mhe. Spika, suala ambalo limejikita kwa Waheshimiwa wengi akiwemo vile vile Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Farida Amour, Mhe. Fatma Mbarouk, Mhe. Hamza Hassan na wengine, ni suala la *GBS*. Hapa kulikuwa kuna mambo mawili; La kwanza Mwenyekiti alitutaka tuelezee wakati walipotembelea kule *BOT* waliambiwa kwamba kuna shilingi 24 bilioni zimetolewa zimepelekwa Zanzibar. Lakini wakati tunasoma hotuba yetu ya bajeti ya Taifa tulimwambia sisi tumepata kama shilingi 17 bilioni. Nataka niseme tu, kwamba hapa kidogo zilichelewa, mwezi uliopita wa Mei tumepokea tena *GBS* ya shilingi bilioni 7.4, ukizijumlisha sasa inakuja shilingi 24.5 bilioni. Hizo ndizo ambazo tumeshazipokea kati ya shilingi 40 bilioni ambazo tulipata ahadi. Kwa hivyo nataka niliweke sawa tu kwamba sasa hivi tupo sawa baina ya takwimu zetu sisi na takwimu za *BOT*.

Wengine walisema kwamba tuondokane na kutegemea wahisani sana. Ndiyo lengo letu na ndiyo maana tumekuja na kuunda Mfuko wa Miundombinu. Ule mfuko tumeanza sasa hivi utatoa bilioni ishirini na tano (bilioni 25)mwaka huu mambo yatakapokuwa mazuri lakini baadae mfuko ule utakua. Kuna mapendekezo mengine hapa yamejitokeza katika kuuongezea huu mfuko, tutayaangalia na yale. Huu mfuko utakuwa, baadae tutaondokana na kutegemea misaada, na hatimaye tutajitegemea wenyewe. Lengo letu kama ni Serikali tufike pahali tujitegemee wenyewe.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lililozungumziwa na limezungumziwa na Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Hassan, suala zima la kutanua basi wigo wa vyanzo vya mapato na wakatoa mfano katika Kisiwa cha Fungu Mbaraka. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ni kweli kisiwa kile ni kizuri sana. Kisiwa kile wataalamu wanasema wale ndege wanaokwenda pale wakajisaidia, ile mali ghafi kama itaweza kuchimbwa basi ina thamani kubwa zaidi, ni mbolea ile.

Watalii wanakwenda kule kuna ndege wa kila aina ambao wanaokwenda, kuna samaki Mhe. Hassan amesema hapa ni mvuvi pekee tuliyenaye kwamba samaki wa kila aina wapo katika eneo lile.

Ni vyema sasa tukaliangalia kwa ukaribu zaidi na mimi ninathubutu kusema ndugu zanguni nitakaa na Mhe. Waziri anayeshughulikia na Utalii, tuone tunafanya nini katika eneo lile kwenye kipindi kijacho ili liweze kuongeza mapato katika Serikali yetu. Hilo tumelichukua na nitakaa na wenzangu wa sekta ili tuweze kulifanyia kazi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumziwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Waheshimiwa wengine wamekuwa wakilizungumzia kwa kipindi kirefu sana, suala la uanzishwaji wa benki ya akinamama, Benki ya Wanawake kule Tanzania Bara.

Nataka niseme tu kwamba imeanzishwa siyo pesa zote zimetoka Serikalini, imeanzishwa na wadau, kwa maana ya *share holders.* Hata mimi nina vijipesa kidogo nimeweka kwenye benki ile. Hii benki nayo tunaitazama kwa mtazamo huo huo. Tumekaa vikao vyetu vitatu; Wizara inayohusika, Wizara ya Fedha, *BOT*, na *PBZ* tumewaalika lakini tunaona cha msingi kwanza hebu tuanzishe angalau na dirisha, tuone hasa mahitaji ya wanawake ni nini. Kama mahitaji ya wanawake kwenye benki hii ni kupunguziwa riba, benki hii itakufa.

Kama mahitaji ya wanawake kuwa ni *fast track*, kuhudumiwa mara moja kwenye *service* zao, pale inawezekana, hebu tuanzieni na dirisha. Tunataka tuangalie utaratibu wa kuanzisha dirisha, na tayari sasa hivi tunaanzia na dirisha la Benki ya Kiislamu, watakuwa na huduma kwa ajili ya wanawake pale ili tuweze kuona maendeleo ya hii huduma za wanawake itakavyokuwa, na baadae tutakuja kuona hasa jinsi gani tutakavyoweza kushajihishana katika kununua *shares* kwenye kuanzisha benki hii. Lakini tusidhanie kwamba benki hii iwe na riba ndogo kwa ajili ya wanawake ili iweze ku-*survive,* haito-*survive* kabisa, itakufa. Lazima ishindane na benki nyengine zilizopo ili iweze kuhimili vishindo, lazima iwe na mtaji mzuri. Hivyo ndivyo tunavyotaka kuiangalia benki hii. (*Makofi*).

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa sana na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Hamza Hassan Juma na wengineo ni kuhusu suala la kushuka kwa thamani ya shilingi kwa dola na kupanda kwa bei za vyakula. Hili nililieleza wakati ninafanya majumuisho ya bajeti ya Taifa, lakini nataka nikumbushe tu kwamba kuna sababu tatu kubwa za msingi zilizopelekea kushuka kwa thamani ya shilingi *against dollar*.

1. Uchumi wa Marekani umekua kiasi ambacho fedha zote thamani yake zimeshuka; *against dollar* ndani ya dunia. Hata ukitazama *Euro*, *Pound, Franc*; zote, mpaka na shilingi yetu imeshuka thamani yake.

2. Ukitazama takwimu ya mauzo ya bidhaa tunazouza nje ambazo zinatupatia dola, kwa mfano kama dhahabu, bidhaa zetu za kilimo tunazosafirisha kwenda nje thamani yake imeshuka. Kwa hivyo uingiaji wa dola ndani umepungua.

3. Fedha ambazo wahisani wameahidi kutusaidia nazo vile vile zimepungua. Hayo yamesababisha mahitaji ya dola kuwa makubwa zaidi katika kipindi hichi.

Lakini ninataka niseme ndugu zanguni ukiacha vyakula vinaagizwa kutoka nje ya nchi, hili halina uhusiano na muhogo, halina uhusiano na viazi, kilichopo hapa watu wafanyabiashara wame-*take advantage*, huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhani tunahitajia bidhaa hizi wame-*take advantage*, lakini kwa kweli hazina uhusiano. Huo mchele, sukari, unga tumetoa *exemption*, tumewafanyia unafuu mkubwa sana wa kuwasamehe kodi wafanyabiashara ili na wao waweze kutoa unafaa kwa bei.

Sasa hili mimi ninasema tu kwamba nimuombe sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tushirikiane katika kufuatilia ili tuweze kuona kwamba ni kiasi gani wenzetu hawa tumewapatia misamaha na wao wameweza kuwasaidia wananchi katika hizo bei.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumziwa ni suala la uongozi wa Kiwanda cha Sukari kudhalilisha wananchi. Suala hili limezungumzwa na Mhe. Mshimba na ikaongozewa kwamba yapo baadhi ya mahoteli vile vile kuwa wanawadhalilisha Wazanzibari.

Nataka niseme tu kwamba nitalifuatilia. Hapa nina wenzangu; Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, Waziri wa Kazi na Utumishi wa Umma, tutakaa na kulitafakari hili na tutalifuatilia ili kuweza kuwaelimisha hawa wawekezaji kwamba Mzanzibari ana haki yake kama mwananchi yeyote duniani, ana haki ya Kikatiba, ana haki ya Kisheria, ana haki ya nchi yake, hapaswi kudhalilishwa ili na upande wa pili nao tuusikilize, *the right to listen both sides*.

Tusikilize na wale ni eneo gani basi wanalowadhalilisha Wazanzibari ili tuweze kufahamiana. Nadhani kwamba tukifikia pahala tukafahamiana, haya matatizo madogo madogo yataondoka.

Mhe. Spika, liliulizwa suala jengine hapa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Abdi Mosi Kombo ukarabati wa Kiwanda cha Sukari na nikaulizwa kiwanda hichi kinazalisha tani ngapi.

Nataka niseme tu kwamba kile kiwanda kinafanyiwa ukarabati mkubwa sana. Hivi sasa kuna mashine ambazo zimeshaagizwa, ukarabati utakuwa na thamani usiopungua dola milioni kumi na mbili. Sisi tunajua kuwa mashine zote ambazo wanazozifungua wanaziweka katika maeneo, na Kamishna wa Uhakiki wa Mali anakwenda kuziangalia zipo na kama za kuuzwa zitauzwa, wanafanya huo ukarabati na wanategemea kukamilisha ukarabati wao katika kipindi kifupi kijacho.

Nimeeleza kwenye hotuba yangu, wameanza na kutoa sukari kwa misingi ya majabirio, wamezalisha kama tani mia mbili kwa misingi ya majaribio na wameitoa ndani wameiuza sehemu na sehemu wametoa kuwasaidia wananchi. Lakini nimesema katika hotuba yangu vile vile matengenezo ya kiwanda hichi yatakapokuwa yapo tayari, kiwanda kitazalisha tani zisizopungua thamanini kwa siku.

Kwa hivyo tutakuwa hatuhitaji sisi sukari na hii ya ziada watakayoipata wataiuza. *Europe* sasa hivi wanahitajia sukari nyingi sana, watakuwa na soko kubwa Afrika Mashariki. Tanzania Bara wanahitajia sukari nyingi sana. Kwa hivyo hayo ni mafanikio makubwa sana tutayopata katika kiwanda hichi. (*Makofi*).

Kiwanda hichi hivi sasa kinaajiri watu wasiopungua elfu moja na mia mbili, ndani ya kiwanda pamoja na mashamba. Kwa hivyo hilo ndiyo lengo letu, na tunawasimamia kwa karibu zaidi; Wizara yangu pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kuna suala jengine limeulizwa suala zima la *ZSSF* itafute miradi ambayo itakayotoa faida kubwa. Mhe. Mshimba na Mhe. Hamza. (*Makofi*).

Nataka niseme lengo la *ZSSF* ndiyo hilo. *ZSSF* ni fedha za wanachama. Hivi sasa wapo katika mpango wa kujenga nyumba za bei nafuu, hivi sasa wapo katika mpango na michoro tayari ya kujenga maduka pale Michenzani. Hii itawasaidia kuweza kupata faida nzuri zaidi. Nyumba zitatolewa kwa wanachama na waliokuwa siyo wanachama. Lengo letu tunawaangalia ndugu zetu wa *DIASPORA*.

Ndugu zetu wa *DIASPORA* wazawa waliopo nje badala ya kuleta pesa zao wakajengewa taratibu, wanaweza kuikuta nyumba pale ipo tayari, wao wanaleta pesa kidogo kidogo kwa *ZSSF* na baadae ile nyumba itakuwa ni yao. Kwa hivyo miradi ya kutengeneza faida kubwa zaidi wanayo tayari na nimeeleza katika hotuba yangu.

Mhe. Hamza Hassan Juma umezungumzia kuhusu habari ya wale Wamarekani ambao walitaka kuwekeza nyumba. *ZSSF* bado inawafuatilia kwa karibu zaidi. Kila anayetaka kuwekeza kwa kushirikiana na *ZSSF* hasa katika eneo la nyumba, nafasi ipo pana zaidi. Mahitaji ya nyumba ni makubwa zaidi. Bado tunawafuatilia kwa ukaribu zaidi na hata mimi mwenyewe nilipokwenda na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete - Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania nilipata nafasi ya kuonana nao. Kwa kweli bado tunawafuatilia zaidi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nilitakiwa nilitolee ufafanuzi juu ya wananchi wataufahamuje Mfuko wao wa Barabara. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Bikame Yussuf Hamad na wengine.

Mfuko wa Barabara lengo lake ni kukarabati barabara na ndiyo lengo kubwa la mfuko huu. Pale inapojitokeza haja ya kujenga barabara isiyozidi kilomita moja, Mfuko wa Barabara unaweza ukatoa fedha hizo ukajenga barabara isiyozidi kilomita moja.

Katika bajeti ya mwaka huu tuliona kwamba Mfuko huu wa Barabara, barabara ni nyingi zaidi zinazotakiwa kukarabatiwa na hali ya fedha kwa kweli ni ndogo mno. Nilikuombeni Waheshimiwa niongeze shilingi mia moja kwenye mafuta na ninakushukuruni sana muliniongeza shilingi mia moja kwenye mafuta. Nikasema pesa ile ninaipeleka kwenye Mfuko wa Barabara. (*Makofi*).

Lakini kwenye bajeti yangu hii nilikwambieni kwamba kwa sababu sasa hivi tunataka kuwezesha Tawala za Mikoa (Madaraka Mikoani), asilimia ishirini na tano ya zile pesa tutawapelekea Tawala za Mikoa kwa ajili ya barabara zetu za ndani.

Sasa pale ndipo ambapo Mhe. Bikame Yussuf ulipozungumzia. Mhe. Farida Amour Mohammed kwamba barabara hizi za ndani zinatakiwa sasa zijengwe kitaalamu, lakini sasa hivi unachokifanya unaweka kifusi, halafu unaita watoto waweke sawa, maji yakija yanaingia majumbani mwetu. Ndiyo kwa maana tunataka tuwawezeshe Tawala za Mikoa na wao waingie, wawe na wataalamu waweze kutengeneza hizi barabara za ndani na baadae huu Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano waje sasa, panapo majaaliwa *in shaa Allah* waweke lami hizi barabara zetu. Tunakwenda kwa awamu lakini madamu tuna nia, mimi nina imani kubwa sana tufafika. (*Makofi*).

Mhe. Spika, lilikuja suala kwa nini kuna fedha zishatolewa na barabara hazijengwi kupitia Mfuko wa Barabara. Nataka niseme tatizo ni moja tu, kwamba Idara yetu ya Ujenzi wa Barabara tunayoitegemea ina vifaa vichache, inapofika wakati

barabara zinapokuwa nyingi na wao vifaa vyao ni vichache wanalazimika kujenga barabara moja baada ya moja. Lakini tunafanya mazungumzo tuone basi tunaweza tukajaribu kumtafuta *contractor* akatufanyia hizi kazi tukamlipa kwa Mfuko wa Barabara. Hilo tunalifanyia mazungumzo na *in shaa Allah* tumewahi kufanya hivyo na tunaendelea kujaribu kufanya hivyo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa na Mhe. Farida Amour Mohammed ni suala la ucheleweshwaji wa kiinua mgongo. Nataka niseme kwamba hili ni kweli na tunalifanyia kazi na limetokana na sababu moja tu kubwa, watu wetu wanaopata viinua mgongo wanakuwa ni wengi kukidhi makisio. Sasa lazima tuongeze bajeti ya viinua mgongo, tuweze kuiongeza ili tuweze kukidhi kwa wakati. Kiuratatibu wanatakiwa baada ya kustaafu katika kipindi cha miezi mitatu anatakiwa aweze kulipwa. Hilo tutalifanyia kazi tuone tutafikia hatua gani.

Mhe. Farida anilikumbusha tu kwenda naye Pemba pamoja na Waziri wangu wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Nataka niseme tu sijalisahau, nilimuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo twende Pemba, lakini Mhe. Waziri kipindi kile alikuwa na safari na Mhe. Rais kwa kwenda Ujerumani, baada ya kurejea kutoka safari ile na mimi nikawa nipo *busy* hapa siwezi kuondoka humu ndani.

Lakini nataka nikuahidi tu kwamba bado wewe utaendelea kuwa Mwakilishi mpaka atakapokuja Mwakilishi mwengine, na sisi tutaendelea kuwa Mawaziri mpaka watakapokuja Mawaziri wengine, tukimaliza hili Baraza nitamuomba Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo tuweze kuongozana na wataalamu kama tulivyofanya kwa Mhe. Bikame Yussuf Hamad kwenye soko, tutaongozana na wataalamu twende tukawaelimishe zaidi wananchi, ingawa tayari wananchi wetu wameshaelimishwa na Mkuu wa Mkoa na wataalamu wangu wa *ZIPA*, lakini kama unataka na mimi Waziri nikishirikiana na Waziri mwenzangu pale Alhaji Said Ali Mbarouk basi tutakwenda *in shaa Allah*, tutawaelimisha wananchi wetu kwa faida yetu sote. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuhusu *PBZ* hawana *ATM* wanayotumia *visa card*. Ni kweli na ni muda mrefu sana sasa tumekuwa tukitafuta lakini sasa wameshakamilisha utaratibu na ninadhani muda mfupi unaokuja kwa maelezo ya *PBZ*, watakuwa tayari kutumia *master card*. Kwa hivyo hii itasaidia zaidi watalii wetu; Pemba, Unguja, Mashamba, Vijijini kuweza kutoa pesa zao kwa kutumia *ATM*, nayo itawasaidia sana *PBZ* kuweza kuongeza mapato. Kwa sababu kila ukitoa pesa mule ndani unalipa shilingi mia tano, kwa hivyo itawasaidia zaidi. (*Makofi*).

Jengine hapo hapo niliombwa basi niangalie uwekaji wa *ATM* kwenye Baraza la Wawakilishi. Tayari bajeti ya kuweka *ATM* katika eneo hili la Baraza la

Wawakilishi ipo tayari na tunatarajia katika miezi ijayo, kuanzia Septemba hadi Disemba, *ATM* hiyo itaanza ujenzi wake katika Baraza hili la Wawakilishi, naomba mambo yaende sawa kama tulivyoyapanga. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna suala ambalo limezungumziwa sana hapa na wenzangu Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Mahmoud, wametaka nitoe ufafanuzi wa kina juu ya maendeleo ya maeneo huru Fumba na Micheweni. Nataka niseme tu uanzishwaji wa maeneo huru kwa Fumba na Micheweni umeanzia kwa awamu ya Dkt. Salmin Amour Juma. (*Makofi*).

Mwaka 1992 Dkt. Salmin Amour Juma alianzisha taaluma hiyo ya kuwa na maeneo huru. Mwaka 1993 ikawekwa sheria. Kulikuwa kuna sheria tatu katika yote yanasimamia maeneo huru. Lakini baadae mwaka 2004, sheria zile tatu zikaunganishwa ikawa sheria moja ambayo ipo *ZIPA*. Lakini hapa hapa ninataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna, wengi hawajui kwamba huyu alikuwa ni Katibu Mtendaji wa Maeneo Huru na kipindi kile alifanya kazi nzuri sana, mwaka 1990 mpaka 1995.(*Makofi*).

Mwaka 1995 Dkt. Salmin Amour Juma Rais wetu alimteua kuwa Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Uchumi, Mipango na Vitega Uchumi. Kwa bahati nzuri akamteua ndugu yake Omar Yussuf Mzee kuwa Katibu Mkuu wake. Tulifanya kazi nzuri sana, tukatafuta wawekezaji. Kipindi cha kwanza cha Dkt. Salmin Amour Juma Serikali haikuwa na uwezo mkubwa sana wa kuwekeza miundombinu katika maeneo yale, lakini ilikuwa na nia nzuri tu. (*Makofi*).

Kipindi cha pili mwaka 1995/2000, sisi sote humu tuliomo ndani ni mashuhuda tukanyimwa misaada, tukazuiliwa misaada kwa ugomvi wetu wa ndani. Tunamuomba Mwenyezi Mungu asiturudishie tena ugomvi wa aina ile, tusimame pamoja misaada iongezeke na nguvu zetu ziongezeke katika kutafuta mapato yetu.
Kipindi kile lakini Mhe. Waziri Shamuhuna alifuatana na ndugu yake Mhe. Omar Yussuf Mzee, ndugu zetu wa *Star City* kutoka India walikuja wakaanza uwekezaji. Lakini baadae na wao hali yao ikawa mbaya.

Mhe. Rais wakati ule Dkt. Salmin Amour Juma alitutuma mimi na Mhe. Waziri wangu twende mpaka India tukazungumze nao, mbona hawaji kuendeleza. Bahati nzuri sisi sote wawili tupo hai, tukaenda mpaka India kuwauliza, hali zao hazikuwa nzuri, wakatuomba wao wameshindwa kuendelea na sisi huku ndani hali zetu hazikuwa nzuri, tukashindwa, na sisi huku ndani hali zetu hazikuwa nzuri tukashindwa na sisi kuendelea. Kimekuja kipindi cha Dkt. Aman Karume miaka 10 hali ilikuwa nzuri, lakini imeonekana kwamba twende katika sekta nyengine ambazo zitasaidia kuinua uchumi. Tumeelekeza *resources* katika barabara Dkt. Shein amekuja amesema hapana.

Jambo la kwanza tulimtembeza katika maeneo huru. Ndugu zangu wa Micheweni mtakumbuka tulipokuja naye kule maeneo huru, ndugu zangu wa Fumba watakumbuka tulipokwenda naye kina Dkt. Mwinyihaji ndugu zangu wa Fumba kina Khamis Mussa, tulikwenda naye Dkt. Shein kumuonesha, akaona ile hali kwa kweli akasema hapa hatuna maeneo huru, kuna haja ya kuweka mkakati maalum katika kipindi hiki cha miaka mitano, kazi za maeneo huru zianze kuonekana. Kazi za maeneo huru zimeanza kuonekana.

Mhe. Spika, kwanza ndugu zetu wa *ZIPA* wameandaa mpango mzima wa matumizi ya ardhi hekta 3,000 kwa upande wa Fumba.

Jamani ni lazima tukubali, unapokuwa huna nyenzo za kutosha ni lazima ufanye kidogo kidogo, ili ukue uende na kwengine. Mpango ule wameshauandaa tayari, wametenga hekta 1,200 kwa ajili ya uwekezaji binafsi, hekta 950 kwa ajili ya makaazi ya vijiji, na hekta 800 kwa shughuli mbali mbali za kijamii.

Kwa hivyo, kwanza wameandaa mpango tu, *master plan* ya Fumba, huwezi kuingia pahala bila ya kuwa na *master plan*. Wameandaa *master plan*, sasa hivi *master plan* ipo. Lakini nini walichokifanya sasa hivi, wametoa miradi.

Imezungumziwa hapa kwamba kuna mradi wa Kiwanda cha Maziwa, wamechukua hekta 7 ule mradi uko pale. Mradi huu thamani yake ni dola 12 milioni. Lakini vile vile wametenga hekta 700 kwa ajili ya Fumba *Satellite City*.

Wakati ule tulikuwa tuna Mhe. Ali Juma Shamuhuna, tulikuwa tuna *Star City*, sasa ni Fumba *Satellite City*. Tayari kampuni moja *Union Developers* wanaandaa sasa hivi, michoro na *master plan* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu; barabara, maji, umeme na tunafanya kazi hizo kwa fedha zetu za ndani. *(Makofi)*

Mradi wa tatu ni mradi wa ujenzi wa mji mdogo wa kisasa, tumewakatia hekta 55. Mhe. Spika, nitakuomba sana tukimaliza Baraza lako Tukufu hili, kabla hawa Wajumbe hawajatawanyika, nataka nilete basi mbili, ofisi yangu itakodisha basi mbili niwapeleke wote Fumba, wakaangalie maendeleo yanavyokwenda Fumba, nataka niombe hilo. Kwa sababu Mhe. Spika, wakati mwengine tunakaa sisi hapa haya mambo hatuyaoni, kuna *illusion* tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, huu mji mdogo tutajenga nyumba kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka Ujerumani, na tayari wameshajenga nyumba mbili *as a demo*, wameziweka pale, za kisasa kabisa, nyumba za bei nafuu wameshazijenga pale twendeni. Mimi nimekutana nao hao Wajerumani na nimeongea nao, nikawapa *blessing* yangu *they should go ahead*. *Focus* yetu ni *Diaspora*. Vijana wetu waliopo nje watakuwa na nafasi ya kununua nyumba.

Mhe. Spika, mradi mwengine ni uanzishwaji wa eneo la viwanda tumeliita *Industrial Park* hekta 100. Tayari *ZIPA* inafanya mazungumzo na wawekezaji ili kuja ku-*develop* na kuweka hayo maeneo ya viwanda.

Mhe. Spika, *Conventional Centre* wamepewa hekta 60 huo ndio ule mpango wa mwanzo ambao tumepanga. Wizara yangu, *ZIPA* na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko sasa hivi tunashirikiana kutafuta fedha kwa ajili ya mradi huu.

Mhe. Spika, ninachotaka kusema sasa hivi kuna lami tumeshaishusha iko maeneo huru pale Fumba, kuna vyombo vinakata ile miamba pale tunataka kutia lami barabara zile za mzunguko, halafu baadae tuingie barabara za ndani. Nikisema hivi mtaona kama kuna miujiza miujiza, lakini nataka nilete basi mbili, Katibu Mkuu Khamis Mussa ameshanisikia, tukimaliza hapa basi mbili tunawachukueni mwende Fumba mkaone maendeleo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali ni endelevu. Nazungumza tena serikali ni endelevu, ikiondoka serikali hii inakamata serikali hii.

Serikali ya awamu ya Dkt. Shein inaongozwa kwa mfumo wa Umoja wa Kitaifa imefanya kazi kubwa sana, na tutaendelea kufanya kazi kwa pamoja ili tuone kwamba maeneo huru haya ya Fumba na Micheweni, kama nia tulivyoiweka mwanzo na sheria basi tunafanikiwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilitakiwa unipe nafasi ya kutosha nitoe maelezo haya, na nimeshayatoa na nadhani inatosha. *(Makofi)*

Uwekezaji wetu kwenye visiwa vidogo vidogo. Mhe. Hamza Hassan mimi nataka nikubaliane na wewe. Sioni hasa *contribution* yake *to our economy*. Wale wawekezaji waliowekeza katika hivyo visiwa vidogo vidogo bado hawajatusaidia. Sina maana yoyote, nasema kama ni Waziri ninayesimamia fedha, ninayetaka mapato, nasema bado wale hawajatusaidia chochote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini hili tumeshaliona serikalini, na tumetoa kazi kwa *ZIPA* waifanye na ninaamini kwamba *ZIPA* iko katika hatua za mwisho, baadae italeta wizarani hiyo kazi na hatimaye tuirudishe tena serikalini ili tuweze kufanya maamuzi. Lakini hatuwezi kutoa visiwa vidogo vidogo, kwa wale waliotembea Maldives utaona thamani yake, kisiwa kimoja kina-*contribute* kiasi gani katika uchumi wa Maldives.

Sisi leo mtu kawekeza pale kiji-*restaurant*, halafu anatwambia kwa mwezi anachangia dola 1,000 katika uchumi wa Zanzibar, haiwezekani jamani. Tutalifanyia kazi Mhe. Hamza Hassan, nakuomba utulie. *(Makofi)*

Kuhusu Kiwanda cha Maziwa na wafugaji wetu. Nadhani kuma Mheshimiwa mmoja amenisaidia sana, Mheshimiwa baba yangu kule Maalim Saleh Nassor, alisema kazi nzuri inafanywa na mwekezaji Bakhressa. Ananunua maziwa kutoka kwa wananchi, lakini hayatoshi, na ndio maana tumemruhusu aingize maziwa ya unga, aongeze na yale. Lakini lengo lake ni kuwasaidia wafugaji, kuwapatia ng'ombe ambao watakaozalisha lita nyingi za maziwa kwa siku, ili kiwanda kile mali ghafi iweze kupatikana Zanzibar. Hilo ndio lengo lake, na sisi kwa upande wetu tukishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Kilimo na Maliasili tunamsaidia sana, na Mwenyezi Mungu atamsaidia ili lengo lake liweze kufanikiwa. Vile vile ulitaka suala la Kiwanda cha Kibiriti. Kweli hata mimi mwekezaji huyo alikuja kuniona, nilimwambia asubiri kidogo tumalize bajeti ili tuweze kukaa sisi *ZIPA* na watu wa Mazingira.

Mwanzo dhana yake na mimi nilifikiria kwamba atatumia miti kupata zile njukuti. Akaniambia *no*, hatotumia miti kupata njukuti...

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tunatoka nje lakini sio muda mkubwa Mhe. Waziri atamaliza, na hoja hii itabidi iamuliwe tukiwa na akidi ya kutosha.

Niwaombe basi Wajumbe wanaotoka nje warudi haraka na walioko nje pia warudi ili tumalize kazi. Mhe. Waziri endelea.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Kwa hivyo, tukimaliza nadhani bajeti hii, tutamtafuta mwekezaji yule tukishirikiana na wewe ili tuweze kukaa naye, tuone tunamsaidiaje katika kuwekeza. Mhe. Spika, ni kweli Kiwanda cha Vibiriti kitaweza kuzalisha ajira nyingi sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, amesema tupunguze madeni. Mimi nakubaliana na yeye.

Mhe. Fatma kasema kwamba je, tunao wataalamu wa kutathmini mali za serikali. Tumeajiri wataalamu, ambao wanatusaidia kutathmini mali za serikali baada ya kuwa-*identify,* na mawizara yetu na ndio maana katika wizara tano za mwanzo tumeweza kupata thamani ya zile mali zetu.

Mhe. Marina Joel Thomas alitaka *ZSSF* pale ambapo mwanachama ameugua wamsaidie basi kupata mafao yake. Hili ni wazo zuri nakubaliana na wewe, hivi sasa tumefanyia marekebisho sheria ya *ZSSF*, kutakuwa kuna sehemu fulani ya mafao yake anaweza akasaidiwa yule mtu ambaye amepoteza ajira. Lakini lengo la mfuko huu ni kumsaidia mwanachama pale atakapofikia umri wa kustaafu, *this is not a bank,* hii sio benki. Lakini hilo wazo tumelipokea na katika marekebisho ya sheria mpya ya *ZSSF* wazo hilo tunalo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi pamoja na Mhe. Hamza Hassan, waliitaka Bima kutoa huduma za afya, Zanzibar *Insurance*.

Mhe. Spika, nataka niseme hivi serikali iliunda Kamati na ikalijadili sana suala hili, kuhusu utaratibu mzima wa kuanzisha Bima ya Afya. Tumeandaa mshauri yupo, amesikiliza hoja zetu, amesikiliza hoja za wadau, na hivi sasa mshauri ameshatoa ripoti yake iko kwenye kamati, kamati wanaipitia na baadae itakwenda serikalini. Lakini Bima wao wako tayari kufanya kazi hiyo kama watapewa, lakini wanasubiri taarifa ya serikali.

Mhe. Spika, hoja nyengine ambayo Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi amesema kwamba Chuo cha Chwaka kipatiwe fedha ili kiweze kutoa wataalamu wengi zaidi. Ombi hili nimelipokea na tutashirikiana kwa karibu zaidi na kuwapatia fedha ili waweze kutoa wataalamu wengi zaidi. Vile vile amesema elimu zaidi itolewe juu ya dhana nzima ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Hii tunatoa na tutawaambia wenzetu wa *ZSSF* waendelee kutoa elimu zaidi.

Mhe. Saleh Nassor, Mhe. Mahmoud Muhammed, Mhe. Abdi Mosi walizungumzia juu ya kuharibiwa kwa barabara hasa kwa hawa ma-*contractor*, wakapendekeza kwamba asilimia 10 ya gharama ya ujenzi watozwe ili iende kuchangia kurekebisha barabara.

Nataka niseme tu, ukiiweka hiyo kwa Mkandarasi, Mkandarasi atairudisha serikalini atakuchaji wewe mwenyewe, isipokuwa tuwabane wazirudishe barabara zetu katika hali iliyokuwa. Wanapoanza kutumia kwenda kuchimba vifusi basi waziangalie barabara zilivyo, na watakapomaliza wazirudishe, lakini wazo la kuwaongezea mfuko fedha zaidi kama nilivyolieleza tumelipokea.

Mhe. Spika, pia aliuliza daraja lile la Vitongoji. Ni kweli mfuko unatengeneza daraja kama kuna matengenezo madogo ya daraja ndogo ndogo kama zile, na tayari daraja hili limo linafanyiwa sasa hivi upembuzi na baadae litarekebishwa daraja hilo.

Mhe. Spika, Mhe. Abdi Mosi alisema kwamba barabara ya kutoka Mjini kuelekea Kaskazini ni mbovu. Nataka nikwambie tu, barabara hizi mbili tunazitafutia fedha sasa hivi. Barabara ya kutoka Mjini /Kaskazini/ Nungwi, barabara ya kutoka Mjini/Makunduchi, na tayari tumeshaomba kupitia Serikali ya India, mambo yatakapokuwa mazuri *In shaa Allah* barabara hizi zitafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, *ZIPA* inaelekeza juhudi zake kwenye utalii tu Mhe. Saleh Nassor. Nataka niseme *ZIPA* inaelekeza juhudi zao katika maeneo mengi sana. Katika utalii, kilimo, kuwavutia viwanda. Lakini wale waliokuja mwanzo ni wale ambao

wanataka kuwekeza kwenye utalii, lakini utaona sasa hivi viwanda vitaanza kuja pale viwanda vidogo vidogo, na nitawaombeni vile vile Waheshimiwa Wajumbe katembeeni, viwanda vidogo vidogo kuna viwanda vipya mule ndani vimeanzishwa vimo mule ndani. Kwa hivyo, *ZIPA* wanajitahidi sana kuvutia wawekezaji wa aina zote, lakini *In shaa Allah* wale ambao wa hoteli, kwa sababu fedha zinazopatikana na hoteli za haraka zaidi kuliko katika maeneo ya viwanda, ndio maana wale wa utalii wanakuja haraka zaidi, lakini tutajitahidi. Vile vile ulitaka kujua kama ile hoteli iliyoko chini ya bahari kama tumeifanyia *EIA*. Tumeifanyia, hakuna mradi wowote ambao unaruhusiwa kuekezwa nchini bila ya kuwa na *Environmental Impact Assessment.* Hiyo ni lazima ipatikane ile *certificate* yake, tujue kwamba hauna athari mradi huo, ndio turuhusu uweze kuwekezwa.

Mhe. Spika, bahati nzuri Zanzibar ni nchi ya tatu duniani kuwa na chumba kilichoko chini ya bahari, na chumba kile kimetutangaza sana sisi, kwenye *CNN* tumeshatangazwa, kwenye televisheni mbali mbali za Arabuni tumeshatangazwa kwa chumba kile.

Chumba kile katika mwaka kinakosa wiki moja tu *booking* na kwa sababu wanakifanyia matengenezo. Lakini *throughout the year* hoteli ile imejaa, kwa sababu hiyo kwamba ni hoteli nzuri moja imewekezwa katika kisiwa chetu cha Pemba. Tunawaomba wengine waje wajitokeze kuwekeza vitu vizuri kama vile.

Mhe. Spika, kuhusu *PBZ* iongezewe mtaji. *In shaa Allah* hili suala tutaliangalia katika mkutano wa wadau. Wiki iliyokwisha nilizungumza na *Managing Director* nikamtaka aitishe kikao cha wadau, ili tuje tuzungumze kwa kina suala hili. Kuna *option* nne atakujanazo katika mkutano wa wadau na baadae na sisi tutazipeleka serikalini, *option* nne za kuweza kuwaongezea mtaji.

Kuhusu *PBZ* iwe na *mobile ATM*. Ushauri mzuri na wakati ule ulipokuwa kwenye Bunge la Katiba Mhe. Saleh baba yangu, ulipokuwa kwenye Bunge la Katiba wakati ule uliona ile *mobile ATM*. Kwa hivyo, na wao tutawashauri basi wawe nayo hii angalau ya kuzunguka zunguka mule vijijini watu wanataka kuchukua pesa, kuweka, watumie hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu ahadi za Mhe. Rais, Mhe. Bikame Yussuf. Hili tutalichukua, wapo watu ambao wanaratibu ahadi za viongozi. Mhe. Rais, Makamu wa Kwanza, Makamu wa Pili ili zote ziweze kutekelezwa kwa kipindi muafaka.

Suala hili nimelichukua na nitawatafuta wanaoratibu, Mhe. Waziri anayeshughulikia Ikulu yupo hapa, na yeye tutaliongelea ili tuone ni jinsi gani hii ahadi ya Mhe. Rais itakavyotekelezwa.

Mhe. Spika, kuhusu Shirika la Bima Pemba. Mhe. Hassan Hamad alitaka kujua hawana jengo hawa. Ni kweli wameomba jengo wauziwe. Tulizungumza na Wizara ya Majenzi, mwelekeo utakuwepo mzuri tu wa kuwauzia hilo jengo, wao wako tayari wauziwe walikarabati, ili baadae walitumie kama ni jengo la Bima.

Taasisi ya Bima ni taasisi ya serikali, na lile jumba ni jumba la serikali. Kwa hivyo, tukiwapa wao wakilikarabati wakilitumia kama ni ofisi, bado litakuwa ni jumba la serikali. Kwa hivyo, hilo tunaliangalia na tumeshaanza kulifanyia kazi.

Vile vile kuhusu maslahi yao. Juzi nimepokea barua kutoka Tume ya Utumishi wameniambia wanalifanyia kazi, na muda mfupi nafikiri watanijibu maslahi yao yamefikia wapi.

Mhe. Mahmoud umeniuliza kuhusu habari ya *database* moja na hapa Mhe. Spika, naomba nitulie kidogo nieleze. Maana yake na yeye alikuomba unipe muda kidogo, sitatumia muda mwingi lakini nieleze. *Database* moja ina faida kubwa sana.

Mhe. Spika, nawataka wale wenzangu Wawakilishi wanaofanya biashara wanisikilize. *Database* moja ina faida kubwa sana, kwa maana bei itakayokuweko Zanzibar ndio ile ile itakayokuweko Bara kwa kitu hicho hicho. Kwa mfano kama umeagiza trekta aina fulani. Kama ushuru utakaokuweko Zanzibar ndio ule ule utakaoonekana Tanzania Bara, lakini nimewaambia wenzangu na nitaendelea tena kuwaambia.

*Database* hii faida yake kwa wafanyabiashara itakuwa wanaweza kuagiza mizigo yao na kuisafirisha kupeleka Bara bila ya bughdha tena, kwa sababu alicholipa yeye hapa ndicho alicholipa yeye mwenzetu kule, isiwe kuna bughdha, kwanza tuhakikishiane hapo.

Jambo la pili, nilisema kwamba *Database* hii itakuwa ina maana kama itakuwa ni *automatic,* yaani kama itakuwa inakwenda bila ya mtu kuitia vidole. Kama kutakuwa kuna mtu kule anachezea *Database* kwa kuingiza *entry* kwa vidole basi hiyo *database* itakuwa haina maana yoyote. Sijui kama nimefahamika? Kwa hivyo nimetoa mfano nimesema watalamu waende Singapore. Singapore kule unaleta mzigo wako unakwenda na *entry* yako unatia *data* zako mashine inakupa *bill* yako, unajua kiasi gani unakwenda kulipa, unakwenda kulipa benki unakuja na risiti yako unatia namba zako inakupa *Certificate* ya kwenda ku-*clear* mzigo wako, hakuna uso unaokutana nao, lakini kama unakutana na uso *database* itakuwa haina maana ya pamoja.

Sasa nawaachia kazi wenzangu wa Muungano na *TRA,* mimi nimeshawaambia faida ya *database;* moja, Wafanyabiashara wa Zanzibar hawatabughudhiwa watapeleka bidhaa zao kule wakatumie soko. Lakini kama itakuwa inachezewa chezewa hiyo itakuwa haina maana na *database* moja. Sasa hapa ndipo ninapofikia, kwa hivyo Mhe. Mahmoud nilikuwa nakata na Waheshimiwa wengine mufahamu umuhimu wa *database,* lakini munatakiwa mwende vipi. Tumezungumzia dhana ya *one stop centre* Mhe. Mahmoud sasa hivi mambo yanakwenda vizuri, kwa sababu *one stop centre* ina taasisi kama tatu mpaka nne hivi inazihitajia wawepo pale.

Kwanza maafisa wa Uhamiaji wawepo, maafisa wa Kazi wawepo, maafisa wa Mazingira wawepo ili kuweza ku-*facilitate* ule mradi uweze kuharakishwa, sasa hivi inachukua wiki moja tu *residence permit* inatoka wiki moja tu, *working permit* inatoka. Tumepiga hatua sana sasa hivi, na tumejaribu kuitengeneza bodi yetu ya *ZIPA* iwe ina watu ambao wenye dhamana, Tawala za Mikoa anaingia Naibu Katibu Mkuu kama ni Mjumbe, Ardhi anaingia mwenyewe Katibu Mkuu kama ni Mjumbe wa bodi ya *ZIPA* ili kuweza ku- *facilitate* wawekezaji wasiwe na matatizo. Kwa hivyo sasa hivi tuko katika hatua nzuri.

Mhe. Spika, Mhe. Mahmoud alitaka kuelewa jinsi ya mkaguzi wa ndani utaratibu wake upo vipi na upatikanaji wa taarifa zake. Huyu mkaguzi wa ndani lengo lake kubwa ni kumsaidia Katibu Mkuu, mkaguzi wa ndani anatazama zile hati zote ziko *okay, prepayment* kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria, halafu anampelekea Katibu Mkuu kumshauri, anamwambia hapa na hapa hapakukaa vizuri, Katibu Mkuu wajibu wake sasa kuita taasisi zake kurekebisha ili kabla ya mkaguzi wa nje hajaja. Unapoihitajia hii ripoti ya mkaguzi wa ndani kwa sasa inabidi uende Wizara moja moja kwa Katibu Mkuu ndio mwenye dhamana ya mkaguzi wa ndani.

Mapato yanayotokana na Mashirika ya Muungano ni kweli yapo mashirika ya Muungano kama *BOT* tunapata gawio, lakini yapo mashirika ya Muungano bado hayajaanza kutoa gawio, tumeanza kuzungumza na mashirika hayo kupitia Wizara mama Wizara ya Fedha, lakini na sisi vile vile tusisahau tuna wajibu wa kuchangia shughuli za Muungano, kwa hivyo tunakuwa tunakwenda huku na huku, lakini niamini kwamba hata haya hayakuchukua muda mfupi, yalichukua muda kidogo. Tunachokifanya ni kujenga hoja ili hoja zetu zikubalike na wenzetu, sio kuvutana, kuvutana hakutoleta faida yoyote. Kwa hivyo hili nalo lipo tunalifanyia kazi ingawa bado kuna mashirika mengine bado hayajaanza. Shirika la Posta vile vile tuna ubia mle ndani inapopatikana faida tunapata. Inaposema sasa faida hii tuongeze mtaji tunaongeza mtaji, umetaka nielezee juu ya kampuni ya *ZANTEL* kweli imeuzwa au inaendelea na kazi zake Zanzibar.

Mhe. Spika, nataka niseme hili ili lifahamike kwa wananchi, *ZANTEL* haijauzwa, narudia, *ZANTEL* haijauzwa, narudia, *ZANTEL* haijauzwa. Katika *ZANTEL* kuna wabia wawili tu ndio waliobakia; kabakia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na *Etisalat*. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina *share* asilimia 15 na Etisalat Shirika la simu la *UAE* ina *share* asilimia 85. Yule mbia wa pili kasema jamani ee mimi hii biashara basi nataka kuuza *share* zangu, huwezi ukamzuia, hata wewe ukiwa na mwenzako mbia ukisema unataka kuuza sehemu yako hawezi kukuzuia.

Na sisi kama Serikali tumekaa vikao mbali mbali tumekubali Etisalat anataka kuuza *share* zake tumekubali, tungekuwa tuna uwezo mkubwa tungezinunua sisi zile *shares,* lakini hatukuwa na uwezo huo, lakini Mhe. Spika, unapouza *share* zako unauza *assets and liabilities* ndio utaratibu wa soko, ukiuza unauza *assets and liabilities,* kwa hivyo yule kauza madeni yake na mali zake.

Na nataka niseme tena aliyenunua sio *TIGO,* aliyenunua ni kampuni ya Millicom. Kampuni ya Millicom inamiliki kampuni ya *TIGO,* kwa hivyo sasa kampuni ya Millicom atakuwa na *shares* kwenye *ZANTEL*, *ZANTEL* itaendeshwa kama *ZANTEL,* na itabakia Zanzibar kama *ZANTEL,* na itabakia Makao Makuu yake Zanzibar, na italipa kodi zake Zanzibar, tumeshakubaliana na wenzetu wataongeza mtaji kuifufua zaidi *ZANTEL,* sisi tumewaambia sisi hatuna fedha za kuongeza, wao wataongeza wataisaidia Serikali ili tuendeshe biashara yetu ya *ZANTEL* yetu.

Mhe. Spika, hoja zilikuwa nyingi nataka niseme kwa kumalizia kwamba wale wote ambao hoja zao nimeshindwa kuzijibu sio kwa sababu sikutaka, ni kwa sababu nimezipokea na nitazifanyia kazi, nina miezi kama mitatu mpaka minne ya kuwepo ofisini, na nitazifanyia kazi kwa kushirikiana na wale wenzangu wote ambao nimewaomba tushirikiane.

Mhe. Spika, naomba nimalizie basi kama kawaida yangu namalizia kwa kukushukuru wewe Mhe. Spika, namshukuru Naibu Spika, nawashukuru Wenyeviti wote wa Kamati zote, nawashukuru Wajumbe kunisaidia miaka mitano hii. Haikuwa kazi nyepesi kuwasilisha bajeti ya Taifa haikuwa kazi nyepesi, siku zote roho yangu walikuwa wanaiweka juu, lakini mumenisaidia nimeweza kumalizia salama usalimini.

Namshukuru pia Mhe. Rais kwa kuniamini katika kipindi chote cha miaka mitano, na mimi nawashukuru watendaji wangu wote wa Wizara ya Fedha kwa kuniamini kuwa nao, inawezekana tumekwanyuana hapa na pale, lakini tusameheane, ndio binadamu alivyo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Spika, kama kawaida yangu namshukuru sana mke wangu bibi Nariman Nassor Mohammed Aboud, kwa kuniruhusu kuwepo hapa bila ya bughudha na hasa katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani.

Nawashukuru pia watoto wangu kwa kunivumilia. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaokubaliana na hoja za Wizara hii ya Fedha kwa mwaka 2015/2016 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.
Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**FUNGU F01 - WIZARA YA FEDHA**

Kifungu 02 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa ufafanuzi wake wa masuala mbali mbali ambayo niliyomuuliza.

Nilijenga hoja kumi na nne, Mhe. Waziri amenijibu hoja kumi, kwa hivyo kwa kweli amejitahidi sana na nampongeza sana. Sasa kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba kutokana na muda hakuweza kujibu yote, nilikuwa nataka ufafanuzi kwa eneo la uongezaji wa Bandari ya Mpigaduri katika uwekezaji unaoendelea kuwekezwa pembeni pembeni ya eneo lile, ambalo tunategemea baada ya kupatikana uchumi mkubwa sana wa Zanzibar wa gesi na mafuta, tunategemea Bandari ile itajengwa na itakuwa kubwa, na inawezekana baadae na maeneo mengine yakaja yakakopwa pale au yakanunuliwa kwa ajili ya kuendeleza ile biashara.

Sasa hili Mhe. Waziri inaonesha, kwa sababu alinijibu yale ya Micheweni, Fumba tumeridhika, lakini hili kidogo hatukupata ufafanuzi. Sasa Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako, kwa sababu nilikuwa na hoja kama tatu, sasa kama nitaweza

kuzisema zote kwa pamoja ili akinijibu tena nisifanye tafrani ya kuzuiazuia vifungu, nafikiri uniruhusu kufanya hivyo. Sasa hoja zenyewe halafu sio kubwa. Kuna hoja moja ya *PBZ*…

**Mhe. Mwenyekiti:** Labda tungeelewana kwanza unakusudia una matatizo kwenye haya mapato, maana haya mapato tunayopitisha hivi sasa tunakusudia ayakusanye afanyie kazi mbali mbali, pengine tunakuja na hiyo Mpigaduri, una matatizo nayo mapato haya.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Kimsingi lile eneo tunategemea litakuwa la mapato ya Serikali tena makubwa sana, lakini namna ya uendelezaji wake sasa hivi naona kidogo kama kuna kitu ambacho kitakuja kusababisha Serikali kuingia hasara kubwa kulipa *compensation,* ndio maana nikaamua kuzuia hapa, *otherwise* labda kama utanambia tusubiri kwenye Uendeshaji, lakini nahisi...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mimi nadhani usubiri kwenye Uendeshaji.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Sawa nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

| | |
|---|---|
| Kifungu P02 Idara ya Mipango Sera na Utafiti | Shs. 5.232,779,500 |
| Kifungu P03 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | Shs.51,000,000,000 |
| Kifungu P04 Idara ya Fedha za Nje | Shs.349,876,154,000 |
| Kifungu P05 | |

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ambayo Mhe. Waziri ameyatoa juu ya suala zima la *ZANTEL,* na sisi bado tukiwa tuko katika *dilemma,* lakini labda ningelimuomba tu Mhe. Waziri anisaidie sasa hii asilimia 15 ambayo ni yetu, kwa sababu tayari tumekwisha kupata mume mwengine, sio kuliko yule wa mwanzo ambaye tulikuwa naye, sasa na huyu mume mwengine hatumjui yukoje. Je, katika kufahamu thamani ya fedha ambayo tuliyonayo ni thamani gani ya hii asilimia 15 ambayo tunayo katika kampuni hii ya *ZANTEL,* kwa sasa *at least* ile thamani yake tu tuijue.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba hii ni biashara kuna baadhi ya mambo hapa ukija ukiyaweka wazi na yeye ana wenzake anashindana nao, namuomba basi Mhe. Mahmoud kama anataka kujua thamani ya ile basi tuweze kukaa halafu niweze kumfahamisha thamani yake, si vizuri kuanza kuitaja hapa kama ni ile.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti nakubaliana na hoja yake na *In shaa Allah* hiyo siku atakayonialika atanipa taarifa kamili juu ya suala hili. Ahsante Mheshimiwa *(Makofi)*

| | |
|---|---|
| Kifungu P05 Idara ya Uhakiki mali na Mitaji ya Umma | Shs. 6,650,000,000 |
| Kifungu P011 Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB)* | Shs.225,943,922,000 |
| Kifungu P12 Idara ya Forodha (*TRA)* | Shs. 113,822,086,000 |
| Kifungu P13 Idara ya Kodi za Ndani (*TRA)* | Shs. 64,717,696,500 |
| **Jumla Kuu** | **Shs. 817,242,638,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU P 01 - PROGRAMU YA USIMAMIZI WA BAJETI NA FEDHA ZA UMMA**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Programu Ndogo ya Mfumo na Udhibiti wa Ulipaji | Shs. 26,221,397,000 |
| Kifungu S02 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali | Shs. 15,588,241,000 |
| Kifungu S03 Programu Ndogo ya Ufuatiliaji na Uratibu wa Misaada kutoka Kwa Washirika wa Maendeleo | **Shs.** 1,787,678,000 |
| **Jumla ya Fungu** | **Shs. 43,587,316,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P02 -PROGRAMU YA USIMAMIZI NA UWEKEZAJI WA MALI ZA UMMA**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Programu ndogo ya Usimamizi wa Mitaji ya Umma | Shs. 2,151,209,000 |
| Kifungu S02 Usimamizi wa Manunuzi na Uhakiki wa Mali za serikali | Shs.99,472,000 |
| **Jumla ya Kifungu** | **Shs.2,250,681,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KIFUNGU P04 PROGRAMU YA MIPANGO NA UENDESHAJI WA SEKTA YA FEDHA**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Utawala na Uendeshaji wa Wizara | Shs. 5,281,501,000 |
| Kifungu S02 | |

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kuniongoza kabla sijaendelea na lile suala langu nilikuwa kidogo sikubaliani na ile hoja ya Mhe. Saleh mkwe wangu aliyosema nafuta *hansard* yangu, kwa sababu nilitumia Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 88, ibara ndogo (c) ambayo inanipa mamlaka ya kuiuliza maswali mbali mbali Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, ile *hansard* yangu bado haikufutika, lakini nashukuru kwa majibu ya Mhe. Waziri. Sasa nafikiri Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa nilikwishatoa maelezo kuhusu zaidi uendelezaji wa eneo la Mpigaduri, na namna sasa hivi linavyoendelea kutumikatumika na kuogopa hasara ya serikali baadae.

Kwa hiyo, labda Mhe. Waziri kuhusu suala la uendeshaji eneo la Mpigaduri labda anisaidie maelezo. Yale masuala mengine kwa sababu moja liko katika Mipango naweza nikalizungumza kabisa suala la stahiki za wale wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, bado wanaendelea kudai haki zao, hili bado hatujalipatia ufumbuzi.

Sasa hili jengine lilikuwa kuhusu Benki ya Watu wa Zanzibar kuendelea kukodi, hili kama utaniruhusu Mhe. Mwenyekiti utamruhusu Waziri alijibu kabisa au nije nizuie fungu la *PBZ* kutaka ufafanuzi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuweza kujenga jengo lao, lakini akinijibu yote kwa pamoja nitakuwa nimeridhika.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Hamza ni kweli aliyauliza haya maswali matatu lakini kutokana na muda na majawabu nilikuwa ninayo.

Suala la bandari ya Mpigaduri serikali imeshakamilisha taratibu zote, imeshaandaa *feasibility study*, imeshaandaa *Environmental Impact Assessment Report*, barua ya mkopo kutoka Serikali ya Jamhuri wa Tanzania hivi sasa taarifa zote hizo zimeshawasilishwa Benki ya *Exim* ya China pamoja na Wizara ya *Commerce* ya China kwa-*approval*. Tunatarajia mambo yakienda vizuri basi *in shaa Allah* pengine mwaka huu tunaweza tuka-*sign* hatua za mwanzo.

Kwa hivyo, hilo lipo, na pale ambapo tunapotaka kujenga bandari hadi sasa sijaona *compensation* ambayo itakayojitokeza katika eneo lile. Lakini kama kutakuwepo na *compensation* yoyote ile basi serikali itakuwa na wajibu wa kuwa-*compensate* wale wananchi walioko pale ili bandari iweze kujengwa. Na tunatarajia kama mambo yatakwenda vizuri ujenzi wa bandari unaweza ukaanza mwanzoni mwa mwakani.

Pili stahili za wafanyakazi wa Afrika Mashariki, kwa sababu wizara yangu Mhe. Mwenyekiti haisimamii wafanyakazi wa Afrika Mashariki, lakini kwa sababu nina ushirikiano mzuri na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atuachie Mhe. Hamza anipe kumbukumbu zote, tuweze kujua ni wafanyakazi wa aina gani na kumbukumbu zao, na ninamuahidi nitazifikisha kwa Mhe. Waziri wa Fedha wa *URT*, kwa sababu na mimi nilipokuwa kule kama Naibu Waziri hili ni eneo moja nililokuwa nikishughulika nalo, najua jinsi ya kushughulika nalo tutamsaidia.

Suala la *PBZ* ni kweli aliliuliza Mhe. Hamza. *PBZ* hivi sasa wameshapatiwa eneo la Mazizini nyuma ya Wizara ya Elimu tayari sasa hivi wanatafuta Mshauri Elekezi ili aanze kazi ya kuchora michoro, na hatimaye kuipitisha michoro ile katika *stages* mbali mbali; katika mkutano wao wa Bodi, *shareholders meeting* halafu tuipeleke serikalini, tunatarajia kazi hiyo ikimalizika tu *PBZ* watakuwa na jengo lao pale. Vile vile *PBZ* wanataka kujenga jengo mbele ya Polisi, ili jengo lile liweze kutumika kwa wateja wakubwa pamoja na wateja wa Mji Mkongwe, wale wa karibu wa maeneo yale. Kwa hivyo, hatua hizo tunazo na wanataka kuondokana na kukodi kwa majengo. Ahsante.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kama nilivyosema namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake na ufafanuzi wake, lakini labda Mhe. Waziri nataka nimuombe anatupunja sana taarifa, kwa sababu haya maendeleo ambayo Mhe. Waziri wanayotarajia kuyafanya basi ni vizuri wangekuwa wanapata muda wanatufanyia kongamano dogo hivi *at least* kutupa yale mipango ya maendeleo.

Unajua sitaki kusema semina, kwa sababu nikisema semina itakuwa inaleta tabu kuja kwenye masikio, lakini alau makongomano ya kuweza kujadili hayo maendeleo. Kwa sababu na sisi pengine tunaweza tukatoa ushauri ambao utaweza kuisaidia vile vile serikali.

Sasa kubwa nililokuwa nataka kusema kabla ya kukaa nilikuwa nawaomba wale wananchi ambao waliokuwa wanatujia, wafanyakazi wa Afrika Mashariki, na wengi wao sasa hivi miaka yao inaendea sitini na zaidi na sabiini na kuendelea, basi Mhe. Waziri ameshatoa kauli kwamba mimi nimpelekee zile kumbukumbu. Sasa na mimi wengine siwajui majumbani kwao, kwa hiyo naomba basi wanitafute ili wanipe zile kumbukumbu zao tumpelekee Mhe. Waziri kwa ajili ya kupata haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naomba tuendelee.

Kifungu S0

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante Mhe. Waziri aliposimama hapa alijitahidi kutujibu baadhi ya hoja zetu pamoja na maoni na masuala yetu, lakini sikumsikia katika suala zima la namna gani *BOT* inasaidia uchumi wa Zanzibar. Suala hili Mhe. Waziri aliposimama sikumsikia akilizungumzia, namuomba anipe majibu katika hili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri maelezo, na kama unataka kusema kitu kuhusu kile kajikongamano alichoomba Mhe. Hamza. (*Kicheko*)

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Mwenyekiti, labda nianze na hilo kongamano. Serikali haina matatizo na kutoa kongamano ili kuelimisha jamii hasa kuwaelimisha Wajumbe wa Baraza la lako Tukufu.

Sisi tuna mpango Wizara ya Fedha Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuapishwa kwa Baraza jipya tuna mpango wa kutoa taaluma ya *PBB* kwa Wajumbe wapya. Sasa nitaomba wataalamu wa benki na wataalamu wengine wa uchumi waje na hapo waweke *paper* zao, ili kwa Baraza jipya nalo kuanza kuliwezesha kitaaluma, hatuna tatizo na hilo, *in shaa Allah* Mungu atujaalie tuwe sote wazima, watakaojaaliwa kurudi salama mmojawapo nikiwa ni mimi vile vile basi tutapata hilo.

Mhe. Mwenyekiti, la pili suala la Mhe. Mahmoud jinsi ya *BoT* kuiwezesha au kuisaidia Zanzibar katika kukuza uchumi wake. Kwanza nataka nimwambie tu kwamba somo hili ni pana sana, lakini nataka nimpe kwa ufupi.

*BOT* kazi yake kubwa kuangalia mwenendo wa uchumi wa nchi na mwenendo wa fedha katika nchi, na kazi yake kubwa nyengine kuishauri serikali maeneo ambayo yakiwekezwa zaidi yanaweza kuleta tija zaidi. Na kazi yake kubwa vile vile kuishauri serikali suala la mikopo iendane na maeneo ambayo yenye tija zaidi, na maeneo mengine ambayo ni kuitahadharisha serikali katika ukopaji wake. Hayo nataka nimuhakikishie Mhe. Mahmoud tuna Wajumbe wetu katika Bodi ya *BOT*, na wao wanapata taaluma hiyo na wanakuja kutusaidia sisi mawaziri ambao wanaosimamia sekta zile.

Kwa hivyo, *BOT* wanatusaidia sana katika maeneo hayo, na ndio maana mkakuta kama kila baada ya muda tunazungumzia kuhusu habari ya *GDP growth*, tunazungumzia kuhusu habari ya *inflation*, kwa sababu wenzetu wanaziangalia kwa undani zaidi katika athari nzima za ukuaji wa uchumi au katika mafanikio ya ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, tunazungumza nao vizuri sana, na wanatusaidia sana katika maeneo hayo.

**Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba tuendelee, nimeridhika na majibu yake.

| | |
|---|---|
| Kifungu S02 Mipango, Sera na Tafiti za Sekta ya Fedha | Shs.19,831,316,000 |
| Kifungu S03 Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba | Shs. 1,238,186,000 |
| **Jumla ya Kifungu:** | **Shs. 26,351,003,000** |
| **JUMLA KUU:** | **Shs. 72,199,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU F02 MFUKO MKUU WA SERIKALI**

**KIFUNGU P01- PROGRAMU YA USIMAMIZI WA MFUKO MKUU WA SERIKALI**

| | |
|---|---|
| Kifungu S01 Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | Shs. 83,928,900,000 |
| **JUMLA KUU:** | **Shs. 83,928,900,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Fedha:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na makadirio haya wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nadhani kwa leo itoshe na tujitayarishe kwa kesho mapema tukiwa tumejaa vizuri, kwa sababu kazi ya kesho sio refu sana itakuwa inahitaji maamuzi; kwa hiyo akidi iwe nzuri sana.

Kwa kawaida baadhi ya Mabunge mengine yanapopitisha *Appropriation Bill* basi huwa mtimie nyote mule ili kuhakikisha kwamba yale matumizi ya serikali mumeyakubali.

Kwa hivyo, tujitahidi kufika kwa wingi ili tuweze kuja kuifanya kazi hiyo kesho mapema, tena wala hakuna maswali inaingia kazi ya kuwasilisha Mswada moja kwa moja, hati zake zimekwishawasilishwa leo, kwa hiyo kesho tunaanza kuweka mezani kusomwa kwa mara ya kwanza, mara ya pili na hatimaye mara ya tatu. Huo ni Mswada mmojawapo ambao unakwenda kwa utaratibu huo, mambo yote haya ya usomwaji kwa mara tatu yanafanyika kwenye mkutano huo huo.

Waheshimiwa Wajumbe kwa hiyo nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mumeifanya, lakini niwaombe wale Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kwamba kile kikao chetu ambacho kilikuwa kiitwe saa nane kitafanyika mara baada ya kuondoka humu ndani. Kwa hiyo, tukutane ukumbi wa juu kuendelea na kikao hicho cha Kamati ya Uongozi.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo basi sasa nasitisha shughuli zetu hadi kesho tarehe 23/06/2015 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 7:38 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 23/06/2015 saa 3:00 asubuhi)*